

**MAKOSA YA KISEMANTIKI KATIKA MAWASILIANO ANDISHI YA KISWAHILI
MIONGONI MWA WANAFUNZI WA SHULE ZA UPILI: MFANO WA KAUNTI YA
KAKAMEGA**

BEATRICE KEMUNTO ARUBA

Tasnifu hii imewasilishwa ili Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada yaUzamili katika
Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Maasai Mara

CHUO KIKUU CHA MAASAI MARA

SEPTEMBA, 2017

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Sahihi-----Tarehe-----

Beatrice Kemunto Aruba

AMOI / K / 6014 / 2012

IDHINI

Tasnifu hii imewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Maasai Mara kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili kwa idhini yetu kama wasimamizi rasmi walioeteuliwa na chuo kikuu.

Sahihi-----Tarehe-----

Dkt. James Omari Ontieri

IDARA YA LUGHA, ISIMU NA UTAMADUNI

CHUO KIKUU CHA MAASAI MARA

Sahihi-----Tarehe-----

Prof. Ernest Sangai Mohochi

IDARA YA LUGHA, ISIMU NA FASIHI

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA RONGO

HATILINZI

Beatrice Kemunto Aruba © 2017

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kupigisha chapa, kutafsiri au kuitoa kazi hii kwa njia yoyote ile bila idhini kwa maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mamangu (Ruth Bosibori Ombaki) na familia yangu, Elijah Aruba Ogoti Omwega (mume wangu), Harriet Jessicah, Bryan Nimrod na Bonventure Willis (watoto wangu) na kwa wataalamu na wanafunzi wote wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

SHUKRANI

Mwanzo kabisa, napenda kumshukuru sana Mola ambaye amenisaidia nakunibariki katika kufanikisha kazi hii.

Kama inavyojulikana mshikamano wa mikono daima hutoa kazi bora. Kwa hivyo mafanikio ya kazi hii yametokana na misaada ya watalaamu mbalimbali.

Kuna wataalamu ambao sina budi kuwataja kutokana na misaada yao mikubwa walijonipatia. Shukrani nyingi ni kwa wasimamizi wangu Dkt. James Omari Ontieri na Prof. Ernest Sangai Mohochi kwa juhudzi zao katika kusimamia na kusahihisha kazi hii hadi kufikia upeo. Aidha, kwa kunipa moyo ulioniwezesha kuifanya kazi hii kwa subira kubwa.

Aidha, ningependa kukishukuru Chuo Kikuu cha Maasai Mara kwa jumla, na hasa, Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Kijamii kwa ushirikiano mzuri ulioniwezesha kufanikisha kazi hii.

Shukrani zangu maalumu ni kwa wahadhiri wangu walionifundisha Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maasai Mara, hususani Dkt. Nancy Ayodi Mokaya Pamoja nao, napendakumshukuru Dkt. Julius Gekonde Mkurungezi Mkuuwa E-Smart Technical College nanaibu wake Bi. Josephine Nyamwange kwa ushauri wao walionipa na kunitia moyo kuendelea na masomo yangu katika Chuo Kikuu cha Masaai Mara. Pia, namshukuru Dkt. Simiyu Kisurulia kwa kushirikianana wasimamizi wangu ili kuniwezesha kumaliza kazi hii.

Mwisho kabisa, shukrani zangu ni kwa wote waliojihushisha kwa hali moja au nyingine ili kufanikisha kazi hii, Mungu awazidishie wote.

IKISIRI

Kimsingi, lugha inawezesha na kuendeleza mazungumzo katika jamii. Lugha hii hujitokeza katika mazungumzo na maandishi. Mawasiliano andishi yanatakiwa kufanywa kwa uangalifu mkubwa ili kukamilisha gharadhi lake katika jamii. Ilivyobainika ni kwamba pasipo lugha, mawasiliano kama shughuli kuu ya kibinadamu hayatafaulu. Ingawa makosa mbalimbali yanayopatikana katika kazi za wanafunzi yametambuliwa na kuchanganuliwa na wataalamu mbalimbali, bidii hazijafanywa katika kubainisha makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili kwa kina. Lengo kuu la utafii huu ni kuchanganua makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili mionganoni mwawanafunzi wa shule za upili katika kaunti ya Kakamega. Utafiti huu umeainisha makosa yaliyojitokeza katika matini za wanafunzi wa shule za upili; kubainisha vyanzo vya makosa husika na kupendekeza mbinu mwafaka za kuyapunguza. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa pamoja na Nadharia ya Sarufi Zalishi. Sampuli ya kitabaka ilitumiwa kuteua shule kumi na mbili za upili na wanafunzi kumi wa kidato cha tatu kutoka kila shule, katika kaunti ya Kakamega ili kufanikisha utafiti huu. Idadi lengwa ya wanafunzi ni mia moja ishirini. Tulikusanya data kutoka nyanjani. Utafiti huu ultiuria hojaji na mjarabu. Watafitiwa walitunga sentensi na kuandika matini yenye maneno kati ya mia mbili na mia mbili hamsini. Data zote zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa maelezo na utumiaji wa jedwali kwa shabaha ya kuonyesh auhusiano wake na malengo ya utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa makosa ya kisemantiki yalijitokeza katika matini za watafitiwa. Vyanzo vya makosa vilijadili wa na kuwekwa wazi. Kuhusu mbinu za kupunguza utokeaji wa makosa katika matapo husika, utafiti huu ulipendekeza mbinu mbalimbali za kuzingatiwa kwa kina. Matokeo ya utafiti huu yametoa mwanga kwa walimu wa Kiswahili, wanafunzi wa shule za upili na Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala kuhusu mbinu za kutumia katika kupunguza makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika matini za watafiti husika. Pia, utafiti huu umependekeza masuala ambayo yanaweza kushughulikiwa kwa kuwa hayakushughulikiwa katika utafiti huu.

YALIYOMO

UNGAMO i

HATILINZI.....	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI	iv
IKISIRI	v
YALIYOMO.....	vi
ABSTRACT.....	x
SURA YA KWANZA.....	11
1.0 Utangulizi	11
1.1 Usuli wa Mada.....	11
1.2 Suala la Utafiti.....	13
1.3 Malengo ya Utafiti.....	13
1.4 Maswali ya Utafiti	13
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti	14
1.6 Sababu za Kuchagua Mada	14
1.7 Umuhimu wa Utafiti.....	14
1.8 Misingi ya Kinadharia	15
1.8.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa.....	15
1.8.2 Nadharia ya Sarufi Zalishi.....	18
1.8.2.1 Misingi ya Nadharia ya Sarufi Zalishi	19
1.9 Mbinu za Utafiti	20
1.9.1 Eneo la Utafiti.....	21
1.9.2 Wahusika Lengwa	21
1.9.3 Uteuzi wa Sampuli	22
Jedwali 1: Shule Zilizoteuliwa katika Utafiti huu.....	22
1.9.4 Vifaa vya Utafiti.....	23
1.9.4.1 Hojaji	24
Jedwali 2: Lugha za Kwanza za Watafitiwa	25
1.9.4.2 Mjarabu.....	26
1.9.5 Ukusanyaji wa Data.....	27

1.9.6 Uchanganuzi wa Data.....	27
SURA YA PILI.....	30
MAPITIO YA MAANDISHI.....	30
2.1 Utangulizi	30
2.2 Maelezo kuhusu Dhana ya Semantiki	30
2.3 Wataalamu Waliojihusisha na Athari ya Lugha za Kwanza (katika Mawasiliano.....	39
Andishi)	39
2.4 Wataalamu waliojihusisha na Makosa Mbalimbali kwa Lugha Lengwa	42
2.5 Wataalamu Waliojihusisha na Athari za Lugha Mbalimbali katika Kiingereza	44
2.6 Wataalamu Waliochanganua Makosa kwa Lugha za Kigeni	49
2.7 Wataalamu Waliojihusisha na Vyanzo vya Makosa Mbalimbali.....	51
SURA YA TATU.....	58
UCHANGANUZI WA MAKOSA	58
3.1 Utangulizi	58
3.2 Makosa ya Kisemantiki.....	58
Jedwali 3: Umaratokezi wa Makosa ya Kisemantiki.....	59
3.2.1 Matumizi ya Sheng	59
3.2.2 Mrundiko wa Maneno katika Sentensi	62
3.2.3 Ufafanuzi Uliokithiri	65
3.2.4 Kutumia Sauti Isiyofaa katika Neno	67
Jedwali 4: Jamii-lugha	68
3.2.5 Matumizi ya Lugha ya kishairi	72
3.2.6 Kuacha Neno katika Sentensi.....	76
3.2.7 Kutenganisha Neno Visivyo.....	78
3.2.8 Matumizi ya Msamiati Usiofaa	80
Jedwali la 5: Kielelezo cha kuimarika kwa konsonanti.....	82
Asili: Mtafiti (2016).	82
3.2.9 Kuacha Sauti katika Neno	84
3.2.10 Kubadilisha Mpangilio wa Fonimu katika Neno.....	86
3.2.11 Kuunganisha Maneno Visivyo	88
3.3 Vyanzo vya Makosa ya Kisemantiki.....	90
3.3.1 Athari ya Sheng'	90

3.3.2.1 Mrundiko wa Maneno katika Sentensi	92
3.3.2.2 Kuacha Sauti katika Neno	93
3.3.2.3 Kutumia Fonimu Isiyofaa katika Neno	94
3.3.2.4 Uteuzi wa Msamiati Usiofaa	95
3.3.2.5 Ufafanuzi Uliokithiri	96
3.3.3. Ukiukaji wa Sheria za Lugha Lengwa.....	96
3.3.3.1 Kuunganishwa kwa Maneno	97
3.3.3.2 Kugawanywa kwa Neno Visivyo.....	97
3.3.4 Athari za Lugha ya Kishairi	98
3.3.4.1 Kuacha au Kuongeza Fonimu	99
3.3.4.2 Kutofuata Mpangilio wa Maneno katika sentensi	99
3.3.5 Kuandika kwa Kasi.....	100
3.6 Hitimisho	102
SURA YA NNE	103
MBINU ZA KUPUNGUZA UTOKEAJI WA MAKOSA YA KISEMANTIKI.....	103
4.1 Utangulizi	103
4.2 Matumizi ya Lugha ya Kiswahili	103
4.3 Njia za Ufundishaji	104
Jedwali: 5 Aina za maneno.....	105
4.4 Mafunzo ya Kujikumbusha kwa Walimu wa Kiswahili	107
4.5 Uandishi wa Mashairi.....	108
4.6 Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala Nchini Kenya.....	108
4.7 Hitimisho	109
SARA YA TANO	110
MUHTASARI, MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	110
5.1 Utangulizi	110
5.2 Muhtasari.....	110
5.3 Matokeo.....	113
5.3.1 Kutambulisha Makosa ya Kisemantiki katika Matini za Wanafunzi wa Shule za Upili.....	113
5.3.2 Kufafanua Vyanzo vya Makosa Yaliyotambuliwa.....	115
5.3.3 Mbinu za Kupunguza Utokeaji wa Makosa ya Kisemantiki Yaliyotambuliwa	116
5.4 Hitimisho	117

5. 5 Mapendekezo.....	118
5.6 Utafiti Zaidi.....	120
MAREJELEO	121
KIAMBATISHO 1: HOJAJI	132
KIAMBATISHO 2: MJARABU	133
Muda: SAA MOJA	133
KIAMBATISHO 3:MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA MJARABU	135
KIAMBATISHO 4: MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA INSHA	137
SARUFI.....	137
MTINDO	138
MSAMIATI	138
MAUDHUI.....	138
ALAMA ZA KUSAHIHISHIA	138

ABSTRACT

Basically, language enables continuity of conversation in the community. This language occurs in speech and writing. Written communication calls for great care in order to accomplish its goals in the society. It was learnt that without language, communication as a major human activity cannot succeed. Although numerous errors found in students work has been defined and analyzed by various experts, so far little attention has been given to semantic errors in written communication in Kiswahili. Therefore, the purpose of this study was to analyze semantic errors in Kiswahili written communication. The specific objectives of this study were to: (i) examine the semantic errors that occur in secondary school students written work; (ii) analyze the sources of the identified semantic errors; (iii) evaluate appropriate ways to correct semantic errors noted in students texts. This study employed the Error Analysis and Generative Grammar Theories. The researcher used purposive and simple random sampling approaches to select twelve secondary schools and ten form three students from each school to respond to a specially designed test and questionnaire. The students were asked to construct sentences and write atwo hundred to two hundred and fifty word essays which were marked and errors identified. The data collected was analyzed descriptively using charts for the purpose of showing its link with the research objectives. The study found that semantic errors occurred in the sentences and the compositions written by the sampled students. To minimize the occurrence of the semantic errors in written work, this study has recommended various strategies. This study will guide students, Kiswahili teachers in secondary schools and the Kenya Institute of Curriculum Development on the best strategies that can be used in minimizing the semantic errors in the written communication. This study has also identified areas for further research in this area.

SURA YA KWANZA UTANGULIZI

1.0 Utangulizi

Sura hii imejikita katika mambo yafuatayo: Suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti na misingi ya kinadharia.

1.1 Usuli wa Mada

Lugha ya Kiswahili ina hadhi na majukumu mbalimbali nchini Kenya. Imekuwa ikitumika kwa miaka takribani hamsini kama lugha ya taifa. Kiswahili ni lugha ya kibantu. Kuna madai kuwa chimbuko la lugha ya Kiswahili ni upwa wa Afrika Mashariki (Massamba, 2001), likiwemo eneo la mkoa wa pwani, nchini Kenya.

Nchini Kenya Kiswahili sanifu ni lugha inayozungumzwa na watu wengi. Massamba (1999), anadai kuwa Kiswahili ni lugha ambayo inatumiwa na watu ambao idadi yake yakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 60 ulimwenguni. Mawazo haya yanaungwa mkono na Bakari (1982) anayeeleza kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya kiafrika inayozungumzwa na watu wengi zaidi ya zote katika Afrika Mashariki.

Kiswahili ni lugha ya kimataifa na ni Lingua Franka inayotumiwa katika shughuli za kibashara na mawasiliano katika maeneo ya kusini mwa Sahara barani Afrika. Vyuo vingi ulimwenguni hufunza lugha ya Kiswahili. Vituo vya utangazaji hutangaza kwa lugha ya Kiswahili pamoja na lugha zingine.

Tume ya Gachathi (1976) ilipendekeza kuwa Kiswahili liwe somo la lazima kisha litahiniwe katika shule za msingi na za upili. Pendekezo hili lilitekelezwa katika mfumo wa 8.4.4 (Mackay, 1981). Hivyo basi kufikia sasa ni miongo miwili tangu Kiswahili kilipoanza kutahiniwa katika kiwango cha kitaifa.

Hivi sasa lugha ya Kiswahili imepandishwa hadhi kuitia katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010 na kufanywa kuwa lugha rasmi. Kwa sababu hii, Kiswahili hutumika katika shughuli rasmi kama vile, bungeni, miongoni mwa shughuli za kielimu na biashara.

Kwa kuzingatia hayo yaliyosemwa kuhusu lugha ya Kiswahili ni dhahiri kwamba lugha hii ni muhimu sana na ina mawanda mapana kimatumizi, tofauti na lugha zingine za kibantu. Pamoja na umuhimu wake huo mkubwa, matokeo ya wanafunzi katika mitihani ya K.C.P.E na K.C.S.E hayaridhishi. Bado kuna madai kuwa matokeo yake yamekuwa mabaya na yanaendelea kudorora. Kutokana na hayo, mwaka wa (2011) kongamano liliitishwa lakini wataalamu wa lugha ya Kiswahili hawakushughulikia sehemu maalumu ambazo zingetua thibitisho la matokeo mabaya ya mitihani ya Kiswahili, walishughulikia chanzo cha matokeo mabaya kwa jumla.

Hata hivyo lugha ya Kiswahili imefanyiwa utafiti na uchunguzi mwingi na wataalamu mbalimbali wa Isimu na Fasihi. Pana haja ya kutafiti makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika kazi za wanafunzi ili tuweze kupendekeza mbinu ambazo washikadau, walimu na wanafunzi wanaweza kuzingatia ili kuboresha lugha ya Kiswahili.

Obeidat (1986), anaeleza kuwa makosa ya kisemantiki hutokea kutokana na ukiukaji wa sheria za lugha lengwa na kupelekea ujumbe kutoeleweka na waliodhamiriwa. Kosa laweza kuwa ni mchanganyiko wa maneno katika mazingira (sentensi) ambayo maana haijitokezi vizuri.

Aidha, makosa ya kisemantiki hutokea pale ambapo neno au msamiati fulani hutumiwa visivyo katika sentensi au kuweka maneno pamoja yanayovuruga maana iliyotarajiwa. Hivyo basi, makosa yanapojitokeza katika maandishi hapatakuwa na mawasiliano na lugha haitakuwa imetekeleza wajibu wake.

1.2 Suala la Utafiti

Ujumbe wa mwandishi utaeleweka na kuleta athari aliyodhamiria kwa hadhira yake iwapo atatumia lugha ipasavyo. Makosa yanapotokea hukwamiza mawasiliano katika jamii. Kazi za wanafunzi zina makosa mbalimbali. Makosa haya hutokana na vyanzo mbalimbali. Utafiti huu ulihusu uchanganuzi wa makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili. Makosa haya huwa pingamizi katika kuimudu lugha ya Kiswahili. Kutokana na udurusu wa kazi mbalimbali za watafiti wa awali, makosa mbalimbali yanayopatikana katika kazi za wanafunzi yametambuliwa na kuchanganuliwa. Hakuna utafiti wa kina uliofanywa kwa kuweka bayana makosa ya kisemantiki katika matini za wanafunzi wa shule za upili. Hali hii inadhihirisha kuwepo kwa mwanya na kumpa mtafiti ari ya kufanya utafiti. Hivyo basi utafiti huu umeziba mwanya huu.

1.3 Malengo ya Utafiti

Azma kuu ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili mionganoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Ili kufanikisha lengo hili kuu, malengo haya mahususi yalizingatiwa:

- i. Kutambulisha makosa ya kisemantiki katika matini za wanafunzi wa shule za upili.
- ii. Kufafanua vyanzo vya makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za upili.
- iii. Kupendekeza mbinu za kupunguza utokeaji wa makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo ambayo yaliwezesha kutimizwa kwa malengo yake.

- i. Je, kuna makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika matini za wanafunzi wa shule za upili?
- ii. Je, vyanzo vya makosa ya kisemantiki katika matini za wanafunzi wa shule za upili ni vipi?
- iii. Je, makosa ya kisemantiki katika matini za wanafunzi yatapunguzwaje?

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika uchanganuzi wa makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika mawasiliano andishi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za upili, kaunti ya Kakamega. Asemavyo Bakari (1988) semantiki ni tawi la isimu lenye usambamba na matawi mengine ya isimu. Semantiki inakuwa ndio makutanio ya taaluma hizi. Utafiti wetu ulichunguza maana katika viwango vya neno na sentensi. Hivyo basi makosa ya kisemantiki yalichanganuliwa kutokana na utungaji wa sentensi na uandishi wa matini na athari zake zilibainishwa na kuchambuliwa. Kaunti ya Kakamega pekee ilishirikishwa katika utafiti huu. Shule katika kaunti ya Kakamega hujumuisha wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali, nchi ya Kenya. Shule za upili ziliteuliwa kwa misingi kuwa wanafunzi wa shule za upili wamefundishwa kwa kina aina mbalimbali za maneno, aina za sentensi, utungaji wa sentensi na uandishi wa insha mbalimbali kwa kina.

1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti huu ulifanywa kutokana na kutambua kwamba uchanganuzi makosa ya kisemantiki katika mawasiliano ndio msingi muhimu wa kuboresha mawasiliano mionganoni mwa wanajamii. Uchanganuzi huu uliweka wazi mbinu ambazo zinaweza kutumiwa katika kupunguza utokeaji wa makosa katika mawasiliano andishi baina ya wanafunzi mbalimbali wa shule za upili.

Kuwepo kwa tetesi kuwa wanafunzi hawafanyi vyema katika somo la Kiswahili. Tetesi hizi ni za ukweli hasa tunapoangalia matokeo ya kitaifa ambayo hayaridhishi. Watahiniwa hupata matokeo duni sana katika somo la Kiswahili. Matokeo haya yasiyoridhisha ndiyo yalichochea utafiti huu.

Pia, Kiswahili ni lugha iliyo na majukumu mengi, zaidi ya kuwa inatumiwa katika mawana mapana. Aidha, umuhimu wa Kiswahili na kupanuka kwa nyanja zinazotumia Kiswahili na ushawishi mkubwa kwa nchi za Afrika Mashariki kutumia lugha ya Kiswahili, sanjari na matumizi ya Kiingereza, kulichangia baadhi ya sababu zilizopelekea utafiti huu kufanywa ili kufanikisha mawasiliano andishi ya Kiswahili.

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa ni mchango mkubwa kwa walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za upili. Katika jitihada zao za kutambua na kuyarekebisha makosa ya

kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wao katika uandishi wa matini anuwai. Kwa kutilia mkazo vipengele vya kisemantiki vilivyojadiliwa, watajenga ujuzi wa mwanafunzi katika mawasiliano andishi ya Kiswahili. Pia, hali hii itasaidia katika kuyapunguza makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika matumizi ya lugha kwa jumla.

Utafiti huu utawasaidia wanafunzi wa shule za upili kwa kuwaelekeza kuhusu makosa ya kisemantiki ambayo yanatatiza uelewekaji wa ujumbe. Utawaongoza kuhusu njia mwafaka za kusahihisha makosa yanayowatatiza katika mawasiliano andishi ya Kiswahili. Hivyo basi, makosa ya kisemantiki yaliyochanganuliwa katika utafiti huu yatakuwa kumbukumbu kwa wanafunzi kwani yatawafaa zaidi kwa kuboresha mawasiliano andishi ya Kiswahili.

Uchanganuzi wa makosa ya kisemantiki ulioshughulikiwa utawafaa sana wanajamii wenye uwili-lugha ama wingi-lugha. Utafiti huu uliweka wazi vipengele ambavyo huwaathiri watumizi wa lugha ya Kiswahili hususani wanapowasilisha ujumbe wao kimaandishi. Kwa hivyo, hali hii itapunguza makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika matumizi ya lugha mionganoni mwa wanajamii.

Utafiti huu utaiwezesha Wizara ya Elimu kuchukua hatua madhubuti za kutunga sera ya lugha stahiki ya kutumiwa na waandishi wa vitabu vya Kiswahili vinavyoidhinishwa katika ufunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya. Pia utafiti huu utawachochea watafiti wengine kuchunguza aina za makosa katika mawasiliano andishi ambayo hayatashughulikiwa katika utafiti huu.

1.8 Misingi ya Kinadharia

Ili kufikia malengo yake, utafiti huu ilitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa pamoja na Nadharia ya Sarufi Zalishi. Nadharia hii ya pili (Nadharia ya Sarufi Zalishi) ilitumiwa baada ya kugunduliwa kuwa nadharia moja haingetosha kuchanganua baadhi ya makosa yaliyogunduliwa katika baadhi za matini za watafitiwa.

1.8.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa

Nadharia hii hutumiwa katika kuchunguza vyanzo vya makosa ya aina mbalimbali katika lugha. Hutumiwa katika kuyapambanua, kuyaainisha na kufafanua makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili.

Nadharia hii ya Uchanganuzi Makosa iliasisiwa na Corder (1967). Inashikilia kuwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili hufanya makosa ambayo yanaweza kubainishwa, kuchambuliwa, kuainishwa na kutathminiwa ili kubainisha mfumo unaofanya kazi. Nadharia hii hutumia mbinu za kiisimu katika kuangazia makosa yanayofanywa na wanaojifunza lugha. Inaelekeza ni kwa jinsi gani makosa yanavyoweza kushughulikiwa. Inabitisha kwamba mionganoni mwa makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili ni makosa ya athari za lugha ya kwanza. Mwalimu ana uwezo wa kuainisha makosa haya pale ambapo anaelewa mfumo wa lugha ya kwanza ya mwanafunzi.

Nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliasisiwa baada ya kugunduliwa kuwa Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi isingetegemewa katika kubashiri kiwango kikubwa cha makosa yaliyotokea katika lugha. Huu ni mtazamo ambao haukuweza kubashiri ugumu uliodhihirika katika ujifunzaji wa lugha. Nadharia hii ilitumiwa sana kati ya miaka ya 1940 na 1960 ambapo ulinganuzi wa lugha mbili mahususi ilitumiwa kama msingi wa kuchanganua makosa yaliyojitokeza katika matumizi ya lugha ya wale waliokuwa wakijifunza lugha ya pili.

Nadharia hii inachunguza makosa kwa kuyahusisha na vyanzo mbalimbali mbali na uhamishaji hasi kutoka lugha ya kwanza. Inafafanua kimakundi makosa yanayofanywa na wale wanaojifunza lugha ya pili huku ikifichua hali ya wanafunzi kukiuka kaida kupitia kwa ufasiri potovu wa vipengele fulani vya lugha na miundo.

Nadharia hii iliibuka katika miaka ya sitini kama tawi la isimu matumizi ili kuthibitisha kwamba sio makosa yote yaliyojitokeza katika matumizi ya lugha ya wale waliojifunza lugha ya pili, yaliyotokana na uhamishaji kutoka lugha yao ya kwanza. Nadharia hii inasitisiza kuwa makosa mengi ya wanaojifunza lugha ya pili, hayatokani na uhamishaji kutoka lugha ya kwanza bali matumizi yasiyo sahihi ya kanuni za lugha hiyo ya pili.

Mwanaisimu wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, Corder (1974) anaeleza vipengele vya nadharia hii ambavyo vilikuwa muhimu na mwafaka katika kufanikisha ufikiaji wa malengo ya utafiti huu. Navyo ni:

- i. Ukusanyaji wa data
- ii. Uainishaji wa makosa

- iii. Ufafanuzi wa makosa
- iv. Uchanganuzi wa vyanzo vyaa makosa
- v. Kutathmini makosa

Sridhar naye (1981:222) anazitambua daraja nane zifuatazo katika Nadharia ya Uchanganuzi Makosa:

- i. Ukusanyaji wa data
- ii. Utambuaji wa makosa yenyewe
- iii. Uainishaji wa makosa mbalimbali
- iv. Kuonyesha idadi ya kila kikundi cha makosa yaliyoainishwa
- v. Utambuaji wa vipengele vinavyosababisha matatizo katika lugha ya pili
- vi. Urekebishaji wa makosa
- vii. Kuchanganua vyanzo vyaa makosa
- viii. Kuonyesha athari inayosababishwa na tokeo la kosa

Utafiti huu ulifaidika sana na maoni yaliyotolewa na wataalamu, Corder (1974) na Sridhar (1981) katika hatua za uchanganuzi makosa. Wataalamu hao wananaelekeza kuwa ukusanyaji wa data kutoka kwa watafitiwa ndio hatua ya mwanzo katika uchanganuzi makosa. Hii ilitusaidia katika kutathmini idadi lengwa ya watafitiwa. Kipengele hiki kilitusaidia kupata data iliyotuwezesha kufikia lengo kuu pamoja na malengo mahususi ya utafiti wetu.

Pia, Nadharia hii ya Uchanganuzi Makosa ilituelekeza kuhusu njia mwafaka za kutumia katika kuchanganua data yetu. Baada ya kukusanya data kutoka kwa watafitiwa, tuliyagawa makosa mbalimbali tuliyotambua katika matini za watafitiwa. Makosa kumi na moja yaliyotambuliwa yalichanganuliwa kwa kina.

Aidha, nadharia hii ilitufaa katika kuchunguza vyanzo mbalimbali vyaa makosa tuliyotambua katika utafiti wetu. Baadhi ya makosa yalikuwa na zaidi ya chanzo kimoja na yalifafanuliwa kwa uwazi. Mengi ya makosa yalitokana na ukosefu wa umilisi wa kanuni za lugha ya pili (Kiswahili). Tuliangazia mikakati ambayo wanafunzi hutumia katika ujifunzaji wa lugha. Hili lilifaalu baada ya kuchanganua data tuliyokusanya kutoka kwa watafitiwa katika kaunti ya Kakamega

Hatimaye, nadharia hii ilituongoza katika kuzua mbinu za kuyarekebisha makosa tuliyotambua kutokana na data tuliyokusanya. Hatua hii ilitoa mwelekeo kwa washikadau mbalimbali katika viwango mbalimbali kuhusu mbinu mwafaka za kurekebisha makosa yanayotokea katika matini za watafitiwa.

Norish (1983), anaeleza kuwa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inaweza kutumiwa kutoa picha ya aina ya matatizo yanayowakumba wanafunzi. Anaandika kwamba utafiti huo ukifanywa kwa ukamilifu unaweza kusaidia katika uandishi wa miongozo ya masomo. Anasisitiza kuwa nadharia hii hutoa mwangaza kuhusu mbinu anazotumia mwanafunzi ili kuepuka matatizo hayo ya ujifunzaji wa lugha ya pili. Nadharia hii ilitufaa sana katika kuainisha makosa, kuchanganua vyanzo vya makosa husika na kupendekeza mbinu mwafaka za kupunguza utokeaji wa makosa yenye. Hivyo basi, ilituongoza kwa kuweka wazi mambo ambayo ni muhimu kwa mtafiti yeoyote anayetumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa.

Baada ya kuteua makala ya kuchunguzwa tulijukumika katika kuainisha na kufafanua makosa yaliyojitokeza katika uandishi wa insha za wanafunzi. Tulizamia data yetu ili kuchanganua vyanzo vya makosa kwa kuhusisha kila kosa na chanzo chake. Hii ilitusaidia kupata ujumbe kamili kuhusu matatizo yanayowakumba wanafunzi katika ujifunzaji wa lugha lengwa (Kiswahili). Kwa kufanya hivyo ilikuwa rahisi kufikia malengo ya utafiti wetu. Nadharia hii ya pili itatusaidia kuchanganua baadhi ya makosa ambayo nadharia ya kwanza haingeweza kueleza kwa kina.

1.8.2 Nadharia ya Sarufi Zalishi

Sarufi Zalishi ilizuka kutokana na kushindwa kwa wanamiundo kutatua shida za kuchanganua lugha. Baadhi ya wanaisimu waasisi wa aina hii ya nadharia ni Chomsky ambaye anaendeleza nadharia hii katika kitabu chake *Syntactic Structure* (1957). Chomsky alieleza upya umuhimu na kazi ya sarufi na pia umbo na muundo mpya ambao sarufi hii mpya ingechukua. Kabla ya Nadharia ya Sarufi Zalishi, wanaisimu walikuwa wakikusanya data nyingi kutoka kwa waliohojiwa. Baadaye waliweza kutoa sarufi ya kisayansi

iliyoandikwa kwa kutalii miundo yake bila kuzingatia maana yake. Wakati huu sarufi ingeelezwa kama kielelezo mwafaka cha lugha.

Chomsky alipendekeza kwamba sarufi iangaliwe kama nadharia inayoeleza jinsi lugha inavyotumika. Sarufi hii mpya iwe chombo cha kuunda na kuzalisha miundo ya kisarufi ya lugha na pia miundo ambayo si ya kisarufi. Chomsky alipendekeza kuwa kazi ya wanaisimu iwe ni kuunda sarufi kama hizi na kutoa njia ambazo zingetumiwa kupima sarufi hizi.

1.8.2.1 Misingi ya Nadharia ya Sarufi Zalishi

Sarufi Zalishi hunuia kueleza uwezo ama umilisi wa mzawa wa lugha. Uwezo ama umilisi na utendaji ni dhima za kimsingi katika Sarufi Zalishi. Sarufi Zalishi hueleza uwezo wa mzawa wa lugha lakini sio utendaji wake.

Sarufi Zalishi inaeleza tungo zote ambazo zinaweza kuzalishwa katika lugha fulani. Inachunguza na kuchanganua tungo hizi kisha kuzitolea maelezo mwafaka. Licha ya kuchanganua miundo ya tungo, Sarufi Zalishi huweza kuzitolea maelezo na umbo la kifonetiki na pia maana yake.

Sarufi Zalishi huweza kueleza sentensi ambazo ni sahihi na zile ambazo si sahihi katika lugha husika. Kumbuka kwamba sarufi za hapo awali zililenga sentensi zenye usarufi pekee (hasa sarufi mapokeo).

Sifa za Sarufi Zalishi ni kwamba inajieleza kinaganaga na kwa uwazi kupitia sheria hivi kwamba msomaji wa sarufi hii hapaswi kutumia makisio yoyote au ujuzi wowote kujaribu kubaini yanayoelezwa na sarufi hii.

Sheria za Sarufi Zalishi huwa na maagizo ambayo hayaelezwi wala kukisiwa kwa sababu yanajieleza yenye na ni ya moja kwa moja. Kwa mfano, maagizo yanayosema kuwa:

S → KN + KT (Iandike sentensi kama Kirai Nomino na Kirai Kitenzi)

Sarufi Zalishi inaweza kubashiri hivi kwamba haielezi tu tungo ambazo tayari zimetungwa lakini inaweza kuzua kwa kubashiri tungo zote (zozote) ambazo kuna uwezekano wa kuzitoa katika lugha husika au pengine sentensi ambazo hazijawahi hata kamwe kutolewa.

Sarufi Zalishi pia inaweza kuonyesha sentensi ambazo sio za lugha husika. Isitoshe, inajisimamia na ina nguvu. Sarufi Zalishi ina mitindo na utaratibu mwafaka na inaweza kuunda sentensi ambazo si za kulazimishwa wala kusukumizwa. Sarufi ya aina hii inamwezesha, kwa mfano anayefundisha lugha au mtu ambaye si mzungumzaji asilia wa lugha hii atoe sentensi zisizo na kikomo akifuata utaratibu huu. Sarufi Zalishi ni tofauti na Sarufi Geuzamaumbo.

Misingi hii ilitusaidia katika uchanganuzi wa data yetu. Ilituelekeza katika kutathmini iwapo watafitiwa walikiuka sheria za sarufi ya lugha lengwa (Kiswahili).

Ilitusaidia kuchanganua sentensi zilizotungwa na watafitiwa ambao sio wazawa wa lugha ya Kiswahili. Kama sentensi hizo zilizingatia miuundo ya Kiswahili – (KN + KT). Iwapo walitumia vipashio vya Kiswahili kwa njia inayostahili. Vipashio hivyo ni kama: Nomino, Kitenzi, Kivumishi, Kiwakilishi, Kielezi, Kiunganishi, Kihuishi na Kihisishi. Pia ilituwezesha kuchanganua miundo ya sentensi za watafitiwa na kuweza kuzitolea maelezo, umbo la kifonetiki na maana yake.

Nadharia hii ilituongoza katika kuchanganua sentensi za watafitiwa zilizo na utata. Sentensi ambazo hukwamiza mawasiliano. Ikumbukwe ya kwamba huu ni utafiti wa kuangazia makosa ya kisemantiki (maana) katika matini za wanafunzi wa shule za upili.

Hatimaye, nadharia hii ilituongoza katika kuchanganua vyanzo vya makosa yaliyobainishwa katika matini za watafitiwa. Hii ni kutohana na misingi yake ya kueleza umilisi wa mzawa wa lugha. Mzawa wa lugha fulani ana uwezo wa kumiliki miundo na sheria za lugha husika. Nadharia hii ilitusaidia kuchanganua vyanzo vya makosa mbalimbali yaliyojitokeza katika matini za watafitiwa kama vile, iwapo mwanafunzi alihamisha sheria na miundo ya lugha yake ya kwanza kwa lugha lengwa na kuzua kauli zenyeye utata.

1.9 Mbinu za Utafiti

Katika sehemu hii tumefafanua namna utafiti huu ulivyofanywa. Tumeeleza njia ya utafiti iliyotumika, eneo la utafiti, wahusika lengwa, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data hizo. Kwa mujibu wa Weiss (1972), utaratibu wa utafiti unazingatia mikakati ambayo hushughulikiwa na kuweka bayana njia zinazotumika

ili kukusanya data na kuchanganua data hiyo. Utaratibu wa utafiti uliotumiwa katika utafiti huu ni utafiti wa nyanjani. Utafiti huu ulimhusisha mtafiti kwenda nyanjani ambako ndiko alikopata data yake. Mtafiti alikusanya data kutoka shule kumi na mbili za upili katika kaunti ya Kakamega. Mtafiti alitumia mbinu ya hojaji na mjarabu ili kupata data mwafaka ya uchanganuzi wa utafiti huu.

1.9.1 Eneo la Utafiti

Kwa vile utafiti huu ulikuwa wa nyanjani, tulitembelea shule za upili kumi na mbili katika kaunti ya Kakamega ili kupata data iliyotimiza malengo ya utafiti wetu. Sababu ya kuchagua kaunti ya Kakamega ni kutokana na kuwepo kwa wakazi kutoka jamii-lugha mbalimbali kama vile, Wakikuyu, Wameru, Wakisii, Wakamba, Waluhya na lugha nyinginezo nchini Kenya (Education taskforce, 2014). Data iliyopatikana ingetusaidia katika uchanganuzi wa makosa ya kisemantiki.

Hivyo basi, makosa yaliyojitekeza yaliwakilisha jamii-lugha nyingi humu nchini. Pia kaunti hii ina shule za viwango mbalimbali (vya kitaifa, kaunti na kaunti ndogo) ambazo ziliwakilisha wanafunzi wote wa kaunti ya Kakamega. Sampuli ya kitabaka ilitumiwa kuchagua shule zilizojumlishwa katika sampuli za watafitiwa. Kutokana na makosa yaliyotambuliwa na kuchanganuliwa, malengo ya utafiti huu yalitimizwa.

1.9.2 Wahusika Lengwa

Katika utafiti huu walengwa walikuwa ni wanafunzi wa kidato cha tatu kutoka shule mbalimbali za upili, kaunti ya Kakamega. Ellis (1985), anapendekeza kuwa ili kutimiza mahitaji muhimu ni vizuri kutumia wahojiwa wenye viwango kama vile:

- i. Elimu sawa
- ii. Mazingira sawa
- iii. Matumizi ya vitabu sawa

Tuliwachagua watafitiwa hawa kwa sababu ndio waliotakiwa kufanya mjarabu kwa kuwa wana kiwango sawa cha elimu, mazingira yao ni sawa na wanatumia vitabu sawa katika somo la Kiswahili. Pia, wamekuwa wakifundishwa kwa kina matumizi ya lugha, utungaji wa sentensi na uandishi wa matini mbalimbali tangu kidato cha kwanza. Majibu yao

yalitusaidia kuchanganua mada yetu ambayo ni, makosa ya kisemantki katika Mawasiliano andishi ya kiswahili.

1.9.3 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti huu ulilenga makosa ya kisemantiki katika insha za wanafunzi wa shule za upili. Uteuzi wa kuzingatia matabaka ya shule ultumiwa kuteua shule kumi na mbili katika kaunti ya Kakamega. Wanafunzi kumi wa kidato cha tatu kutoka kila shule waliteuliwa ili kufanya mjarabu uliosaidia katika utimizaji wa malengo ya utafiti huu. Illichukuliwa kuwa idadi ya shule kumi na mbili zilizoteuliwa zingeweza kutoa data ya kutosha ya kuchanganua makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili nchini. Shule zilizoteuliwa ziliwakilisha shule zote kwa sababu zinapatikana katika kaunti ya kakamega.

Uteuzi wa kitabaka ultumiwa kwa kuwa utafiti wetu ulidhamiria kuwahuishisha watafitiwa kutoka shule mbalimbali (kaunti ya Kakamega). Huu mtindo ultusaidia kukadiria idadi ya shule zilizohitajika kutoka kila tabaka ili kufanikisha utafiti huu. Hatimaye mtafiti aliteua shule mbili za kitaifa, sita za kaunti na nne za wilaya. Asemavyo Patton (2001), hakuna sheria za idadi katika uteuzi wa sampuli ya utafiti. Muhimu ni mtafiti kufikia sampuli kifu. Idadi hii ya watafitiwa mia moja na ishirini (120) iliyoteuliwa ilitosheleza haja ya utafiti ambao ulinuia kuchunguza makosa ya kisemantiki ya kijumla kwa watafitiwa ambao ni wanafunzi wa shule za upili katika kaunti ya Kakamega. Pia, idadi kubwa zaidi isingeshughulikiwa kikamilifu na mtafiti katika usahihishaji na uchanganuzi wa makosa ya kisemantiki kwa walengwa. Jedwali lifuatalo linaonyesha tabaka na idadi ya shule zilizoteuliwa:

Jedwali 1: Shule Zilizoteuliwa katika Utafiti huu

TABAKA

IDADI YA SHULE

- | | |
|-----------------|-------|
| 1. Kitaifa | Mbili |
| 2. Kaunti | Sita |
| 3. Kaunti ndogo | Nne |

Jumla

Kumi na mbili

Asili: Data ya nyanjani (2016)

Katika jedwali lililo hapo juu ni dhahiri kuwa mtafiti hakuegemea tabaka moja katika ukusanyaji wa data. Alikusanya data kutoka shule mbili za kitaifa, sita za kaunti na nne za kaunti ndogo. Zaidi ya hayo, shule nne zilikuwa za mseto, nne za wasichana na nne za wavulana. Isitoshe, shule nne za mseto zilikuwa za kutwa ilhali za wasichana na za wavulana zilikuwa za bweni. Idadi ya wanafunzi walioteuliwa kutoka kila shule ni kumi (10), jumla ya watafitiwa ilikuwa mia moja ishirini (120). Tulitumia orodha ya majina katika rejista kuwateua wanafunzi waliojumlishwa katika sampuli ya watafitiwa ili kufanikisha utafiti huu. Tuliwateua watafitiwa kwa kuruka idadi fulani ili kufikia watafitiwa 10 kutoka kila shule. Huu mtindo ultumika katika shule zenyenye mkondo mmoja wa wanafunzi katika kidato cha tatu kwa kutegemea idadi ya wanafunzi katika rejista. Walakini katika shule za kitaifa na za kaunti tulitumia mbinu tofauti kuwateua watafitiwa. Baadhi ya shule zilikuwa na mikondo mitano (5) hadi sita (6) ya wanafunzi wa kidato cha tatu. Ilitubidi kuteua watafitiwa wawili wawili kutoka kila mkondo. Kwa mfano, mkondo ‘A’ mtafiti aliteua mwanafunzi wa kwanza na wa mwisho, mkondo ‘B’ mwanafunzi wa pili katika rejista na wa pili kutoka mwisho na kadhalika kwa kila mkondo. Hii ilitusaidia kupata watafitiwa wa viwango mbalimbali vya kielimu (werevu, wastani na wa chini). Ilisadifu kuwa wanafunzi kutoka jamii-lugha mbalimbali walishirikishwa katika ukusanyaji wa data ya utafiti huu.

1.9.4 Vifaa vya Utafiti

Selinger na Shohamy (1989), walitoa mapendekezo juu ya mbinu za kukusanya data inayohusu makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili. Mapendekezo hayo yalikuwa:

1. Wanafunzi wajibu maswali ya tafsiri kwenye hojaji
2. Wanafunzi wapewe mjarabu wa insha
3. Kuuliza wanafunzi wapewe vipindi vya kutamba hadithi

Kati ya mapendekezo haya, tulizingatia pendekezo la kwanza na la pili ambapo hojaji na mada ya insha ilikuwa moja kwa shule zote kumi na mbili zilizoteuliwa. Mbinu hii ilizingatiwa kulingana na hatua za ukusanyaji wa data zilizotolewa na Sridhar (1981).

1.9.4.1 Hojaji

Wanafunzi mia moja ishirini (120) walioteuliwa kutoka shule kumi na mbili (12) kushiriki katika utafiti huu, walipewa hojaji ambayo ilikuwa huru na ambayo iliwa hitaji kutoa habari za kibinagsi na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa jumla. Watafitiwa walielezwa kuhusu ujumbe uliohitajika katika hojaji. Hojaji iliambatanishwa kwenye karatasi ya mjarabu. Walielezwa umuhimu wa kujaza hojaji kikamilifu ili kupata data itakayofanikisha utafiti huu.

Katika hojaji watafitiwa walihitajika kutaja lugha yao ya kwanza. Sababu kuu ilikuwa, kumsaidia mtafiti kutathmini iwapo mtafitiwa alikuwa na athari yoyote kwa lugha ya pili ya Kiswahili. Asemavyo Halliday (1966), ujifunzaji wa lugha ya pili kwa kawaida hufanyika baada ya ujifunzaji wa lugha ya kwanza kukamilika. Katika kiwango hiki ajifunzaye lugha huwa tayari amejenga umilisi wa kutosha wa kimawasiliano katika lugha ya kwanza. Mawazo haya yanaungwa mkono na Chomsky (1957) asemavyo kuwa sheria ambazo msemaji mzawa anazijua aliziita umilisi na utumiaji wa sheria hizo akaziita utendaji (Nadharia ya Sarufi Zalishi). Kutokana na hali hii, lugha ya kwanza ya mwanafunzi inaweza kuathiri kwa kiasi fulani lugha ya pili, ya tatu na zaidi, kwa sababu baadhi ya kanuni za lugha ya kwanza hutumiwa katika usemajji na uandishi wa lugha ya pili. Jedwali lifuatalo linaonyesha lugha za kwanza za watafitiwa wote mia moja ishirini (120) walioshiriki katika utafiti huu.

Jedwali 2: Lugha za Kwanza za Watafitiwa

SHULE	A	B	C	D	E	F	G	H	I	J	K	L	Idadi ya watafitiwa
LUGHA													
<i>Kiluhya</i>	03	04	04	03	04	04	04	03	05	04	04	04	46
<i>Kikalenjin</i>	01	01	01	02			02	01	01		01		10
<i>Kiborna</i>	03												03
<i>Kisomali</i>	01												01
<i>Kikuyu</i>		02		01	01		02		01		01	01	09
<i>Dholuo</i>	01	02	01	01	02	01	01	01	01		02		13
<i>Kiswahili</i>					01	01	01			01	01		05
<i>Kitaita</i>			01			01		01		01			04
<i>Ekegusii</i>		01	01	01	01	01		01		01		02	09
<i>Kiteso</i>	01			01		01		02	01	02		02	10
<i>Kimasai</i>					01								01
<i>Kisabaoti</i>			01	01		01		01			01	01	06
<i>Kimeru</i>			01						01	01			03
JUMLA													120

Asili: Mtafiti (2016)

Watafitiwa walitarajiwa kutaja mahali pa kuzaliwa na mahali wanakoishi. Ijapokuwa watafitiwa wengi ni wazaliwa wa kaunti ya Kakamega na wazungumzaji wa lugha ya Kiluhya kama lugha yao ya kwanza, wanaishi katika miji mbalimbali nchini. Katika miji hii wakazi hutoka jamii-lugha mbalimbali. Hii ilitusaidia katika kuchunguza kama makosa ya kisemantiki yaliyojitokeza katika matini za watafitiwa yana athari ya lugha ya mitaani, mathalani Sheng. Aidha, tulichunguza iwapo mahali anakoishi mtafitiwa palichangia kuwepo kwa makosa ya kisemantiki katika matini za watafitiwa.

Pia, watafitiwa walitarajiwa kutaja lugha zingine wazijuazo. Hii ilikuwa kwa minajili ya kutaka kujua iwapo lugha wazijuazo watafitiwa huwa mojawapo ya vyanzo vya makosa ya

kisemantiki yaliyojitekeza katika matini za watafitiwa. Asemavyo Haroon (1998), lugha inapokutana na nyingine ambayo si sehemu ya fonolojia ya lugha husika, watumizi wa lugha hiyo watatafuta mbinu ya kukabili mabadiliko hayo ya sauti hiyo itamkwe katika lugha husika. Hivyo basi, hii ilitusaidia kuchanganua nafasi ya lugha hizo katika makosa ya kisemantiki tuliyoyabainisha katika utafiti huu.

Habari kuhusu uwezo wa watafitiwa kujieleza kwa lugha ya kwanza kwa ufasaha ulikuwa na umuhimu mkubwa kwa mtafiti kugundua iwapo watafitiwa wanawezi kujieleza kwa lugha ya kwanza kwa ufasaha, pana uwezekano wa makosa ya kisemantiki kutokea katika insha za wanafunzi.

Isitoshe, watafitiwa walitakiwa kueleza kama wanapenda kuhudhuria vipindi nya somo la Kiswahili. Ujumbe huu ilitusaidia katika kuchanganua vyanzo nya makosa ya kisemantiki yaliyojitekeza katika matini za watafitiwa, hususani pale ambapo watafitiwa walitumia msamiati usiofaa kufidia uhaba wa msamiati bora katika utungaji wa sentensi na uandishi wa matini kwa jumla. Hali hii huchangia kuwepo kwa matokeo duni katika somo la Kiswahili.

1.9.4.2 Mjarabu

Watafitiwa mia moja ishirini walioteuliwa kama sampuli ya utafiti huu kutoka shule kumi na mbili katika kaunti ya Kakamega, walipewa mjarabu uliowahitaji kutunga sentensi mbalimbali. Katika utungaji wa sentensi, mtafiti alitaka kujua iwapo watafitiwa wana umilisi wa kutumia viambajengo nya sentensi ili kuunda sentensi zilizo na maana. Kwa mujibu wa Laufer (1997), katika semantiki maneno yanapangwa katika vipengele vilivyo na maana katika sentensi. Kila neno lionyeshe liko katika tapo gani na lazima kila neno litumiwe vizuri kama ni nomino ama ni kitenzi, kivumishi au kielezi na kadhalika. Hii itamsaidia msomaji yeyote yule kuchanganua vyema neno analolitafitia ili kupata maarifa anayotaka. Pia, watafitiwa walitakiwa kuandika matini juu ya, **“Umuhimu wa magazeti kwa wanafunzi wa shule za upili.”** Mada hii iliwapatia watafitiwa uwezo wa kujieleza kwa ukamilifu na hatimaye tuliweza kusahihisha na kuchanganua makosa ya kisemantiki kwa njia rahisi. Watafitiwa walipatiwa muda wa saa moja kufanya mjarabu. Muda huu ulikadiriwa kutokana na ukubwa wa mjarabu. Watafitiwa walitakiwa kutumia kati ya

maneno mia mbili na mia mbili hamsini (200-250). Baadaye tulijikita katika usahihishaji wa mjarabu tuliowapatia watafitiwa husika walioteuliwa kushiriki katika utafiti huu.

1.9.5 Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa Sridhar (1981), daraja ifuatayo huzingatiwa katika Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Ukusanyaji wa data kutoka kwa watafitiwa kupitia uandishi wa insha au majibu ya mtihani. Hivyo basi, tulianza ukusanyaji wa data ya utafiti huu kutoka insha za wanafunzi 120 kutoka shule kumi na mbili (12) za upili katika kaunti ya Kakamega. Hii ni baada ya kupata kibali kutoka kwa Baraza la kitaifa la Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi. Baadaye tulitembelea afisi ya Mkuu wa Elimu kaunti ya Kakamega ambaye alitupatia barua iliyotuwezesha kukusanya data yetu. Wakuu wa shule za upili mbalimbali tulizotembelea ili kukusanya data, walituruhusu kwa kuwahuisha wakuu wa Idara ya Kiswahili kutusaidia kupata data sahihi. Katika shule za mseto za kutwa, tuliruhusiwa na walimu wakuu kukusanya data kati ya Jumatatu na Ijumaa kutoka kwa watafitiwa walioteuliwa kimaksudi na kuwekwa kando na wengine. Wakati mwafaka wa kukusanya data ulikuwa kati ya saa kumi unusu jioni hadi saa kumi na moja unusu jioni baada ya ratiba ya masomo ya siku. Katika shule za bweni, wakati murua ulikuwa wikendi (Jumamosi na Jumapili) kati ya saa kumi na mbili unusu hadi saa moja unusu asubuhi na jioni, kabla ya kuanza ratiba ya shule na baada ya ratiba ya siku. Kabla ya mtafiti kuanza kukusanya data kutoka kwa watafitiwa, aliwaeleza watafitiwa dhamira ya kukusanya data hiyo ili kuondoa wahaka mionganoni mwa watafitiwa. Walimu wa idara ya Kiswahili kutoka shule zilizojumuishwa katika sampuli ya utafiti, waliwajibika katika kusimamia mjarabu ambao ulichukua muda wa saa moja. Sababu kuu ya walimu husika kusimamia mjarabu ni kuhakikisha kuwa watafitiwa walioteuliwa wameshiriki kikamilifu katika kujaza hojaji na kuandika matini kwa uwazi. Hatimaye, mtafiti alikabidhiwa data tayari kwa usahihishaji na hatimaye kwa uchanganuzi.

1.9.6 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ni ule uchunguzi wa data iliyokusanywa nyanjani na kufanyiwa uamuzi fulani kuihusu. Kwa mujibu wa Mbwesa (2006), uchanganuzi wa data ni jumla ya shughuli na taratibu zote ambazo mtafiti huifanyia data yake ili kufikia uamuzi na matokeo fulani kutokana na data hiyo.

Baada ya kukusanya data nyanjani (kutoka kwa watafitiwa ambao walikuwa ni wanafunzi wa shule za upili, kidato cha tatu, katika kaunti ya Kakamega), tulijukumika katika usahihishaji wa insha za watafitiwa 120. Tulizingatia mchakato wa Sridhar (1981) katika Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Mchakato wa Sridhar (mtaje) ulitumiwa kama mfumo wa uchanganuzi wa data. Hatua hizo ni:

- i. Utambuaji wa makosa
- ii. Uainishaji wa makosa mbalimbali
- iii. Kuonyesha idadi ya kila kikundi cha makosa yaliyoainishwa
- iv. Utambuaji wa vipengele vinavyosababisha matatizo katika lugha ya pili
- v. Urekebishaji wa makosa
- vi. Kuchanganua vyanzo vyaa makosa

Baadaye mtafiti alichanganua makosa ya kisemantiki kwa kuzingatia umaratokezi wa kila kosa. Kwa mujibu wa James (1998:103), katika kuyaainisha na kuchanganua makosa yaliyofanywa na wanafunzi katika matini zao, ni vyema kuzingatia umaratokezi wa kila kosa husika tukilinganisha na urefu wa matini. Mawazo ya msomi huyo yalitusaidia katika kutathmini iwapo mwanafunzi anarudia kosa husika mara kwa mara au limetokea mara moja katika matini nzima. Mwanafunzi anaweza kuacha herufi fulani katika uandishi wake na wakati mwingine akaitumia. James (mtaje) anaendelea kusema kuwa katika hali kama hii tunachukulia kama kutomakinika kwa mwanafunzi anapoandika kazi yake. Iwapo mwanafunzi angepatiwa fursa ya kuipitia kazi yake, anaweza kujirekebisha. Hivyo basi, katika uchanganuzi wa data yetu, tulitilia maanani umaratokezi wa kila kosa katika matini za wanafunzi.

Baada ya kupitia insha ya kila mwanafunzi na kugundua makosa ya kisemantiki aliyyofanya, mtafiti aliyaainisha na kuyaweka katika matapo mbalimbali kisha aliweza kuyafafanua huku akidhibiti nadharia tete kwa kutumia data alizozipata. Mtafiti aliweza kuzitafsiri na hatimaye kuiwasilisha ithibati hiyo kwa kutambua sehemu zenye uhusiano wa moja kwa moja na lengo kuu, maswali ya utafiti na madhumuni ya utafiti huu. Baadaye mtafiti alichunguza chanzo ama vyanzo mbalimbali vilivyochangia makosa ya kisemantiki yaliyojitokeza katika insha za wanafunzi. Katika kuangazia vyanzo vyaa makosa

tuliwashirikisha wanafunzi ili kuweka wazi maana za baadhi ya istilahi zilizotumiwa na watafitiwa, hususani Sheng. Isitoshe, tulipendekeza mbinu zinazoweza kuzingatiwa ili kupunguza utokeaji wa makosa yaliyochanganuliwa katika matini za watafitiwa husika. Hatimaye, mtafiti alitumia mbinu za kimaelezo na majedwali ili kurahisisha usomaji wake.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia kazi mbalimbali zilizopitiwa na mtafiti kwa minajili ya kugundua yale yaliyoandikwa kuhusu mada husika. Maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu dhana ya semantiki yameshughulikiwa kwa kina. Pamoja na yale yaliyo na uhusiano na malengo ya utafiti, yamechambuliwa huku umuhimu wake katika utafiti huu ukiwekwa bayana.

Suala la makosa limeshughulikiwa kwa wingi japo kwa namna tofautitofauti. Wasomi mbalimbali wamechunguza jinsi makosa hujitokeza katika lugha ya mazungumzo na ile andishi kwa kurejelea makundi anuwai ya watumiaji wa lugha. Katika kazi zote tulizopitia, hatukuona kazi yoyote iliyoshughulikia makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili mionganini mwa wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Hivyo basi, tumechambua kazi mbalimbali katika sehemu inayofuata.

2.2 Maelezo kuhusu Dhana ya Semantiki

Wataalamu ambao wameishughulikia taaluma hii ya semantiki, hujishughulisha zaidi na uhusiano uliopo baina ya maana na muundo wa lugha, kwa kuwa maana ni kigezo muhimu katika kuielewa lugha. Katika taaluma hii, maana inayoshughulikiwa sana ni maana fikirika. Maana hii huyakusanya mambo ya kimsingi yanayofikirika. Nimefafanua hoja za wataalamu mbalimbali waliowahi kuandika kuhusu dhana ya semantiki na wamesema mengi katika mkabala huu.

Kwa mujibu wa Obuchi na Mukhwana (wataje), semantiki ni stadi ya maana na jukumu la kimsingi lake ni kueleza maana ya maneno na dhana. Wanasemantiki hushughulikia maana katika viwango vya vipashio huru na maana ya vipashio hivyo katika tungo. Hii ina maana kuwa maana huchunguzwa katika kiwango cha maneno huru na maana katika sentensi. Semantiki kama taaluma ni muhimu kwani isipozingatiwa vyema, mawasiliano ya wanadamu hayawezi kusahilika kamwe. Hali hii inatokana na ukweli kuwa jukumu kuu la

lugha ya mwanadamu ni mawasiliano ambayo huhusisha upashaji wa ujumbe. Viambajengo vya lugha ya mwandamu hubeba na kudhihirisha maana na ufanuzi wa maana husika. Viambajengo hivyo vya lugha ni: fonimu, mofu, maneno na sentensi. Kwa mantiki hii, lengo la sheria za kifonolojia na sintaksia ni kuunda tungo na sentensi zenyé maana. Semantiki huchunguza namna ambavyo viambajengo vya lugha huhusiana ili kuleta maana kamili. Hivyo basi, mofu na maneno huweza kuwa na maana yanaposimama pekee lakini yakakosa kuwa na maana katika tungo au sentensi mtawalia. Inabainika wazi kwamba semantiki huchunguza maana katika viwango vya mofu au maneno huru na pia maana katika tungo zilizokamilika kama vile sentensi.

Obuchi na Mukhwana (2010), wanaendelea kueleza kuwa maana inayoshughulikiwa sana ni maana fikirika. Maana hii hukusanya mambo ya kimsingi yanayofikirika. Kwa mfano, neno ‘pea’ litakusanya uhusiano kama vile fikia hali ya ukubwa, fagia, jozi, tunda linalofanana na pera. Kutokana na mfano huu, inabainika kuwa maana fikirika ni maana inayokusanya mambo mbalimbali tunayoweza kuyafananisha au kuyahusisha na neno fulani. Mambo haya ndiyo yanayozalisha masuala yanayopambanua neno moja na lingine. Haya hasa huwa ni masuala ya kimaana na hukusanya sifa mbalimbali za neno fulani. Katika kubainisha haya masuala ya kimaana, alama za kujumlisha (+) na kuondoa (-) hutumiwa ili kuonyesha uhusiano huo. Kwa mfano, neno ‘*mvulana*’litabainishwa ifuatavyo kisemantiki:

Mvulana

+ uhai		+ uhai
+ uume	au	- uuke
+ uchanga		- uzee
+ binadamu		+ binadmu

Mvulana

Ijapokuwa masuala ya kimaana hutumika katika kubainisha maana za maneno, si rahisi kupata masuala ya kimaana yatakayoonyesha tofauti hizo katika baadhi ya maneno au

kuonyesha tofauti hizo baina ya maneno kwa kuwa yanakaribiana sana kimaana. Hivyo, baadhi ya maneno huweza kutofautishwa au kuhusishwa na maneno mengine kwa kuurejelea uhusiano wa maneno hayo na maneno mengine.

Pontner (2005), ana maoni yanayokaribiana na ya Obuchi na Mukhwana (wataje). Anasema kuwa katika semantiki ya maneno, neno moja linaweza kusheheni maana tofauti linapotumiwa katika muktadha. Kwa mfano, katika lugha ya Kiingereza kuna neno moja tu la kutajia hali zote za mchele '*rice*'. Katika lugha ya Kiswahili kuna maneno takribani sita (6) ya kutajia mchele.

Mchele – mchele mbichi

Mpunga – mchele ukiwa shambani

Mashendeya – mchele mbovu

Pilau - mchele uliopikwa kwa viungo

Biriani – mchele uliopikwa kwa birinzi

Wali – mchele uliopikwa

Hivyo, lugha ya Kiswahili ina mkondo wa neno mchele ulio mpana zaidi ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza. Ikiwa hakungekuwa na maneno hayo yote kueleza hali zote za mchele, basi neno moja '*mchele*' lingetumiwa.

Jackendoff (1987), anaandika kuwa semantiki huchunguza namna viambajengo vya lugha huhusiana ili kuleta maana kamilifu. Hivyo, mofu na maneno huweza kuwa na maana yanaposimama pekee lakini yakakosa kuwa na maana katika tungo au sentensi. Kwa mfano, mofu '-zee' inasimamia dhana iliyo na umri mkubwa (iliyozeeka) lakini ikiongezewa mofu iliyosimamia ngeli, mofu hiyo haitabeba maana yoyote kwa mfano, zee – m/ki. Neno lolote lisipotumiwa mahali panapostahili kwenye sentensi halitawasilisha maana iliyokusudiwa. Kwa mfano neno 'dada' linarejelea ndugu wa kike lakini litakapoingizwa mahali pasipofaa katika sentensi halitupi maana yoyote. Kama vile, *dada mtawa huyu ni*. Hivyo basi, taaluma ya semantiki hushirikishwa na tanzu za isimu ambazo ni fonolojia, mofolojia na sintaksia. Uhusiano wa mofu katika mofolojia na ule wa muundo wa ndani na wa nje wa sentensi katika sintaksia ni uhusiano wa kimaana.

Dowty (1986), anadai kuwa semantiki ni kipengele kinachojihusisha na shida za kimaana. Taaluma hii inahusu jinsi mwanadamu anavyopata umilisi wa maana katika lugha. Anadai kuwa binadamu anapata maana ya maneno kwa kuangalia kitendo ambacho mwenzake anakitenda. Kwa mujibu wa Lakoff (1988), semantiki lazima ijihushishe na kufafanua baadhi ya vipengele ambavyo havijashughulikiwa na sintaksia pamoja na mofolojia katika sentensi. Kwa hivyo, semantiki hufafanua maana katika sentensi ambayo haishughulikiwi katika vima vingine vya lugha.

Bakari (1988), anadai kwamba semantiki hujishughulisha na masuala yafuatayo:

- i. Maana na uainishaji wa maana za maneno.
- ii. Maana za tungo.
- iii. Taratibu za kuchambua maana.
- iv. Etimolojia ya maana za maneno katika sentensi.
- v. Nadharia za uchambuzi wa maana.

Hii ina maana kuwa katika semantiki maana inaweza kubainishwa kiisimu katika kiwango cha neno na katika kiwango cha tungo kama vile sentensi na makala iliyio kubwa zaidi. Wanaismu wengi hujishughulisha zaidi na uhusiano uliopo baina ya maneno na muundo wa lugha. Hivyo basi, kuijua lugha si kuzijua sauti, silabi, neno na kanuni za sarufi yake wala kuhodhi shehena kubwa ya msamati wake tu. Kunahusisha kufahamu maana ambazo zimeambatanishwa na mambo hayo katika miktadha ya kijamii.

Wasemavyo Karanja na Habwe (2004), taaluma ya semantiki ni utanzu wa isimu unaochunguza maana katika lugha ya mwanadamu. Semantiki hutafiti maana za fonimu, mofimu, maneno na tungo. Maana hushughulikiwa katika viwango vyote vya lugha kama vile sauti, maneno na sentensi. Hii ina maana kuwa, ‘maana’ ndicho kipengele muhimu zaidi katika uchunguzi wa lugha ya mwanadamu. Hii ni kwa sababu kazi kuu ya lugha ni mawasiliano na mawasiliano huhusisha upashaji wa ujumbe ambaa hueleweka katika maana ya tamko. Pasipo kupasha ujumbe hapatakuwa na mawasiliano na kwa hivyo lugha haitakuwa imetekeleza wajibu wake. Ujumbe hudhihirika katika maana na ufanuzi wa maana zilizobebwa na vipashio vya lugha vinavyohusika kama vile fonimu, neno na sentensi.

Tyler na Evans (2003), wanadai kuwa maana ya maumbo huungana ili maana kamili ya sentensi iweze kujitokeza. Ni lazima neno lihusishwe na kile ambacho mnenaji anataka kukisema ili maana ya leksia iweze kujitokeza. Hivyo basi, maana hupatikana katika ile hali ya utendaji wa jambo katika tamko.

Maoni ya mtaalamu huyu yanalingana na ya Filmore (1968), ambaye anadai kuwa, katika kiwango cha sentensi kuna uhusika ambao ni muhimu sana. Uhusika ni dhana ya kisarufi itumikayo kuonyesha dhima ya maneno katika tungo. Mtazamo huu una misingi katika nadharia ya isimu inayodai kuwepo kwa muundo wa ndani na wa nje wa lugha. Filmore (1968), alitumia wazo la muundo wa ndani kuzua kile alichokiita *sarufi ya uhusika*. Sarufi ya uhusika ina umuhimu wa pekee katika uchambuzi wa tungo. Hivyo basi, mtu anapojifunza lugha hujifunza pia kanuni za kuyaunganisha maneno ili kujenga sentensi. Kanuni hizi humwezesha kutofautisha maana katika sentensi mbalimbali. Kwa mfano:

Yohana alimuua Maria.

Maria alimuua Yohana.

Paka alimfukuza panya.

Panya atamwongoza paka.

Hata kama maneno katika sentensi hizi yamefanana katika maumbo yake, yana maana tofauti (kileksia). Inadhihirika basi kuwa muundo wa kisintaksia wa virai, vishazi na sentensi huchangia katika kuwasilisha maana fulani.

Kulingana na Filmore (mtaje), vitenzi vya mwendo vilihusiana kwa namna fulani na nomino katika sentensi. Nomino zilikuwa na utendaji kazi maalumu. Utendaji kazi huo unabakia vivyo hivyo hata kama sentensi itafanyiwa mageuzi. Anaendelea kusema kuwa hayo yalikuwa majukumu ya nomino hizo. Kwa mfano:

Baba anasoma gazeti

Mama anapika wali

Mtoto anacheza mpira

Katika sentensi hizi nomino ‘*baba*’, ‘*mama*’ na ‘*mtoto*’ zinatenda kazi ya mtenda. Hii ni kwa sababu zinasababisha vitendo fulani kutendeka. Hata sentensi hizo zibadilishwe na kuwa katika kauli ya kutendewa, mtenda atabakia kuwa yuleyule.

Mwanaisimu Cann (1983), ameeleza kuwa iwapo mwanafunzi yeoyote yule anataka kupata maana ya neno, basi ataangalia vipengele ambavyo vinajulikana kama visasili ambavyo huunda maana ya kitu kinachotajwa. Mwanafunzi anapounganisha vipengele hivi anaweza kupata maana ya kitu kinachodhamiriwa. Kwa mfano, neno ‘*meza*’ hugawanywa kwa kuwa kitu kisicho na uhai. Kitu kilichotengenezwa kwa mbaao, madini au kioo chenye uvungu na ubapa juu. Inatumiwa kwa kulia, kuandikia au kwa mchezo, kina matendegu na kadhalika. Upungufu wa kupata maana katika hali hii ni kuwa, unaweza kupata kifaa kingine kilicho na maelezo kama haya na hakiwezi kutumiwa kwa kuandikia lakini kina sifa kama zilizoorodheshwa. Anazidi kufafanua kuwa viwakilishi vyta vipengele vya kitu katika ubongo wa binadamu ndiyo humsaidia kupata maana.

Katz (1986), anadai kuwa maana ya neno inasemekana kuwa inapatikana kwa namna neno linavyotumika. Anasema kuwa maana hupatikana katika kudhihirisha kwa ishara kile msemaji anakitaja; kwa mfano, mtu anapozungumza kuhusu ‘*ng’ombe*’ anamwonyesha kwa ishara kuwa huyu ndiye mnyama ambaye anamzungumzia. Njia nyingine ya kupata maana ni kusema tu kile ambacho msemaji anadhamiria. Maana ya pili hutoa vidokezo vinavyosaidia maana kupatikana na maana ya kwanza huungana na maana ya pili kutoa jawabu kamili. Anasema kuwa ni lazima mnenaji aangalie anachokidhamiria katika uneni au neno lake. Hali hii hujulikana kwa kidhahania tu. Hii inasaidia mtu kujua kile mnenaji anachokidhamiria. Anadai kuwa maana ya neno hujulikana kwa kulihusisha neno hilo na kitu kinachokaribiana na kile kinachotamkwa. Kwa mfano, *mbuzi* anahuishwa na *kondoo* na hapo maana inaweza kujitokeza na mwishowe maana inapatikana.

Mwanaisimu William (1992), anasema kuwa kujua maana ya kitu ni kujua ukweli wa jambo hilo. Anadai kuwa iwapo mtu anataka kujua maana ya neno fulani ni lazima maelezo haya yawe na ukweli ambaao unalingana na hali halisi ya ulimwengu. Kwa mfano, iwapo mtu anatamka uneni, kuna ‘*vita*’ ni lazima kitendo hiki kihuksike na hali ya ukweli hivi kwamba mapigano baina ya watu, wanyama au mataifa yashuhudiwe katika maeneo fulani. Anadai kuwa maneno ni vipengele muhimu vinavyounda sentensi. Maneno haya

lazima yawe na maana inayokubalika. Yaani, ni lazima yasimamie viarifa, vitenzi, nomino, visifa na viwango vingine muhimu vinavyounda sentensi. Hatuwezi kuwa na sentensi pasipo kuwa na maneno ambayo yana maana. Naye Lewis (1997), anakiri kuwa kila uneni una uhusiano na kile kinachotamkwa. Kulingana naye, uneni ni mambo dhahania ambayo mnenaji anayo katika mawazo yake, ambayo anataka kuwasilisha. Anadai kuwa maana ya maneno ni mambo thabiti ya kisaikolojia; yaani, dhana mbalimbali au picha zinazopatikana katika ubongo wa binadamu. Kwa hivyo, semantiki hutegemea saikolojia; tena kuelezea maana ya maneno hutegemea nia ya kisaikolojia ya mnenaji au hali ambazo zina uhusiano na uneni. Anadai kuwa kirejelewa huwa muhimu katika kuelezea maana ya neno kwa sababu kinahusiana na hisia za mwanadamu.

Kempson (1977), anadai kuwa binadamu huelewa maana ya maneno kwa kuhusisha neno hili na kitu fulani. Kwa mfano, wanafunzi wanaozuru mbuga za wanyama pori na wakipata neno ‘ndovu’ limenakiliwa katika mlango watahusisha neno hilo na mnyama wanayemwona ndani ya lango hilo na hapo wataweza kupata maana ya mnyama huyo. Anadai kuwa watu hupata maana ya maneno kwa kuchunguza neno hilo linaashiria nini; yaani, kwa kutumia neno moja / maneno mawili ili kupata maana kamili. Kwa mfano, neno ‘mwalimu’ huongezwa ‘mlevi’ kuwa ‘mwalimu mlevi’. Hapo, mwanafunzi atakuwa ameunganisha maneno mawili kupata maana. Hii ina maana kuwa neno lolote lile hupata maana yake kutohana na maneno mengine yanayounganishwa na neno lile.

Naye Newmey (1987), anadai kuwa semantiki inachangia pakubwa katika kuifanya sentensi yoyote ile ieleweke na itoe maana mwafaka. Ili sentensi yoyote ieleweke kamili lazima kuwepo na matapo mbalimbali ya kimaana yanayofanya sentensi kueleweka. Alitambua neno wakala —yaani anayesababisha jambo kutokea; mada pamoja na chanzo cha jambo; na mwisho malengo ambayo yanastahili kutimizwa ili sentensi ikamilike. Alisema kuwa sentensi ikiwa na mpangilio mwafaka wa matapo haya basi maana itaweza kujitokeza vizuri.

Zimmermann (1986), anasisitiza kuwa matini huleta maana kwa sababu ya ule mwendeleo wa kuelezea maarifa na maelezo katika muktadha unaorejelewa. Anasema kuwa muktadha huo lazima uwe na mwelekeo mwafaka na hali kadhalika uweze kulingana na hali halisi ya ulimwengu.

Mwanaisimu Talmy (2000), anadai kuwa maana katika dhana ni mkusanyiko wa maelezo yanayokubalika. Inadhihirika kwamba kando na uneni wowote ule, mpangilio wa matukio na imani kuhusu jambo/mambo fulani, lazima yawepo ili maana murua iweze kujitokeza katika maandishi. Wakati watu wanapojieleza katika matini/muktadha wowote ule, dhana ya virejelewa inafanyiwa kazi katika ubongo wa binadamu ambapo hali hii huhifadhiwa. Hali kadhalika, virejelewa hivi na dhana hufanyiwa kazi mara kadhaa kwa wakati mmoja. Hii ndiyo sababu inafanya binadamu kuweza kutoa uneni au kuelewa maana katika matini/muktadha kwa wakati mmoja.

Eco (1976), anadokeza kuwa lazima kuwepo na mipaka kati ya semantiki na pragmatiki ili kuondoa utata kati ya taaluma hizi mbili. Anadai kuwa hata kama tofauti ipo, kwa kiasi, ni vyema kufafanua zaidi mipaka kati ya taaluma hizi ili muktadha wa kile kinachozungumzwa ufahamike vyema.

Mwanaisimu Lyon (1968), anadai kuwa leksikografia ni kipengele muhimu sana katika kuelezea lugha yoyote ile. Anasema kuwa, neno lolote lile lazima lielezwe kifonolojia, yaani, jinsi neno hilo lilivyoundwa; lazima lielezwe jinsi lilivyopangwa; kipengele cha mofolojia lazima kielezwe vizuri. Vilevile, anadai kuwa ni lazima neno lielezwe jinsi msomaji anavyoweza kupata maana ya neno hilo katika sentensi na mwisho mpangilio wa neno hilo katika sentensi lazima lifafanuliwe zaidi. Hivyo basi, ni lazima neno liwe na maana katika sentensi ili lifahamike vyema.

Laufer (1997), anadai kuwa katika kiwango cha semantiki, maneno yanaweza kupangwa katika vipengele vilivyo na maana sawa katika sentensi. Anasema kwamba katika kiwango cha sarufi, maneno yanaweza kupangwa katika vikundi ambavyo vinajulikana kama matamshi ya maneno. Hivyo basi, kila neno au leksia lazima idhihirishe hilo neno liko katika tapo gani au ni neno la kiwango kipi katika leksikografia. Kila neno lazima lielezwe vizuri kama ni nomino au ni kitenzi. Hapa msomi ye yeyote atawezeku changanua vyema, neno analolitafitia ili kupata maarifa anayohitaji.

Chomsky (1970), anadai kuwa mfumo wa kileksia ulichukuliwa kuwa na viwakilisho kama vifuatavyo: wakala; anayesababisha jambo lifanyike; mada, wazo ambalo linazungumziwa; kiini, habari inakotoka na mwishowe mada kuu ili sentensi ikamilike.

Kwa mfano, neno ‘*mnunuzi*’ lazima lionyeshe vitengo hivi ambavyo vimetajwa. Nani anayenunua, ananunua kutoka wapi na nini kinamfanya kununua kitu hicho. Kulingana na nadharia ya semantiki, ni kwamba maana ya usemi ulio na utata hutokea na maana ya vipengele katika sentensi kwa namna vipengele hivyo vinaunganishwa.

Naye Turner (2006), anasema kuwa viwakilisho vya kisemantiki vinaweza kuelezewa kama vipengele ambavyo vinaonyesha vitu katika ulmwengu wa mambo au vitu vinavyozungumziwa kuyahusu. Pia, inadaiwa kwamba viwakilisho vya kisemantiki ni mambo yanayotendeka katika ufahamu wa binadamu. Hii ndiyo sababu mtu anapotaja neno ‘*mbwa*’ hustahili kuwa na kiwakilisho cha neno hili. Yaani, katika ubongo wa mtu atajaribu kuwa na kiwakilisho thabiti cha huyo mnyama. Mwanafunzi anapokuwa akijifunza lugha ya pili huwa ana fahiwa na kanuni iliyoasiwa na Chomsky (1981), inayodai kuwa kuna mambo ya kidhahania ya kiisimu ambayo yanahuksika na lugha zote za kiasili. Kanuni hizi zinadai kuwa hali awali ya akili ya mnenaji wa lugha ya kwanza huchangia pakubwa katika umilisi wa lugha ya kwanza. Hali hii dhahania huweza kumtatiza mwanafunzi anapajaribu kumiliki lugha ya pili. Hivyo basi, lugha ya pili itakuwa na ugumu fulani katika ujifunzaji wa mwanafunzi ambaye tayari ana umilisi wa lugha ya kwanza.

Griffiths (2006), anasisitiza kuwa iwapo mzungumzaji atanua kuzungumza na mwenzake, lazima mawazo yale anayotaka kuwasilisha yawe yamehifadhiwa katika ubongo wa binadamu ili kuwe na mawasiliano sawasawa. Anadai kuwa ni lazima kuwepo na kiwakilishi hasa cha kile kinachotajwa na mzungumzaji wakati anapotoa uneni. Anadokeza kuwa, anapoeleza hali hii, ni lazima aonyeshe kuwa kitendo anachokitaja kinalingana na hali halisi ya maisha. Anasisitiza kuwa, iwapo ni lazima kuwe na mawasiliano na maelewano, lazima kuwepo na mawazo pamoja na uhakika wa kile ambacho uneni unataka kuwasilisha. Hapa, yule anayesikiliza atawezekuelewa kile anachotakikana kufanya. Kwa hivyo, tendo hilo litalingana na muktadha wa hali halisi ya maisha, kwa sababu kutakuwa na uhakika wa kitendo hicho. Anasema kuwa ni lazima ishara itumike ili msikilizaji aweze kufahamu vyema viwakilishi vilivyomo katika ubongo wa binadamu anapotajiwa neno, tendo au kitu.

Mawazo ya mwanaisimu huyo yanaungwa mkono na Heim (1989), ambaye anasema kuwa, ili mawasiliano yaafikiwe, mambo mbalimbali hutokea. Kwanza, mzungumzaji huwa na jambo fulani ambalo angependa kuwasilisha kwa msikilizaji. Ujumbe unaowasilishwa huwa na umbo au ishara inayolewaka kwa msikilizaji, kwa njia ya maandishi au ishara za aina kwa aina na kadhalika. Tamko lolote huweza kutolewa tafsiri inayofaa na inayofahamika kiisimu. Hivyo basi, semantiki inaelewaka kama sehemu ya umilisi alio nao msemaji au mzawa wa lugha. Umilisi wa kiisimu alio nao kila mzawa wa lugha humwezesha kusema na kuyaelewa yaliyosemwa na wengine. Umilisi wa kisemantiki basi ni sehemu halisi ya umilisi wa kiisimu.

2.3 Wataalamu Waliojihuisha na Athari ya Lugha za Kwanza (katika Mawasiliano

Andishi)

Akichambua insha za wanafunzi kuhusiana na makosa yanayotokana na athari za lugha za Kibukusu, Were (1996), alibainisha kwamba lugha ya Kibukusu ilisababisha viwango vikubwa vya makosa yanayopatikana katika insha za wanafunzi hasa makosa ya tahajia na msamiati. Kazi ya msomi huyu ilitusaidia katika kutambua baadhi ya vyanzo vya makosa katika lugha ya Kiswahili. Tofauti iliyopo na utafiti huu ni kuwa wakati msomi huyu alitumia watafitiwa kutoka jamii-lugha moja (Wabukusu), utafiti wetu uliwahuisha watafitiwa kutoka jamii-lugha mbalimbali.

Akichunguza athari za lugha ya mama katika lugha ya pili, Wilkins (1972), aligundua kuwa makosa ya matamshi, tahajia, sarufi na msamiati yana mtindo wa kujitokeza katika lugha za wahusika mbalimbali. Hivyo, kutokana na ushahidi wa kasoro ama dosari za lugha, pana uwezekano wa kuainisha athari za lugha ya mama katika lugha ya pili. Anashauri kwamba mazungumzo na maandishi ya mwanafunzi anayejifunza lugha ya kigeni yakichunguzwa, hapana shaka kwamba baadhi ya kasoro zina chanzo chake katika lugha ya mama. Anaeleza kuwa katika jitihada za mwanafunzi kutamka lugha ya kigeni, anaathiriwa na sauti zilizomo katika mfumo wa lugha ya mama na hali za kifonolojia za sauti hizo. Anafafanua kwamba kadri ambavyo tofauti kati ya lugha zinapozidi ndivyo ambavyo vikwazo vya kujifunza lugha ya Kiswahili vinavyoongezeka. Utafiti huu ni wa manufaa kwa kuwa ulitupa msingi wa kuelewa chanzo cha makosa yanayofanywa na

wanafunzi. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na wake kwa njia mbili: Kwanza, utafiti huu umejikita katika athari za lugha ya mama kwa mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili ilhali wetu ulijikita katika makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili. Pili, mtaalamu huyu ametumia Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi ilhali sisi tulitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa.

Naye Onyango (1997), akichunguza athari za lugha ya Kinyala katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, alitambua kuwa wanafunzi wa asili ya Kinyala huhamisha miundo yao ya lugha ya kwanza katika harakati za kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili, hali ambayo inaathiri upataji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Katika kuchunguza matatizo yanayowakabili wanafunzi wakati wa somo la Kiswahili, athari za lugha ya kwanza zimetajwa kama chanzo kikuu cha dosari zilizopatikana katika kazi za wanafunzi. Utafiti wetu ulifaidika na mawazo haya kwa kuwa umefafanua athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Tofauti ni kuwa utafiti wake umejikita katika athari ya Kinyala ilhali wetu ulizamia makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi kutoka kwa wanafunzi wenye asili tofautitofauti.

Akishughulikia suala la kuathiriana kwa Kiswahili na Kigisu nchini Uganda, Haroon (1998), aligundua kuwa Kigisu kiliathiri mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiswahili. Anasema kuwa, kutokana na tofauti za kimuundo kati ya lugha hizi mbili, watafitiwa walihamisha muundo wa nje wa kisintaksia wa lugha yao kwa lugha ya pili (Kiswahili). Hali hii ilikuwa chanzo cha makosa aliyogundua Haroon (1998) katika mpangilio wa maneno katika sentensi zilizotungwa na watafitiwa husika. Utafiti huu ulitufaidi kwa kuwa ulitufafanulia baadhi ya vyanzo vya makosa katika matini za wanafunzi wa shule za upili. Hata hivyo, kazi ya msomi huyu ilitofautiana na yetu kutokana na hali kuwa, mtafiti huyu alijikita katika kipengele cha sintaksia ilhali sisi tulizamia katika kipengele cha semantiki.

Akishughulikia athari ya EkeGusii katika mtihani wa Kiswahili, Mangwa (2004) aligundua kwamba wanafunzi wengi wa asili ya EkeGusii hupoteza alama nyingi insha zao zinaposahihishwa kutokana na athari za makosa ya lugha ya kwanza. Utafiti wa mtaalamu huyu ni wa manufaa kwa kuwa unatupa chanzo cha makosa katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu unahusiana na wetu katika mbinu za ukusanyaji data. Mtaalamu huyu alitumia

insha katika ukusanyaji wa data sawa na utafiti wetu ambapo tulitumia uandishi wa insha katika ukusanyaji wa data. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na wa mtaalamu huyu kwa kuwa alishughulikia suala la athari za EkeGusii kwa Kiswahili ilhali sisi tulizingatia athari za lugha mbalimbali nchini Kenya katika mawasiliano andishi ya Kiswahili.

Naye Mukuthuria (2004) akishughulikia athari ya lugha ya Kitigania kwa lugha ya Kiswahili, aligundua kwamba lugha ya Kiswahili na KiTigania zimeathiriana katika kiwango cha mofolojia. Japo uchunguzi huu ulikuwa umejikita katika kiwango cha mofolojia, ulibainisha kwamba kuna kuathiriana kwa lugha hizi mbili katika viwango vyatya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Utafiti wa mtaalamu huyu ulitusaidia katika kufafanua makosa ya kisemantiki kwa kina, kwa kuwa makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia huchangia makosa mengi ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili. Utafiti huu unahusiana na wetu ambao ulichunguza vyanzo vyatya makosa katika mawasiliano andishi ya Kiswahili. Licha ya hayo, utafiti wetu ulitofautiana na utafiti huo kwa kuwa alizamia watafitiwa kutoka jamii moja (Watigania) nasi tuliwatumia watafitiwa kutoka jamii-lugha mbalimbali.

Akichunguza makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kikamba wanapojifunza Kiswahili sanifu, Mbula (2011) aligundua kuwa lugha ya Kikamba huathiri lugha ya Kiswahili hasa katika fonimu na silabi. Alionyesha jinsi sauti zilivyoongezwa au kudondoshwa katika matumizi ya maneno ya Kiswahili kutokana na athari ya lugha ya Kikamba. Utafiti huu unakaribiana kwa kiasi kikubwa na utafiti tuliofanya kwani utafiti wa mtaalamu huyu umetuwekea msingi wa kuelewa kipengele cha fonimu. Tofauti ya utafiti huu na wetu ni kuwa katika utafiti wetu sisi tuliwatumia watafitiwa kutoka jamii-lugha mbalimbali ilhali Mbula (2011) alijishughulisha na watafitiwa kutoka jamii-lugha moja (Wakamba). Pia, alishughulikia kipengele cha fonimu ilhali sisi tulizamia zaidi katika sauti, neno na sentensi.

Katika utafiti mwingine, Chepkwony (2012) akishughulikia matatizo ya kisarufi mionganii mwa wanafunzi wa Kipsigis wanaojifunza Kiswahili sanifu, aligundua kwamba makosa mengi ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wa Kipsigis yanatokana na athari ya lugha ya Kipsigis. Alitambua kuwa wanafunzi wa Kipsigis huhamisha viambishi kutoka lugha ya Kipsigis na kuviingiza katika Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulitusaidia kutambua makosa ya

kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili. Utafiti huu unahusiana na wetu kwa njia mbili: Kwanza, alitumia uandishi wa insha katika ukusanyaji wa data sawa na mbinu ambayo tulitumia katika utafiti wetu. Pili, mtaalamu huyu alitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa sawa na nadharia ambayo tulitumia katika utafiti wetu. Licha ya hayo, utafiti wetu ulitofautiana na utafiti huo kwa njia nne: Kwanza Chepkwony (2012), alitumia wanafunzi wa shule za msingi (darasa la sita) kama watafitiwa ilhali utafiti wetu ulitumia wanafunzi wa shule za upili (kidato cha tatu) kama watafitiwa; pili, mtafiti huyu alijikita katika shule nne (4) za msingi katika wilaya ya Bomet, sisi tulizamia shule kumi na mbili (12) za upili katika kaunti ya Kakamega; tatu, alitumia watafitiwa kutoka jamii-lugha moja (Kipsigis) ilhali sisi tulitumia watafitiwa kutoka jamii-lugha mbalimbali; nne, msomi huyu alijikita katika kipengele cha sarufi ilhali sisi tulizamia kipengele cha kisemantiki katika kiwango cha neno na sentensi.

2.4 Wataalamu waliojihusisha na Makosa Mbalimbali kwa Lugha Lengwa

Katika utafiti mwingine, Mutungu (2001), akichunguza makosa ya kileksia yanayojitokeza katika insha za wanafunzi wa shule za upili wilayani Kiambu, aligundua kuwa makosa mengi yaliyojitekeza kwenye insha za wanafunzi yanatokana na athari ya lugha ya kwanza, kutojua mipaka ya sheria, tafsiri na utohozi usiofaa, upungufu wa misamiati na mbinu dhaifu za ufundishaji. Utafiti wa mtaalamu huyu ulikuwa wa manufaa kwa kuwa ulitupa vyanzo vya makosa katika lugha ya Kiswahili. Utafiti wake unahusiana na wetu katika mbinu za ukusanyaji wa data. Mtaalamu huyu alitumia uandishi wa insha katika ukusanyaji wa data sawa na sisi ambao tulitumia uandishi wa insha katika ukusanyaji wa data. Hata hivyo, utafiti huo ulitofautiana na wetu kwa njia tatu: Kwanza, mtaalamu huyu alitumia nadharia ya Lugha Kadirifu ilhali sisi tulitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa; pili, mtafiti huyu alitumia wanafunzi wa kidato cha pili kama watafitiwa ilhali utafiti wetu uliwatchumia wanafunzi wa kidato cha tatu kama watafitiwa; tatu, mtaalamu huyu alijikita katika shule tano (5) wilayani Kiambu ilhali sisi tulijikita katika shule kumi na mbili (12) katika kaunti ya Kakamega.

Katika utafiti mwingine, MBAABU (1995), akichunguza maingiliano ya lugha za kwanza na Kiswahili sanifu, alitambua kuwa makosa yanayofanywa na watu yanaweza kugawanywa katika makundi manne ambayo ni kundi la kimatamshi, kisarufi, kimaana na kimaandishi.

Makundi haya manne huingiliana kiasi kwamba kosa la kimatamshi linaweza pia kuwa la kisarufi na linaweza kuathiri maana ya matamshi au maandishi. Anaendelea kusositiza kuwa mengi ya makosa ya kimatamshi yanatokana na mwingiliano wa lugha za kwanza na Kiswahili sanifu. Kila lugha inayo mpangilio maalumu wa sauti ambazo hupatikana katika maneno ya lugha hiyo. Makosa mengi ya kisarufi yanahu kuchanganya viambishi vya ngeli tofauti, hasa viambishi vya hali ya umoja na wingi wa ngeli, pamoja na viambishi vya ngeli nyingine. Makosa ya kimaana kwa wingi yanababishwa na upungufu wa msamiati pamoja na athari za lugha za kwanza. Makosa ya kimaandishi husababishwa na makosa ya kimatamshi.

Pia, MBAABU (1978), alishughulikia asili ya Kiswahili, kukua na kuenea kwake pamoja na kuchunguza lajaja kuu za lugha ya Kiswahili. Pia, kwa kiasi alishughulikia fonolojia ya Kiswahili na mofolojia alipojihusisha na ngeli za Kiswahili. Aligundua kuwa Kiswahili kimeathiriwa sana na lajaja kuu za Kiswahili. Vilevile MBAABU (1985), alifanya utafiti ambao haukuwalenga wanafunzi darasani. Alichunguza makosa ya kisarufi na kifonolojia yanayofanywa na Wakenya mbalimbali wanaojifunza Kiswahili. Alisema kuwa baadhi ya makosa yalitokana na lugha ya kwanza. Aligundua kuwa sauti zilidondoshwa katika matumizi ya maneno katika Kiswahili kutokana na athari ya lugha ya kwanza. Kwa upande wa sarufi, aligundua kuwa viambishi vilivyo hamishwa kutoka lugha ya kwanza na kuingizwa katika lugha ya Kiswahili vilisababisha makosa ya kimuundo. Kazi hizi za MBAABU (1978, 1985), zilikuwa na manufaa makubwa kwa utafiti wetu kwa kugundua kuwa lugha ya kwanza na lajaja mbalimbali katika kaunti ya Kakamega ziliathiri lugha ya mwanafunzi kwa upande wa kisemantiki. Hata hivyo, kazi za mtafiti huyo zilitofautiana na utafiti wetu kutokana na mambo mbalimbali. Kwanza, MBAABU (1978) alishughulikia asili ya Kiswahili, kukua na kuenea kwake ilhali sisi tulishughulikia makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili. Pili, mtaalamu huyu alijikita katika vipengele vya sarufi, fonolojia na mofolojia alipojihusisha na ngeli, wakati ambapo tulijikita katika kipengele cha semantiki pekee. Tatu, MBAABU (1985), alifanya utafiti usiowalenga wanafunzi darasani, bali Wakenya mbalimbali wanaojifunza Kiswahili ilhali wetu uliwalenga wanafunzi wa shule za upili, kidato cha tatu kaunti ya Kakamega.

Mbaabu (1995), anaendelea kusema kuwa mbali na makosa yanayosababishwa na athari za lugha za kwanza, makosa mengine ambayo yanakilemaza Kiswahili sanifu ni maandishi ya tungo za Kiswahili hasa tenzi na mashairi. Katika lugha ya kishairi, mshairi anao uhuru wa kutumia lugha kilahaja au kwa njia apendayo ili atimize urari wa vina na mizani katika tungo zake. Baadhi ya walimu hufunza mashairi hayo bila kueleza kwamba ipo tofauti kati ya tungo hizo na Kiswahili sanifu. Katika maandishi ya insha ni makosa kutumia lugha ya ushairi. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa umeshughulikia maingiliano ya lugha za kwanza na Kiswahili sanifu na matumizi ya lugha ya kishairi katika Kiswahili sanifu ilhali wetu ulishughulikia makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za upili. Utafiti huu ultufaa kwa kutufafanulia makosa ya maingiliano ya lugha za kwanza na Kiswahili sanifu na athari za lugha ya kishairi katika uandishi wa insha.

Moshi (1971), alichunguza maneno ya Kiswahili na Kiingereza yaliyokopwa na lugha ya Kiganda. Alishughulikia athari ya hizi lugha katika vima vya kifonolojia na mofolojia. Alitilia mkazo kuwa lugha za Kiafrika sharti zikope ili kukabiliana na hali ya mpito ambayo inahitaji Waafrika kubadilishana mifumo yao ya kisiasa, kijamii na kiuchumi ili iwiiane na msukumo wa mahitaji ya kisiasa. Utafiti wake Moshi (1971) ultiusaidia katika utafiti wetu kwa kugundua kuwa watafitiwa waliathiriwa na lugha ya Kiingereza na Sheng katika uandishi wao na hatimaye kuchangia makosa katika matumizi ya Kiswahili. Hata hivyo, kazi hiyo ilitofautiana na utafiti wetu kwa kuwa wakati msomi huyo aliangazia maneno katika lugha mbili (Kiswahili na Kiingereza) yanayokopwa na lugha ya Kiganda, sisi tulishughulikia makosa ya kisemantiki katika lugha ya Kiswahili hasa kwa wanafunzi wa shule za upili

2.5 Wataalamu Waliojihusisha na Athari za Lugha Mbalimbali katika Kiingereza

Katika uchunguzi wake wa kina kuhusu jinsi lugha za kwanza za watoto wa shule kutoka baadhi ya jamii za Kenya zinavyoingiliana na kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiingereza, Njoroge (1987), aligundua kuwa athari mionganoni mwa watoto hupungua vile

wanavyoendelea kujifunza lugha ya Kiingereza na kuna uwezekano wa athari hizo kutoweka kabisa. Anasisitiza kuwa katika harakati za ujifunzaji lugha ya pili watoto huathiriwa na miundo ambayo wanajua kutokana na lugha ya kwanza. Anaendelea kutufahamisha kwamba ujifunzaji wa lugha ya pili kwa kawaida hufanyika baada ya ujifunzaji lugha ya kwanza kukamilika. Mawazo ya msomi huyu yalitusaidia katika utafiti wetu ambapo tuligundua kwamba athari ya lugha ya kwanza ilichangia makosa ya kisemantiki katika Kiswahili andishi. Hata hivyo, utafiti huo wa Njoroge (mtaje) ulikuwa tofauti na utafiti wetu kwa kuwa wakati msomi huyo aliangazia jinsi lugha ya kwanza inavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiingereza, sisi tulizamia katika vyanzo anuwai nya makosa ya kisemantiki na uhamishaji hasi kutoka lugha ya kwanza. Pia, Njoroge (mtaje), aliangazia watoto wa shule kwa ujumla ilhali sisi tuliangazia watafitiwa bainifu wa shule za upili, kidato cha tatu. Isitoshe, Njoronge ameeleza jinsi lugha ya kwanza inaathiri Kiingereza ilhali utafiti huu unachanganua vyanzo nya makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili.

Spada na Lightbourn (1999), wakichunguza makosa yanayojitokeza katika uandishi wa Kiingereza uliofanywa na wanafunzi wa Kijapani, wanasema kuwa ni vigumu kutambua chanzo cha makosa na si dhahiri kubaini sababu za wanafunzi kufanya makosa. Waligundua kuwa wanafunzi wakati mwingine wanapuuza kutumia alama za kisarufi zinazohitajika katika lugha ambazo wanachukulia kuwa ngumu. Hali hii humwacha msomaji bila ujumbe kumhusu mwanafunzi anayejifunza lugha. Jambo hili hutokea kwa kutojua taratibu na namna lugha ya pili inavyofanya kazi. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa umeshughulikia athari ya Kijapani kwa lugha ya Kiingereza bali wetu ulishughulikia athari mbalimbali katika lugha ya Kiswahili mbali na lugha ya kwanza. Hata hivyo tulifaidika na utafiti wao katika kutambua sababu zinazowafanya wanafunzi kufanya makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili.

Katika utafiti uliofanywa na Gouala (1991), juu ya athari za lugha asili kwa lugha ya Kiingereza nchini Kongo katika matamshi na muundo wa ripoti, alielezwa kwamba wanafunzi hukumbwa na matatizo katika matamshi na muundo wa Kiingereza kwa sababu ya lugha zao za asili. Hii inaonyesha kwamba mwanafunzi huathiriwa na lugha ya asili katika uwezo wake wa kupata Kiingereza. Aligundua kuwa katika sehemu za mashambani

hali halisi inaonyesha kuwa lugha za asili zinatumiwa kufundishia hadi darasa la mwisho la shule za msingi. Kazi ya Gouala (mtaje) ni tofauti na utafiti wetu kwa njia mbili: Kwanza, alijikita katika athari za lugha asili kwa lugha ya Kiingereza ilhali sisi tulizamia katika makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili; pili, eneo la utafiti ni tofauti na letu. Msomi huyu alifanya utafiti wake katika nchi ya Kongo ilhali sisi tulifanya utafiti wetu katika taifa la Kenya, kaunti ya Kakamega.

Muchome (1998), alichunguza mahusiano kati ya Cinamwanga na Kiingereza. Masuala aliyoyatilia maanani ni ujuzi wa lugha na tabia za kiisimu zinazotokana na mahusiano ya lugha hizi mbili. Madhumuni yake yalikuwa, kutoa maelezo ya kiisimu yanayotokana na maingiliano ya Cinamwanga na Kiingereza. Athari za ubadilishanaji wa ndimi ni mionganoni mwa masuala aliyoyatifi huku akizingatia matumizi ya lugha katika muktadha wa ofisi na mionganoni mwa wakulima. Akitumia Nadharia ya Kijamiinafsia (Mackey, 1968), alibainisha kuwa lugha ya Cinamwanga ina athari za lugha ya Kiingereza. Hatimaye ilidhihirika kuwa athari zilizotokana na Cinamwanga ziliingia katika lugha ya Kiingereza. Kazi ya msomi huyo ilikuwa ya manufaa kwetu kwa kuibua suala la maingiliano ya lugha na baadaye kuathiriana. Tuligundua kuwa wanafunzi wengi walikuwa wameathiriwa na lugha za kienyeji na lugha ya Kiingereza katika uandishi wao wa insha. Kazi ya Muchome (mtaje), ilitofautiana na yetu kwa njia nne kuu: Kwanza, wakati mtafiti huyu aliangazia mahusiano kati ya lugha ya Cinamwanga na Kiingereza, sisi tulizamia katika makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili. Pili, mtafiti huyu alitumia Nadharia ya Kijamiinafsia (Mackey, 1968) katika utafiti wake ilhali sisi tulitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Tatu, mtafiti huyu alifanya utafiti wake katika maeneo ya Jamhuri ya Uganda, kwa kabila la Cinamwanga pekee ilhali sisi tulijikita katika taifa la Kenya, kwa jamii-lugha mbalimbali katika kaunti ya Kakamega. Nne, wakati mtafiti huyu aliwatumia wafanyakazi katika ofisi mbalimbali na wakulima kama watafitiwa wake, sisi tuliwatumia wanafunzi wa shule za upili ili kupata data ya utafiti huu.

Kwa mujibu wa Nabea (2009), lugha ya Kiswahili na Kiingereza zimeathiriana kiasi kwamba wenye uwezo wa kuzungumza lugha hizi hubadilisha msimbo wanapozungumza, na Kiingereza hutumika na leksia ya lugha za kienyeji. Alichunguza lugha ya Kimeru na

kubaini kwamba wazungumzaji wa Kimeru hukopa maneno ama kutoka kwa Kiswahili au Kiingereza na kuyaingiza katika muundo na mofolojia ya Kimeru. Mfano:

Bantrain (They trained me) train + Meru structure

Gatwaforcethilwe (We were forced) force + Meru structure

Nitwavamiilwe (We were attacked) Kiswahili + Meru structure

Mifano iliyo hapo juu inaonyesha kuwa Kimeru kimeathiriwa na Kiswahili na Kiingereza katika kiwango cha kimofolojia hivi kwamba pahali ambapo kuna pengo la msamati, lugha hizi hujaza pengo hilo na kurahisisha mawasiliano. Utafiti wa mtaalamu huyu unahusiana na wetu uliochunguza vyanzo vya makosa ya kisemantiki katika lugha ya Kiswahili. Hata hiyo, kazi ya mtaalamu huyu ilitofautiana na utafiti huu kwa njia tano (5) kuu: Kwanza, wakati ambapo msomi huyu alijikita katika jamii lugha moja pekee ya Wameru, sisi tulizamia jamii-lugha mabalimbali; pili, Nabea (mtaje), alishughulikia kipengele cha mofolojia ilhali sisi tulichunguza makosa ya kisemantiki; tatu, wakati sisi tulijikita katika maeneo ya Kakamega kwa minajili ya kupata data iliyofanikisha utafiti wetu, msomi huyu alizamia maeneo ya Meru; nne, mtaalamu huyu alitumia mbinu ya matamshi ili kupata data yake ilhali sisi tulitumia uandishi wa insha; tano, wakati sisi tulitumia lugha moja tu ya Kiswahili, mtafiti huyu alitumia athari ya lugha mbili (Kiingereza na Kiswahili).

Mwangi (2011), alishughulikia makosa ya kimofosintaksia katika uandishi wa Kiingereza yanayojitokeza katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili jijini Nairobi. Aligundua kuwa makosa hutokana na mnyambuliko mbaya wa vitenzi, matumizi mabaya ya vihusishi, vivumishi, virejeshi, viunganishi, njeo na hali, mpangilio wa maneno katika sentensi na upatanisho wa kisarufi (ngeli) usiofaa. Utafiti huu ni wa manufaa kwa kuwa ulitupa msingi wa kuelewa baadhi ya sababu zinazochangia makosa katika lugha. Utafiti huu unahusiana na wetu kwa nadharia ya utafiti kwa kuwa mtafiti huyu alitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa sawa na nadharia ambayo tulitumia katika utafiti wetu. Pia, alitumia watafitiwa wa shule za upili sawa na utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti wetu ulitofautiana na utafiti huo kwa kuwa alipania makosa ya kimofosintaksia ilhali sisi tulijikita kwa kina katika makosa ya kisemantiki katika viwango vya neno na sentensi. Pia,

utafiti wa msomi huyu ulijikita katika lugha ya Kiingereza ilhali sisi tulizamia lugha ya Kiswahili.

Akijishughulisha na makosa yanayojitokeza katika uandishi wa Kiingereza uliofanywa na wanafunzi wa Kichina, Jie (2010) alitambua kuwa uhamishaji hasi kutoka lugha ya mama, kutojua mpangilio wa maneno katika Kiingereza, matumizi ya kanuni za Kichina na maneno yenye utata kuandika sentensi katika Kiingereza huchangia baadhi ya makosa katika lugha ya Kiingereza. Pia, aligundua kuwa wanafunzi wengi wa Kichina huwa na maneno sahihi lakini hawajui jinsi ya kuyatumia kwa sababu utaratibu wa kuandika sentensi katika Kiingereza ni tofauti na Kichina. Utafiti wake ulifaidi utafiti wetu katika upande wa vyanzo vya makosa. Tofauti ni kwamba mtaalamu huyo alitumia watafitiwa wa Kichina pekee ilhali wetu ultumia watafitiwa kutoka jamii-lugha mbalimbali. Pili, katika utafiti wetu tulitumia lugha ya Kiswahili ilhali utafiti huo ultumia lugha ya Kiingereza.

Akishughulikia makosa yanayofanywa na wanafunzi wa Kiarabu waliokuwa wakijifunza Kiingereza kama lugha ya pili, AbiSamra (2003), alitambua kuwa uhamishaji hasi kutoka lugha ya kwanza na hali za mumo kwa mumo huchangia baadhi ya makosa katika lugha ya Kiingereza. Aligundua kuwa wengi wa wanafunzi wa Kiarabu walikuwa na makosa ya kisarufi, kisintaksia, uakifishaji mbaya, kileksia, kisemantiki na kutozingatia kanuni za uandishi wa insha. Licha ya utafiti huu kuchunguza lugha ya Kiingereza ultiufaa kwa kutufafanulia baadhi ya makosa yanayofanywa na wanafunzi katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Utafiti wake Abisamra (mtaje) ulifanana na wetu katika upande wa nadharia. Tofauti ni kwamba, msomi huyu alitumia watafitiwa wa Kiarabu pekee ilhali wetu ni mpana kwa kuwa uliwaluhusisha watafitiwa kutoka jamii-lugha mbalimbali nchini Kenya. Pia, ye ye alitumia lugha ya Kiingereza ilhali sisi tulitumia lugha ya Kiswahili.

Naye Noor (1996), akiangazia makosa ya kisintaksia yanayofanywa na wanafunzi wa Kiarabu wanaojifunza Kiingereza, aligundua kuwa wanafunzi wengi wa Kiarabu walihamisha sheria za lugha ya Kiarabu katika utungaji wa sentensi kwa lugha ya Kiingereza. Waliakifisha sentensi zao visivyo na kuchangia makosa mengi ya kisintaksia. Licha ya utafiti huo wa Noor (1996) kuangazia makosa ya kisintaksia katika lugha ya Kiingereza, utafiti huo ultiufaa kwa kufafanua baadhi ya makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili. Hata hivyo, utafiti huu ultiufautiana na wa msomi

huyu kwa njia tatu kuu: Kwanza, wakati sisi tulitumia watafitiwa kutoka jamii-lugha mbalimbali, mtafiti huyu alitumia watafitiwa kutoka jamii-lugha moja ya Kiarabu pekee; pili, msomi huyu aliangazia makosa ya kisintaksia ilhali sisi tulijikita katika makosa ya kisemantiki; tatu, wakati mtafiti huyu aliangazia lugha ya Kiingereza, sisi tuliangazia lugha ya Kiswahili.

Akishughulikia tafsiri sisisi Ontieri (2011) anasema kuwa makosa yanayotokana na tafsiri sisisi kutoka lugha mbalimbali za kwanza pamoja na Kiingereza, huathiri lugha lengwa (Kiswahili). Alitambua kuwa makosa hutokana na kuhamishwa kwa miundo na maumbo kutoka lugha za kwanza hadi lugha ya pili kwa njia isiyokubalika. Vipengele vilivyoathiriwa zaidi na hali hii ni maneno, sehemu ya tungo, na hata tungo nzima. Utafiti huu ulituwezesha kuelewa baadhi ya vyanzo vya makosa yanayofanywa na wanafunzi katika uandishi wa insha. Licha ya hilo, utafiti wetu ultofautiana na utafiti huo kwa kuwa amechunguza makosa yanayotokana na tafsiri sisisi ilhali wetu ulishughulikia makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili.

2.6 Wataalamu Waliochanganua Makosa kwa Lugha za Kigeni

Wakifanya utafiti kuhusu makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ngeni, Burt na Kiparsky (1972), waligundua kuwa wanafunzi walihamisha miundo ya lugha zao za kwanza kwa lugha ngeni. Hali hii ilivuruga maana ya sentensi kutokana na matumizi mabaya ya viunganishi. Utafiti huu unahusiana na wetu kwa njia moja; wataalamu hawa walitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa sawia na nadharia tuliyotumia katika utafiti wetu. Maoni ya wataalamu hawa, yalitoa mwanga kuhusu uhamishaji kutoka lugha moja hadi nyingine na namna unavyotatiza ujifunzaji wa lugha ya pili. Pia, utafiti huu ultusaidia katika kuchunguza vyanzo vya makosa ya kisemantiki katika utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti wa Burt na Kiparsky (1972), unatofautiana na wetu kwa njia mbili: Kwanza, wakati wataalamu hawa walijikita katika wanafunzi kwa jumla, sisi tulizama katika shule za upili, kidato cha tatu, kaunti ya Kakamega. Pili, utafiti huu uliangazia makosa yanayofanywa na wanafunzi kwa jumla ilhali utafiti wetu ulijikita katika makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili.

Bakari (1982), ambaye alichunguza mofolojia ya lahaja za Kiswahili, alisema kuwa Kiswahili kimeathiriwa na lugha za kigeni kama vile Kiarabu, Kiingereza na Kireno. Kwa mfano:

Karate - Kireno

Gazeti - Kiingereza

Kamili - Kiarabu

Vilevile alisema kuwa Kiswahili kimekopa kutokana na lugha za bara. Naye Kembo-Sure (1996), anaungana na Bakari (1982), kwa kusema kuwa, njia rahisi lugha inaweza kuathiri nyingine ni kupitia ukopaji wa maneno. Mtaalamu huyu anaendelea kusema kuwa, Kiswahili kina maneno mengi yenye asili ya Kiarabu, lakini si Kiswahili peke yake kilicho hivyo, Kihausa (Afrika Magharibi) na Kimalay (Malaysia) hali zao ni kama Kiswahili. Zote zina maneno chungu nzima yenye asili ya Kiarabu na fungamano la Uislamu. Maoni ya wataalamu hawa yalitusaidia katika utafiti wetu kwa kugundua kuwa Kiswahili kimeathiriwa sana na lugha ya Kiingereza, Kireno na Kiarabu na kusababisha makosa ya kisemantiki katika utungaji wa sentensi na uandishi wa insha. Tuligundua kuwa baadhi ya wanafunzi walikopa msamiati wa lugha ya Kiingereza na kuutumia katika uandishi wao ili kukidhi mahitaji yao. Hata hiyo, utafiti huo ulitofautiana na wetu, kwa kuwa Bakari (1982) alichunguza jinsi Kiswahili kimeathiriwa na lugha za kigeni ilhali sisi tulijikita katika makosa ya kisemantiki katika matini za wanafunzi wa shule za upili.

Akichambua sababu zilizopelekea lugha kuathiriwa kisarufi alipokuwa akishughulikia udhaifu wa ngeli za kimofolojia za Kiswahili, Mukuria (2002), anadai kuwa nomino nyingi za mkopo katika Kiswahili hazina viambishi na hivyo hali hii huzua utata wa kuzainisha katika makundi hasa kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Pia, nomino zingine zinaweza kuwa na viambishi sawa lakini zikizingatia uwiano wa kisarufi usiolingana na makundi husika ya nomino, viambishi vingine vya kimofolojia vikijumlishwa katika matumizi kwa sababu ya kukosa umilisi wa lugha vinaweza kuzua mpotosho, na tatizo la baadhi ya nomino kuwa katika hali ya wingi. Hakuzamia makosa ya kisemantiki ila anatoa pendekazo la kukabiliana na hali hii kama matumizi ya mbinu ya kimuundo katika kufundisha sarufi ya Kiswahili. Kazi hii ya Mukuria (mtaje), ilitufaidi

sana katika utafiti wetu kwa kuangazia nomino za mkopo na athari zake katika taluumma ya semantiki, kupitia data iliyofanikisha utafiti huu wetu. Tofauti iliyopo kati ya tafiti hizi mbili ni kuwa, wakati mtaalamu huyu alipozamia ngeli na uwiano wake, sisi tujikita katika makosa ya kisemantiki

Akiangazia jinsi ambavyo lugha ya Kiswahili inavyoweza kukuzwa kwa upande wa msamiati pamoja na lugha za kienyeji, Ryanga (2000), anaeleza kuwa kukuza Kiswahili kama lugha ya taifa kuandamane na ukuzaji wa msamiati wa lugha za kienyeji ili ziweze kusaidiwa kutumika katika miktadha mbalimbali ya kisiasa, hasa katika karne hii ya ishirini na moja (21). Aidha, aliongezea kuwa, hali hii ingewezesha kuingiliana na dhana mpya za kiteknolojia katika matumizi, hasa ya karne hii ya 21. Ryanga (mtaje), anaendelea kusema kwamba, kukopa istilahi hizo zilizoundwa kidesturi na ambazo zimekubalika kwa urahisi na wazungumzaji, kungesaidia kiwango cha lugha za Kiafrika kujitajirisha kimsamiati baina yao kabla ya kukopa kutokana na lugha za kigeni. Alishauri kuwa, Kiswahili kingeepuka athari nyingi za kigeni na kujikita katika sarufi na msamiati wa asili ya Kiafrika, hali ambayo ingeimarisha uafrika na ubantu. Maoni ya mtaalamu huyu yalikuwa muhimu katika utafiti huu ambapo tuligundua misamiati migeni katika matini za watafitiwa kutokana na maendeleo ya teknolojia mpya, hususani mtandao. Baadhi ya istilahi zilichangia makosa ya kisemantiki, kwa sababu watafitiwa walizitumia pasi kujua maana halisi ya istilahi husika. Hata hivyo, utafiti wetu ulikuwa tofauti na wa mtaalamu huyo kwa kuwa tulichunguza makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili ilhali msomi huyu alijikita katika ukuzaji wa Kiswahili sambamba na lugha za kienyeji ili kuunda misamiati mipy badala ya kukopa kutoka kwa lugha za kigeni na kuathiri lugha ya Kiswahili.

2.7 Wataalamu Waliojihusisha na Vyanzo vya Makosa Mbalimbali

Furaha (2001), alishughulikia vyanzo vya makosa ya kisintaksia katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili mionganini mwa Waidakho. Madhumuni ya utafiti huo yalikuwa kujua iwapo Kiidakho, kama lugha moja ya kwanza, huathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili katika ngazi ya kisintaksia mionganini mwa wanafunzi katika Ikolomani wilaya ya Kakamega, mkoa wa Magharibi mwa Kenya. Kutokana na matokeo ya utafiti na mjadala uliofanyika katika ripoti hii, ni dhahiri kwamba Kiidakho

kama lugha ya kwanza kwa msemaji ambaye anajifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili husababisha makosa ya kisintaksia. Alihitimisha kuwa, walimu wa Ikolomani, idara ya Kiswahili wanapaswa kutambua tofauti kati ya Kiidakho na lugha ya Kiswahili na uainishaji wa nomino ili kufundisha Kiswahili kwa ufanisi. Kazi ya mtafiti huyu ilikuwa ya manufaa katika utafiti wetu, kwa kuwa iliweka wazi kuwa Kiidakho huathiri lugha ya Kiswahili kisintaksia. Pia katika utafiti wetu tuligundua kuwa wanafunzi katika kaunti ya Kakamega waliathiriwa na lugha zao za kwanza katika uandishi wao na kusababisha makosa ya kisemantiki. Utafiti wa mtaalamu huyu ulihusiana na wetu kwa njia mbili: Kwanza, Furaha (mtaje) alifanya utafiti wake katika maeneo ya Kakamega sawia na utafiti wetu; pili, alitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa sawia na nadharia tuliyotumia katika utafiti wetu. Hata hivyo, kazi ya msomi huyu ilitofautiana na kazi yetu. Wakati mtafiti huyu alitumia wanafunzi wa jamii-lugha moja tu ya Waidakho, sisi tuliwatumia watafitiwa kutoka jamii-lugha mbalimbali. Pia, tulizamia makosa ya kisemantiki ilhali mtafiti huyu alijikita katika kipengele cha sintaksia.

Naye Wanyoike (1978), alishughulikia fonolojia ambapo anaonyesha mifano mbalimbali ya ukiukaji wa kanuni za matumizi ya Kiswahili sanifu unaofanywa na wanafunzi kutoka jamii kadhaa nchini Kenya kama Wajaluo, Wakikuyu, Wakamba, Wahindi na Wakalenjin. Aligundua kuwa wanafunzi kutoka jamii hizi waliathiriwa na lugha zao za kwanza na kusababisha makosa mengi ya kisarufi katika maandishi yao ya lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwetu kwani ulitusaidia kugundua kuwa wanafunzi mbalimbali walikiuka kanuni za lugha ya Kiswahili katika utungaji wa sentensi na kuchangia makosa ya kisemantiki katika kazi zao. Pia, waliambisha viambishi mbalimbali kwa baadhi ya nomino ambazo kwa kawaida haziambishwi. Tofauti kati ya tafiti hizi mbili ni kuwa, Wanyoike (mtaje) alijikita katika jamii-lugha tano (5) pekee ilhali sisi tujikita katika jamii-lugha mbalimbali za Jamhuri ya Kenya. Pia msomi huyu alishughulikia kipengele cha fonolojia ilhali sisi tuliangazia kipengele cha semantiki.

Muthu (2005) akishughulikia makosa ya kisintaksia katika tafsiri za makala ya gazeti la *Taifa Leo*, aligundua kuwa waandishi wengi hufanya makosa wakati wanapojishughulisha na vipashio vingine muhimu vya kisintaksia katika tafsiri, dhamira, hali, njeo na usawazishaji wa utamaduni katika lugha ya Kiswahili. Muthu (mtaje), alipendekeza tafiti

zaidi zifanywe kuhusu makosa kwa kuwa jamii tofauti nchini Kenya zimeingiliana na kusababisha hali ambapo mara nyingi haiwezekani tena kuyahusisha makundi mbalimbali ya watu na lugha moja. Hali hii huchangia kuwepo kwa makosa kutokana na watu kuzijua lugha zaidi ya moja. Tofauti na utafiti huo ni kuwa amechunguza makosa ya kisintaksia katika magazeti (*Taifa Leo*) ilhali sisi tulichunguza makosa ya kisemantiki katika matini za wanafunzi wa shule za upili.

Naye Hermes (1972), akiangazia makosa yanayofanywa na wanafunzi wanapozungumza na kuandika. Aligundua kuwa makosa hutokea kwa kuacha baadhi ya elementi zinazohitajika au kuongeza elementi zisizohitajika au kuchagua elementi isiyo sahihi au kupanga maneno visivyo. Aliendelea kusema kuwa njia hizi pekee hazitoshii katika kuchanganua makosa yanayofanywa na wanafunzi. Tanzu za mofolojia, sintaksia na leksia sharti zihuishwe katika uchanganuzi makosa. Kazi hii ilitoa mwanga kwa utafiti huu hasa katika aina ya makosa yanayofanya na wanafunzi katika uandishi wao. Utafiti wa Hermes (mtaje) ulihusiana na wetu kwa kuwa alitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa sawa na tuliyotumia katika utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti huo ulitofautiana na wetu kwa kuwa mtafiti huyo alikusanya data akitumia mazungumzo na maandishi ilhali utafiti wetu ulikusanya data kwa njia ya maandishi pekee. Pia, Hermes (mtaje), alianganzia makosa ya wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili kwa jumla wakati sisi tulijikita katika makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili, hususani kidato cha tatu, kaunti ya Kakamega.

Dulay na Burt (1974) wakishughulikia makosa yanayofanywa na wale wanaojifunza lugha ya pili, waligundua kuwa makosa mengi hutokana na lugha hiyo na wala hayasababishwi na lugha ya kwanza na yana chanzo chake mumo humo katika lugha hiyo. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa umeshughulikia makosa ya kijumla yanayofanywa na wale wanaojifunza lugha ya pili ilhali wetu ulishughulikia makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi kwa wanafunzi wa shule za upili. Hata hivyo, maoni ya mtaalamu huyu yalikuwa ya manufaa katika utafiti wetu, kwa kutufafanulia baadhi ya vyanzo vya makosa yanayofanywa na wale wanaojifunza lugha ya pili.

Wakishugulikia makosa yanayofanywa na mtu anayejifunza lugha ya pili, Richards (1974) na Brown (1994) waligundua kuwa makosa ya mtu anayejifunza lugha ya pili yaweza

kusababishwa na ujumlishaji uliokithiri, upuuzaaji wa kanuni, kutozingatia kanuni kikamilifu, kuazima ruwaza kutoka kwa lugha ya kwanza na kutanua ruwaza kutoka kwa lugha ya pili. Kazi ya wataalamu hawa ilitufaa sana katika utafiti wetu kwa kutufafanulia baadhi ya visababishi vya makosa katika lugha ya Kiswahili. Utafiti wao unatofautiana na wetu kwa kuwa sisi tulishughulikia makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili ilhali utafiti wao ulijihuisha na makosa yanayofanywa na mtu anayejifunza lugha ya pili.

Akichunguza makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili, Lengo (1995), aligundua kuwa makosa yameenea kwa kutozingatia sheria za lugha lengwa. Matumizi ya wakati uliopita katika vitenzi, ujumlishaji uliokithiri na matumizi ya nyakati mbili tofauti katika sentensi moja huchangia makosa katika lugha. Makosa haya hujitokeza sana kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili bila kuzingatia mfumo wa lugha ya kwanza. Utafiti wa mtaalamu huyo ilitusaidia katika kuchanganua kwa kina makosa tuliyobainisha katika matini za wanafunzi wa shule za upili na kuweka wazi vyanzo vya makosa husika. Kazi yake Lengo (mtaje), ilikuwa na uhusiano na utafiti huu kwa kuwa mtaalamu huyo alitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa sawa na nadharia tuliyotumia katika utafiti wetu. Hata hivyo, kazi hiyo ilitofautiana na utafiti wetu, kwa kuwa mtafiti huyo alichunguza makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili pasi kuangazia kiwango ilhali katika utafiti wetu tulichunguza makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili, kidato cha tatu, kaunti ya Kakamega.

Nurse (1986), alishughulikia lugha za kibantu katika eneo la Afrika Mashariki. Katika kazi yake, alishughulikia ushahidi wa kiisimu unaothibitisha nyendo za Wabantu na wakati walipokuja na kukalia eneo la Afrika Mashariki. Kilicho na umuhimu katika kazi ya Nurse (mtaje) ni kuwa, alikiri kwamba wazungumzaji wa lugha tofauti wanapokutana huathiriana. Aliendelea kusema kuwa, kuathiriana kunaweza kuwa kwa msamiati, wakati mwingine kwa fonolojia na mofolojia. Hata hivyo, alisema kuwa pana hali chache sana ambapo lugha huchanganyikana na kuzua pijini. Kazi ya mtaalamu huyu ilitusaidia katika utafiti wetu kwa kutuangazia kuwa wanafunzi wanapobadilisha makazi yao, pana uwezekano wa lugha yao kuathirika na kuchangia makosa ya kisemantiki katika uandishi wao wa Kiswahili. Tofauti iliyopo na utafiti huu ni kuwa, msomi huyu aliangazia nyendo

za Wabantu kwa kijumla, ilhali sisi tulijikita katika wanafunzi wa shule za upili kutoka jamii mbalimbali. Pia, Nurse (mtaje) alishughulikia makosa katika kiwango cha msamiati, fonolojia na mofolojia, ilhali sisi tulijikita katika kipengele cha semantiki.

Naye Adam (2000), alibaini kuwa, shuruti za lugha za kuhudumia watumizi wake kulingana na kiwango cha maendeleo ni chanzo cha lugha kuathiri na kuathiriwa. Akizungumzia jinsi ambavyo athari zinajilingiza katika lugha yoyote ile, anasema kuwa kadri mawazo, ujuzi na matamano ya watu yanavyobadilika au kupanuka, lugha nayo kwa haraka, hujizoesha hali hiyo mpya kwa kupanuka. Anadai kuwa, hali hii husababisha makosa mbalimbali katika lugha husika ya Kiswahili. Maoni ya Adam (mtaje), yalikuwa na uzito katika utafiti wetu, kwa kuweka wazi hali ya lugha kuathiriana na kusababisha makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wengi katika utafiti wetu waliathiriwa sana na lugha ya Kiingereza, Sheng' na lugha ya kwanza na kusababisha makosa ya kisemantiki katika insha zao. Licha ya hayo, kazi ya mtafiti huyu ilikuwa tofauti na yetu kwa kuwa, akiangazia jinsi athari zilivyojiingiza katika lugha yoyote ile ilhali sisi tulijikita katika makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya lugha ya Kiswahili.

Naye Ontieri (2010), akiangazia makosa katika insha za wanafunzi wa shule za upili (Wilaya ya Nakuru) aligundua kuwa wanafunzi husika walitumia lugha iliyovurugika kutokana na makosa ya kisarufi, kitahajia na kimsamiati. Jambo hili hupelekea watahiniwa kupoteza alama nyingi wakati wa kusahihishiwa kazi zao. Ontieri (mtaje), alipendekeza kuwa tafiti zaidi zifanywe ili kuweka wazi vyanzo vya makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika mawasiliano andishi ya Kiswahili mbali na yale yaliyo na chanzo chake katika lugha ya kwanza. Mapendekezo ya mtaalamu huyu yaelekea kupata jibu kutokana na utafiti huu. Utafiti wa msomi huyu ulitufaa kwa kutuelekeza kutambua vyanzo vya makosa katika insha za wanafunzi wa shule za upili. Licha ya hayo, utafiti huu unahusiana na wetu katika mbinu za ukusanyaji wa data na watafitiwa. Msomi huyu alitumia watafitiwa wa shule za upili kama sisi. Aidha, alitumia mjarabu katika ukusanyaji wa data sawa nasi. Tofauti kati ya utafiti huu na wetu ni kuwa wakati msomi huyu alizamia katika kuchunguza makosa yanayojitokeza katika vipengele vitatu vya kisarufi, tahajia na

msamiati, utafiti wetu ulijikita katika makosa yanayojitokeza katika viwango vya neno na sentensi.

Naye Murioki (2012), akiangazia makosa yanayofanywa na wanafunzi wa shule za upili katika kujibu maswali ya ufahamu na ufupisho (102/2), aligundua kuwa wanafunzi wengi hawazingatii maudhui, dhamira, lugha na istilahi mbalimbali zilizotumiwa katika ufahamu na ufupisho. Utafiti huo ni tofauti kwa kuwa umeshughulikia ufahamu na ufupisho (102/2) ilhali sisi tulishughulikia uandishi wa insha (102/1). Hata hivyo, tulifaidika kutokana na utafiti huo katika lugha na istilahi zilizotumiwa na wanafunzi katika uandishi wa matini.

Akijishughulisha na makosa yanayofanywa na Taasisi ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika uteuzi wa vitabu vya kufundishia, Michira (2009) aligundua kuwa mchakato wowote wa kuteua vitabu vichache kutoka jumla wa vitabu hivyo hauna budi kudhihirisha kiwango fulani cha upendeleo. Hali hii hukumbwa na changamoto si haba, kama vile ukiritimba, hali ambayo waandishi wachache wanatalamaki silabasi ya Kiswahili. Baadhi ya vitabu vilivyoidhinishwa vimeandikwa na wafanyakazi wa taasisi ambao ndio wanaofanya ukaguzi na uidhinishaji. Maoni ya mtaalamu huyu yalitusaidia katika utafiti wetu ili kutathmini kama hali hii huchangia baadhi ya makosa ya kisemantiki yaliyogunduliwa katika matini za wanafunzi wa shule za upili. Tofauti ni kwamba Michira (mtaje), amejishughulisha na makosa yanayofanywa na wafanyakazi katika Taasisi ya Elimu nchini Kenya ilhali utafiti wetu uliwalhusu wanafunzi wa shule za upili.

Asiba (1985) akishughulikia lugha ya Sheng' katika mawasiliano andishi, anasema kuwa makosa mengi huletwa na waandishi wa vitabu ambao hutumia sheng' katika uandishi wao. Mengi ya makosa hutokana na athari za lugha za kiasili za Kiafrika. Anachukulia Sheng' kama chanzo cha kuzorota kwa Kiswahili sanifu nchini Kenya. Utafiti wa mtaalamu huyu ni muhimu kwa kuwa umetuelekeza kuwa Sheng' huchangia makosa katika lugha ya Kiswahili. Kazi hii inatofautiana na utafiti wetu kwa kuwa mtafiti huyu alichunguza athari ya Sheng' katika lugha ya Kiswahili ilhali utafiti wetu ulichanganua vyanzo zaidi vya makosa katika Kiswahili hasa katika utanzu wa semantiki.

Utafiti uliofanywa na K.I.E (2000) ulibainisha kuwa wanafunzi wengi wa shule za msingi na za sekondari wanakabiliwa na matatizo ya kimatamshi, uteuzi wa msamiati, sarufi na

kuingiliana kwa lugha. Hali hii inaathiri mawasiliano, baadhi ya wazungumzaji wanaeleweka kwa shida ilhali wengine hawaeleweki kabisa. Utafiti huu ulitusaidia katika utafiti wetu kwa kugundua kuwa baadhi ya wanafunzi waliathirika hadi kiwango cha kushindwa kuwasilisha walichodhamiria katika insha zao na kusababisha makosa ya kisemantiki kwa kuwa mawasiliano yalitatzika. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na utafiti wetu kwa kuwa wakati sisi tulijikita katika makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili, hususani kidato cha tatu. K.I.E (2000), waliangazia matatizo ya kimatamshi, uteuzi wa msamiati, sarufi na kuingiliana kwa lugha katika viwango vyote vyaya elimu (shule za msingi hadi sekondari).

SURA YA TATU

UCHANGANUZI WA MAKOSA

3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumechananua makosa mbalimbali ya kisemantiki yaliyojitokeza katika data yetu. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa, Corder (1974) aliainisha vipengele muhimu vya kuzingatiwa katika uchanganuzi makosa. Vipengele hivyo ni pamoja na: utambuaji wa makosa yenewe, uainishaji wa makosa mbalimbali na kuonyesha idadi ya kila kundi la makosa yaliyoainishwa. Hivyo basi, baada ya data zilizopatikana kutoka kwa watafitiwa mia moja ishirini (120), ambao ni wanafunzi wa shule za upili, kaunti ya Kakamega, kuhakikiwa na kupitiwa kwa uangalifu, matokeo yake yalipangwa kadiri ya mgawanyo wa makundi.

Pia, katika sura hii tumejadili vyanzo vya makosa ya kisemantiki yaliyojitokeza katika matini za watafitiwa. Asemavyo Sridhar (1981), ni muhimu kuchanganua vyanzo vya makosa mbalimbali kama vile athari ya lugha ya kwanza, ukosefu wa utaratibu wa kuendeleza maneno ya lugha ya Kiswahili na kadhalika.

3.2 Makosa ya Kisemantiki

Makosa mbalimbali ya kisemantiki yaliyotambuliwa, yaliainishwa katika makundi mbalimbali na baadaye yakasahihishwa. Tulizingatia umaratokezi wa kila kosa katika kupimia asilimia ya makosa. Mtafiti aliyaweka makosa hayo pamoja kwa watafitiwa wote walioshirikishwa katika utafiti na kupiga mara mia moja. Kisha makosa hayo yaliwekwa katika jedwali ili kurahisisha usomaji wa maudhui yatokanayo na uchanganuzi wa data husika. Aghalabu uchanganuzi wa data husika umehusishwa na lengo kuu la utafiti wa mada hii. Baada ya kuyapanga kwenye jedwali, tulienendelea na hatua ambayo ni ya uchanganuzi wa makosa yenewe ili kuona ukweli unaotawala katika data hizo ambazo hatimaye, ndizo zilizotupatia msimamo wetu kuhusu mada ya utafiti huu. Makosa mia saba arobaini na saba (747) ya kisemantiki yalitambuliwa katika utafiti huu. Makosa hayo yalipochanganuliwa, tuliyarekebisha ili kuondoa kasoro ambazo zilifanywa na watafitiwa. Kwa mantiki hiyo, jedwali lifuatalo ndilo linaloonyesha muhtasari wa makosa ya kisemantiki yaliyotambuliwa katika data yetu.

Jedwali 3: Umaratokezi wa Makosa ya Kisemantiki

	AINA	IDADI	ASILIMIA
1	Matumizi ya sheng	89	11.9
2	Mrundiko wa maneno katika sentensi	69	9.2
3	Ufafanuzi uliokithiri	75	10.0
4	Kutumia sauti isiyofaa katika neno	91	12.2
5	Matumizi ya lugha ya kishairi	59	7.9
6	Kuacha neno katika sentensi	66	8.8
7	Kutenganisha neno visivyo	67	8.8
8	Matumizi ya msamiati usiofaa katika muktadha	110	14.7
9	Kuacha sauti katika neno	58	7.8
10	Kubadilisha mpangilio wa fonimu katika neno	17	2.3
11	Kuunganisha maneno visivyo	46	6.2
JUMLA		747	100

Asili: Utafiti wa nyanjani 2016

Jedwali hili ni ushahidi kuwa watafitiwa wengi walikuwa na shida katika matumizi ya msamiati usiofaa katika muktadha. Hili tapo lilikuwa na jumla ya makosa **110** ya kisemantiki ambayo ni asilimia **14.7** ya jumla ya makosa yote yaliyobainishwa katika matini za watafitiwa walioshirikishwa katika utafiti huu. Hii ndiyo idadi kubwa zaidi ya makosa yote ya kisemantiki yaliyobainishwa. Kubadilisha mpangilio wa fonimu katika neno ndio ulikuwa na idadi ndogo sana ya makosa katika utafiti huu. Makosa katika tapo hili yalikuwa **17** ambayo ni asilimia **2.3** ya makosa yote yaliyobainishwa. Kwa mantiki hiyo, tutachanganua kila kosa kulingana na vile yameorodheshwa katika jedwali hilo hapo juu.

3.2.1 Matumizi ya Sheng

Mbaabu (1996) anaeleza kuwa kuchipuka kwa lugha msimbo ya sheng kulikuwa kama suluhisho la hali ya wingi-lugha katika mji wa Nairobi. Kulitokana na hali ya ukosefu wa uwiano na utaifa katika jamii na sera ya lugha inayowafanya Wakenya kuzungumza lugha

kwa mpangilio wa Kitriglosia ambako kuna lugha ya Kiingereza, Kiswahili na lugha ya mama. Hivyo, uchipukaji wa Sheng ultokana na haja ya kijamii baada ya ukosefu wa mfumo thabiti wa sera ya lugha nchini Kenya. Hata hivyo, Iraki (2004) ana maoni tofauti na haya anaposema kuwa mbali na kuwepo kwa mfumo wa Kitriglosia wa matumizi ya lugha nchini Kenya na ambao unasisitiza zaidi matumizi ya Kiingereza, Kiswahili na lugha za mama, bado Sheng ingechipuka. Hii ni kwa sababu vijana mjini Nairobi baada ya kukabiliana na mazingira ya wingi-lugha na kuwa hawakuwa na umilisi kamili wa lugha yoyote katika mazingira hayo, basi hawakuwa na budi kutumia ubunifu wao wa kiisumu kuiundi lugha yao wenyewe.

Pia kuna kubuniwa kinasibu kwa maneno ya Sheng. Shida huwa katika jamii-lugha yenye uwili lugha na wingi-lugha kwa kuwa huathiri wanafunzi katika uundaji wa vitenzi, nomino na hata sentensi nzima. Hata hivyo ni vigumu kutoa asilimia sahihi ya maneno ya lugha mbalimbali yaliyotumika kuunda msamiati wa lugha msimbo ya sheng. Iraki (2004), akitumia kamusi ya Sheng-Kiingereza yenye karibu vidahizo 800, anasema kuwa huenda asilimia 20 ya maneno ya Sheng yamekopwa kutoka lugha ya Kiswahili, asilimia 13 kutoka kwa lugha ya Kiingereza huko asilimia 67 kutoka lugha nyingine mbalimbali zinazozungumzwa jijini Nairobi na vitongoji vyake.

Kwa mujibu wa Patricial (1990), katika maneno **128** ya sheng aliyyofanyia uchunguzi, **90** yalitokana na Kiingereza; **25** yalitokana na Kijaluo na neno **moja** tu lilitokana na kiwango cha msamiati tu. Sarufi ya Sheng kwa hakika, ni muundo wa Kiswahili. Viambishi vya ngeli za nomino, nyakati na mnyambuliko, vyote ni vya Kiswahili. Uundaji wa maneno katika msimbo wa Sheng hufuata sarufi ya lugha za kibantu hasa Kiswahili. Kwa mfano, **alidhanywa**, kitenzi hiki kina ‘a’ ambayo ni kiima (nafsi), ‘-li-’ kiambishi cha wakati (uliopita), ‘-dhany-’ ni mzizi wa kitenzi ‘-w-’ ni mnyambuliko katika kauli ya kutendwa na ‘-a’ ni kiishio. Hivyo basi, muundo wa Sheng unazingatia muundo wa Kiswahili sanifu ambao ni KI+KI au KII + KI na kadhalika. Kundi hili lina makosa **89** ambayo ni asilimia **11.9** ya jumla ya makosa yaliyotambuliwa. Mifano ifuatayo inaonyesha kuwa watafitiwa waliazima ruwaza kutoka kwa msimbo wa Sheng na kuutumia katika lugha ya Kiswahili katika matini zao na kutatiza mawasiliano. Kwa mfano:

- 1)* *Mtoto alifurwa na chungu.*
- 3)* *Sukari imesanywa na mbochi na...*
- 4)* *Papa alipatikana rife na budaa alipokuwa...*
- 5)* *Alibroki chungu cha shoshi jana.*
- 6)* *Chungu alidemwa na kinyonga.*
- 7)* *Niligotea wasee waliokuwa wa..*
- 8)* *Bro alileta vege kutoka...*
- 9)* *Depa alimchapa Otish na kupelekwa hos na...*
- 10)* *Nilisaka baba tao tangu...*
- 11)* *Baba alijenga hao ya...*

Mifano iliyo hapo juu inadhihirisha kuwa Sheng si lugha bali ni mchanganyiko wa msamiati unaotumiwa pamoja na sarufi ya Kiswahili. Hii ndiyo sababu Sheng huathiri Kiswahili zaidi kuliko vile inavyoathiri Kiingereza ambacho kinaonekana kuchangia baadhi ya msamiati. Katika mfano (1-7) Sheng hufuata sarufi ya Kibantu na hasa Kiswahili kama vile **alifurwa, imesanywa, alidemwa, alibroki na niligotea**. Neno **alifurwa** ambalo lilitumiwa badala ya **aliumwa** limechukua muundo wa Kiswahili sanifu. Viambishi mbalimbali viliambishwa kama vile, ‘a’ kimetumiwa kama kiambishi cha nafsi (kiima), ‘-li-’ ni kiambishi cha wakati (uliopita), ‘-fur-’ ni mzizi wa kitenzi ilhali ‘-w-’ ni mnyambuliko na ‘-a’ ni kiishio. Mwanafunzi alipotumia maneno hayo katika sentensi alivuruga maana iliyonuiwa kwa sababu si wasomi wengi walio na umilisi wa msamiati wa Sheng. Kwa kawaida Sheng haidumu kwa muda mrefu kwa kuwa hubadilikabadilika kutegemea mazingira kila kuchao.

Kimuundo, kama wasemavyo Abdulaziz na Osinde (1997) Sheng ina mfumo wa sintaksia ya Kiswahili hata ingawa imekopa vipengele vingine vyta kiisimu kama vile Fonolojia, Mofonolojia na hata Leksia kutoka kwa lugha mbalimbali zinazopatikana jijini Nairobi kama vile Kiingereza, Kiswahili na baadhi ya lugha za mama. Hii huenda ndiyo sababu ya Iraki (2004) kudai kuwa Sheng ni lugha msimbo ambayo imeundwa kwa kukopa maneno kutoka lugha ya Kiswahili, Kiingereza, lugha za mama Kifaransa kati ya lugha nyingine nyingi ambazo maneno yameunganishwa pamoja kwa kufuata sheria za kisintaksia za lugha ya Kiswahili. Pia, kuna njia nyingine ambayo majina halisi ya mahali au watu

huongezewa viambishi ‘-sh’ au ‘-s’, katika mfano wa (9) **Otish** na **hos** yametumiwa badala ya **Otieno na hospitali** mtawalia. Maneno **vege, hao, tao rife** na **bro** katika (8, 10 na 11) yalikopwa kutoka lugha ya Kiingereza na kufupishwa ili kuunda maneno mafupi. Maneno haya hutokea kama dokezo la neno kamili. Kuna njia nyingine ya kubuni maneno kinasibu. Hii ni hali ya kuzipanga fonimu za lugha kulingana na utaratibu wa ujenzi wa lugha iliyohusika ili kuunda neno ambalo halipo katika lugha. Kwa njia hii maneno mapya ya lugha huundwa kwa kuzingatia kanuni za isimu za lugha husika kisha zikapatikana dhana mbalimbali. Mifanyiko hii yaweza kuwa maingiliano ya sauti moja na nyingine au sauti tofauti kuunganishwa na kuunda neno jingine. Sauti hubadilika kutegemea mazingira ya kifonolojia zinamotokea. Mwanafunzi anapotumia maneno yaliyopitia michakato hii ya uundaji katika sentensi, msomaji huweza kupata ujumbe uliokusudiwa au usiokusudiwa. Marekebisho mwafaka ni kama ifuatavyo:

1. Mtoto aliumwa na chungu.
2. Kifaranga amekufa wakati...
3. Sukari imekusanywa na yaya na
4. Papa alipatikana mtoni na baba wakati...
5. Alivunja chungu cha nyanya jana...
6. Chungu aliliwa na kinyonga
7. Niliwasalimia vijana waliokuwa...
8. Ndugu yangu aliletu mboga kutoka...
9. Naibu wa mwalimu Mkuu alipomchapa Otieno na kumpeleka hospitali.
10. Nilimtafuta baba mjini tangu...
11. Baba alijenga nyumba nzuri.

3.2.2 Mrundiko wa Maneno katika Sentensi

Kwa mujibu wa Njogu, Mwikali na Aswani (2006) sentensi kwa kawaida husimamia mwambatano sarifu wa mafungu ya maneno, wenyewe maana inayokubalika na wazo lililokamilika. Usarifu na ukubalifu hutegemea sheria za lugha sanifu. Sheria hizo ndizo zinazoeleza kanuni ambazo humwongoza msemajili ili aweze kuwasiliana na wasemajili wengine wasiomiliki lugha husika. Kwa mujibu wa Chomsky (1957), Nadharia ya Sarufi Zalishi, inajieleza kinaganaga na kwa uwazi kuitia sheria, hivi kwamba msomaji wa

sarufi hapaswi kutumia makisio yoyote kujaribu kubuni yaliyoelezwa. Kwa mfano maagizo yanayosema kuwa:

$$S \longrightarrow KN + KT$$

Sentensi ya Kiswahili huwa na sehemu mbili kuu. Sehemu hizi ni Kirai Nomino na Kirai kitenzi. Kirai Nomino ni sehemu ya sentensi inayotokea upande wa kushoto wa sentensi, nayo hubeba nomino au kiwakilishi chake ambacho ni kiima. Kirai kitenzi hutokea upande wa kulia wa sentensi, nayo hubeba kitenzi ambacho ni kiarifu. Kisha hufuatwa na kitendwa au kitendewa ambacho ni shamirisho (SH) katika sentensi. Kwa hivyo, vipashio vya sentensi huwa na mfuatano kulingana na majukumu katika nafasi vitakavyochukua katika sentensi.

Sentensi ndiyo tungo ya juu kuliko kishazi na ambayo huweza kujengwa na kishazi huru kimoja au kishazi huru kimoja na kishazi tegemezi kimoja. Sentensi huwa kipashio huru kimuundo na kikubwa zaidi kati ya vipashio vya kiisimu ambavyo hutumiwa kisarufi. Luga zote za ulimwengu zina utaratibu maalumu katika upangaji wa maneno ili kuunda sentensi zenye maana. Kando na kuonyesha namna ambavyo maneno ya ainaaina hufuatana katika kuunda santensi, lazima uhusiano uliopo kati na baina ya viambajengo vya sentensi udhihirike wazi.

Luga ya Kiswahili ikiwa mojawapo ya lugha za ulimwengu ina utaratibu wake ambao unastahili kuzingatiwa ili kuunda sentensi iliyokamilika kimaana. Kwa mfano, mojawapo ya sheria za kiisimu ni kuwa, kivumishi hufuata nomino, kitenzi huja kabla ya chagizo na kadhalika. Iwapo utaratibu huu hautazingatiwa katika utungaji wa sentensi, msomaji atatatizika kung'amua maana iliyodhamiriwa. Katika utafiti huu, watafitiwa wengi hawakizingatia utaratibu wa kuunda sentensi zilizosheheni maana. Baadhi yao walirundika maneno katika utungaji wa sentensi na matokeo yake ni sentensi ambazo hazikueleweka kwa urahisi. Makosa yaliyotambuliwa ni **69** ambayo ni asilimia **9.2** ya makosa yote. Zifuatazo ni baadhi ya sentensi zenye makosa hayo:

12)* *Yule mtoto ameenda kumnunulia baba yake maziwa sokoni na miguu yake.*

13)* *Juma aliuza zabuni zile kwa sabuni zake ili asipate hasara juu yake.*

- 14)* *Mbali na hayo pia magazeti huwafanya wanafunzi kujua mzuri na kuelewa...*
- 15)* *Baba wangu ziwani alivua papa mkubwa alipoenda.*
- 16)* *Husaidia wanafunzi kwa kuboresha vizuri lugha vile anaposoma gazeti.*
- 17)* *Papa amevuliwa baharini na mvuvi mzee yule papo...*
- 18)* *Sukari ilimwagika yote sakafuni na mtoto wa*
- 19)* *Baba kazini ameenda na matiri ya...*

Mifano hiyo hapo juu inaonyesha sentensi ambazo henzieleweki moja kwa moja. Katika mfano wa (12), mwanafunzi alikosea alipotumia kivumishi **yule** kabla ya nomino **mtoto** inayovumishwa. Matumizi ya kiunganishi **na** huonyesha kuwa miguu ni baadhi ya vitu ambavyo vilihitajika kununuliwa na wala si kitumizi. Mrundiko huu wa maneno katika uandishi wa matini kwa kiwango kikubwa unatatiza uelewekaji wa ujumbe kwa urahisi. Katika (13), mwanafunzi alichanganyikiwa na vitate **sabuni** na **zabuni**. Alitarajiwa kutufahamisha ni nini mhusika anauza kwanza ili aendelee kutueleza namna alivyouza. Hata hivyo, sentensi nzima imevurugika kwa kurundika maneno pasi kufuata utaratibu mwafaka.

Matumizi ya viunganishi viwili mwanzoni mwa sentensi pamoja na maneno **kujua mzuri na kuelewa** katika (14), yamerundikwa na kuifanya sentensi husika kutoleweka vyema. Mfano uliopo katika (15), mwanafunzi alikosea kwa kuweka chagizo **ziwani** baada ya kivumishi na kitenzi kisaidizi **alipoenda** mwishoni mwa sentensi na wakati unapoisoma unatatizika kwa kuwa ujumbe haueleweki moja kwa moja. Kosa sawa na hilo lilitokea katika (16), pale ambapo mwanafunzi alianza sentensi kwa kitenzi kisaidizi **husaidia** kikifuatwa na nomino **mwanafunzi** na hatimaye kumalizia kwa nomino **gazeti** visivyo. Kitinzi kisaidizi hufuatwa na kitinzi kikuu au kitinzi halisi wakati wote katika utungaji wa sentensi ya Kiswahili. Mrundiko huo wa maneno hupelekea kuwepo kwa kosa la kisemantki kwa kuwa ujumbe haueleweki. Kutojua sheria au kaida za lugha anayejifunza, mwanafunzi hutumia sheria bila kujua jinsi zinavyopaswa kutumiwa. Aghalabu mwanafunzi huwa amefunzwa kanuni za lugha anayojifunza lakini kwa kuwa hajazimudu vyema, yeye huzitumia hapa na pale bila kuwa na uelewa wa kuzitumia.

Katika (17-18), nomino tendewa imetangulia katika sentensi badala ya nomino tendi na kuvuruga mpangilio wa sentensi. Kwa mfano katika (18), haieleweki kama ni mtoto alimwaga sukari au wote walimwagika kwa pamoja. Vilevile kivumishi **yote** kimetumiwa katika nafasi isiyostahili na kuitatiza sentensi zaidi. Hatimaye, katika mfano (19), matumizi ya chagizo **kazini** na maneno **na** na **matiri** yamevuruga ujumbe zaidi. Mwanafunzi alitumia **na** badala ya **kwa** na **matiri** badala ya **matatu** kwa sababu ameathiriwa na lugha ya kwanza pamoja na msimbo wa Sheng.

Makosa hayo yote hapo juu hutokea wakati mwanafunzi hajui kazi ya viambajengo (nomino, kiwakilishi, kivumishi, kitenzi, kielezi, kiunganishi, kihuishi na kihisishi) katika sentensi. Hajui mahali mwafaka pa kutumia kiambajengo husika katika sentensi. Huu udhaifu wa mwanafunzi kushindwa kubainisha nafasi na matumizi mwafaka ya viambajengo vya sentensi hahihuishi na lugha ya kwanza ya mwanafunzi bali lugha ya pili (Kiswahili). Mpangilio mwafaka wa sentensi hizo hapo juu ni kama ifuatavyo:

12. Mtoto yule ameenda sokoni kwa miguu kumnunulia baba yake maziwa.
13. Juma aliuza sabuni zake kwa zabuni ili asipate hasara...
14. Zaidi ya hayo, magazeti huwasaidia wanafunzi kuelewa na kujuu..
15. Baba yangu alimvua papa mkubwa baharini..
16. Wanafunzi wanaposoma magazeti huboresha lugha...
17. Mvusi yule mzee amemvua papa...
18. Mtoto alimwaga sukari yote sakafuni..
29. Baba ameenda kazini kwa matatu.

3.2.3 Ufafanuzi Uliokithiri

Huu ni utumiaji wa maneno ya kuzungusha au maneno mengi yanayovuruga maana. Kama anavyoeleza Crowley (1982), kuna misukumo kadhaa ambayo inamfanya mwanafunzi kuhamisha maana ya neno kutoka lugha asili hadi lugha ya pili. Mwanafunzi huhamisha maana ya neno kutoka lugha ya kwanza hadi lugha anayojifunza kwa sababu ya hali inayojulikana kama upanuzi wa maana. Naye Lott (1983), ana mawazo yanayokaribiana na ya Crowley anaposema, kuna mifumo mingine ya lugha inayowatatiza wanaojifunza lugha. Lugha huwa tofauti na lugha nyingine, mwanafunzi anapojifunza lugha iliyo tofauti

na lugha yake ya kwanza hupata shida sana. Mwanafunzi husika tayari amejifunza mifumo ya lugha ya kwanza kwa hivyo itakuwa vigumu kwake kuanza kujifunza mifumo iliyo tofauti na lugha yake ya kwanza. Tayari akilini mwake amemudu mifumo ya lugha ya kwanza anayoitumia kila siku katika mawasiliano. Kwa kufanya hivyo ujumbe usiotarajiwa humfikia msomaji. Iwapo mwanafunzi atabanwa na msamiati wa neno katika lugha ya pili, hupanua msamiati wa neno alilo nalo ili kukabiliana na hali inayomkanganya Katika tapo hili kulikuwa na makosa **75** ambayo ni asilimia **10** ya jumla ya makosa yote yaliyotambuliwa katika utafiti huu. Tapo hili lilikuwa na mifano ifuatayo:

- 20)* *Walevi wanaonywa na kutumia kwa wingi mapombe, sigara, marijuana, kube... ili kuwa na maisha yasiyokuwa na malaria kwa maisha..*
- 21)* *Chungu ndio walichangia woga aliokuwa nao mingi mtoto yule wa mzee anayekaa karibu na si...*
- 22)* *Lugha inayoandikwa na magazeti haya ni lugha ya Kiswahili sanifu na pia kuna matumizi mwingi ya lugha ya methali, misemo, vitendawili...*
- 23)* *Wanafunzi badala ya kukaa ovyo ovyo barabarani wakichungulia watu bila ya kuwa na chochote cha kutenda ni vizuri wajihusishe na kusoma magazeti...*
- 24)* *Kiswahili imefanywa vigumu katika uzungumzi wake na lugha inayotumika sana na vijana wa shu...*
- 25)* *Magazeti kuna vitu vingi ambavyo inaweza kuwaleta mabaya wanafunzi na kuharibu miili yao...*

Katika mifano iliyo hapo juu, mwanafunzi hufanya makosa hayo kwa kukosa msamiati bora wa kujieleza. Hivyo basi, mwanafunzi hujaribu kufafanua kwa kutumia maneno mengi ili kuwasilisha ujumbe aliодhamiria katika muktadha na hatimaye husababisha makosa mengi yakiwemo ya kisemantiki. Baadhi ya maneno yaliyotumiwa hayana maana yoyote ila tu kuvuruga maana iliyokusudiwa. Mathalani katika (20) mwanafunzi hajui neno **mihadarati** na hivyo anajieleza kwa maneno mengi kama, **mapombe, sigara, marijuana**, na kadhalika. Pia alifanya kosa kwa kuongeza kiambishi ‘ma’ kwa neno pombe kuashiria wingi. Kisarufi, kiambishi ‘ma’ hakina maana yoyote katika nomino ‘**pombe**’ ila tu kilifanya neno husika kuwa na kasoro.

Kwa mujibu wa Mdee (1988), kiambishi kinaweza kuambishwa kabla na baada ya mzizi wa neno na hivyo kupelekea kuundwa kwa maneno mapya. Sharti ikumbukwe kuwa si maneno yote yanayoambishwa katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, nomino za pekee haziambishwi kwa sababu zinawasilisha maana kamilifu zinapotumiwa katika maandishi. Katika mfano wa **(21-25)**, makosa ni yale yale yanayotokana na ufanuzi uliokithiri. Mwanafunzi alijaribu kujieleza kwa lugha ya Kiswahili kutokana na mawazo ya lugha ya kwanza. Hii ina maana kuwa mwanafunzi alijikita katika kutafsiri ujumbe wake kutoka lugha yake ya kwanza hadi lugha ya Kiswahili. Sentensi hizo zinaweza kurekebishwa kwa kutumia msamati unaofaa kama ifuatavyo:

20. Walevi walionywa dhidi ya utumiaji wa mihadarati ili kuwa na siha njema...
21. Chungu walimwogfya mtoto wa jirani..
22. Lugha magazetini huwa na ukwasi mkubwa wa tamathali za usemi..
23. Badala ya vijana kuzembea, wajihushe na usomaji wa magazeti...
24. Sheng' imeathiri lugha ya Kiswahili...
25. Magazetini mna mambo mengi yanayoweza kuwadhuru...

3.2.4 Kutumia Sauti Isiyofaa katika Neno

Matamshi ya maneno ya lugha yoyote ile ni mfumo wa sauti. Hali ya kutumia sauti moja mahali palistahili sauti nyingine tofauti, ilichangia kuwepo kwa kasoro katika baadhi ya maneno yaliyotumiwa na baadhi ya watafitiwa. Mawasiliano bora yatakuwepo iwapo sauti itatumika ipasavyo. Mwanafunzi hufanya kosa hili kwa kutumia sauti moja mahali ambapo palihitajika sauti nyingine tofauti. Hali hii ilichangia kuwepo kwa makosa ya kisemantiki kwa baadhi ya matini za watafitiwa. Kundi hili lilikuwa na makosa **91** yaliyotambuliwa ambayo ni sawa na **10.9**. Mifano ifuatayo inadhihirisha makosa husika:

- 26)**Baba alipokea mahali ya dada...*

- 27)* *Mama alimpikia baba simu wakati...*
- 28)* *Nilipoenda sokoni nilinunua baba ya...*
- 39)* *Sheng' huadhiri Kiswahili...*
- 30)* *Baba alianguka jini alipokuwa...*
- 31)* *Ufunguza uchungu kwa..*
- 32)* *Yeye ana yutahi...*

Makosa katika **26** hadi **32** huashiria namna ambavyo wanafunzi walivyochangua sauti isiyofaa na kuitumia mahali pasipofaa. Hali hii ilipelekea kuwepo kwa kosa kwa sababu maana iliyokusudiwa haikumfikia aliyedhamiriwa. Makosa mengi yalisababishwa na athari ya lugha ya kwanza ya mwanafunzi. Jamii-lugha nyingi hazina baadhi ya sauti zilizobadilishwa hapo juu katika lugha zao za kwanza. Halliday (1964), anaelezea kuwa ujifunzaji wa lugha ya pili kwa kawaida hufanyika baada ya ujifunzaji wa lugha ya kwanza kukamilika. Katika kiwango hiki ajifunzanye lugha huwa tayari amejenga umilisi wa kutosha wa kimawasiliano katika lugha yake ya kwanza. Uwezo au umilisi na utendaji ndizo dhana za kimsingi katika utumiaji wa lugha (Nadharia ya Sarufi Zalishi). Nadharia hii hufafanua ujuzi wa mzungumzaji asilia wa lugha wa kuweza kumudu lugha yake, ujuzi huu haupatikani kutokana na kujifundisha lugha darasani. Ujuzi huu unahu utumiaji lugha husika, kuielewa na kuweza kutoa na kuzua tungo, sentensi na maneno mengi ya lugha asilia. Kupitia kwa uwezo, mzungumzaji asilia wa lugha anaweza kudondoa sentensi ambazo ni sahihi na ambazo si sahihi. Kutokana na hali hii, lugha ya kwanza inaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa lugha ya pili. Wasemavyo Buliba, Nyonje na Mwihiika (2006), nchini Kenya kuna imani kuwa makundi yafuatayo yanaweza kutambulishwa na kutofautishwa kwa sauti zifuatazo:

Jedwali 4: Jamii-lugha

KUNDI	SAUTI
Wajaluo	/ s, sh /
Wakikuyu	/ r, l /
Waluhya	/ b, p, r,l, g, k /

	/ h, mb, nd /
Wakamba	
	/ z, s, ch, j, k, g /
Wakalenjin	
	/ s, sh, g, gh, s, z, b, p, ch, j ,l ,r/
Wakisii	

Asili: Buliba, Nyonje na Mwihiika (2006)

Mifano iliyopo katika (26-30) inaonyesha matumizi mabaya ya /l/ nafasi ya /r/, /k/ nafasi ya /g/, /b/nafasi ya /p/, /dh/ nafasi ya /th/, /j/ nafasi ya /ch/ na /f/ nafasi ya /p/ na kuwa na neno tofauti na lile lililohitajika katika muktadha huo. Hali hii husababishwa na ukaakaishaji wa fonimu. Lass (1984), anadai kuwa mfanyiko huu sauti hubadilisha mahali na jinsi ya kutamkwa kwake, aghalabu kwa kuhamishwa kwenye kaakaa gumu. Lugha mbalimbali huwa na ukaakaishaji wa sauti mbalimbali. Katika Kiswahili sauti za kaakaa gumu ni tatu. Nazo ni /j/, /ŋ/ na /tʃ/. Kwa hivyo, katika Kiswahili ukaakaishaji hutokea pale sauti isiyo ya kaakaa gumu hubadilika na kuwa mojawapo ya sauti ya kaakaa gumu. Mfanyiko huu hupitia hatua mbalimbali. Kwanza, /i/ huyeyushwa na kuwa nusu irabu /j/, kisha nusu irabu hiyo hudondoshwa huku sauti ya kipasuo /k/ ikidhoofika na kuwa /tʃ/. Yaani:

/k/ → /tʃ/ - /i/

Ukaakaishaji katika lugha ya Kiswahili

/ki + akula/ → [kjakula] → [tʃjakula] → [tʃakula]

Kwa mfano, ingetarajiwa neno kutamkwa *“kiakula” kutokana na mofimu zinazounda neno hili “ki + akula”. Tofauti hii ya kimatamshi inasababishwa na msururu ufuata wa mabadiliko ya kifonolojia.

- i. Badiliko la kwanza linatokea katika [kiakula] ambapo /a/ inaathiri /i/ na kuifanya nusu vokali (uimarakaji)

/i/ → [j] – v (isiyo i)

Hivyo basi neno hili latarajiwa kutamkwa * [kjakula].

- ii. Hata hivyo /j/ ambayo ni nusu vokali ya mbele inaathiri /k/ kwa njia mbili. Kwanza “inavuta” mbele na kuifanya itamkwe katika kaakaa la mbele na wakati huo huo kuidhoofisha na kuifanya kuwa sauti ya kipasuo kwaruzo [tʃ]. Mabadiliko haya yote hufanyika kwa pamoja katika ubongo wa mse maji.

Ukaakaishaji pia hutokea katika vivumishi. Wasemavyo Habwe na Karanja (2004), ukaakaishaji katika vivumishi hutokea hasa katika mipaka ya mofu za vivumishi. Vivumishi ambavyo huhusika sana ni vile ambavyo mizizi yao huanzia na irabu. Kiambishi awali pekee ambacho husababisha ukaakaishaji katika Kiswahili ni kile kiambishi /ki/

Kiambishi /ki/ kinapowekwa pamoja na vivumishi ambayo mizizi yao inaanza na irabu ukaakaishaji hutokea. Baadhi ya vivumishi ambamo ukaakaishaji hutokea ni pamoja na:

Vivumishi vimilikishi

[-ako] → [ki +ako] → [kyako] → [chyako] → [chako]

Hapa tunaona kuwa kizuiwa hafifu /ki/ ambacho hutamkiwa kwenye kaakaa laini kinabadilika na kuwa kwamizwa /tʃ/ ambacho hutamkiwa kwenye kaakaa gumu

Ukaakaishaji hutokea katika nomino chache za Kiswahili. Mzizi lazima uwe na irabu. Kwa mfano:

Umbo la ndani *umbo la ndani* *umbo la nje*

Ki +ombo → kyombo — chyombo → chombo

Vilevile katika vitenzi ukaakaishaji hutokea hasa pale mofu /ki/ inapowekwa pamoja na mofu /o/ ya urejeshi.

/ki/ → /o/ ya urejeshi

[A] + [li] + [ki] + [o] + [ki] + [pat] + [a]

1 2 3 4 5 6 7

A + li + cho + ki + pat + a

1 2 3 4 5

Ambapo [ki] + [o] = cho

Hivyo basi mofu ya 3 (tatu) /ki/ na ya 4 (nne) /o/ zinaungana na wakati huo huo panatokea ukaakaishaji ambapo /k/ inakaakaishwa na kuwa /ch/. Hii ndio ilichangia mabadiliko yaliyopo hapo juu.

Kwa mfano katika (26) fonimu (l) ambayo ni kitambaza imechukua nafasi ya (r) ambayo ni kimadende. Licha ya kuwa fonimu hizi hutamkiwa katika ufizi, haziwezi kubadilishana nafasi. Katika neno ‘**mahali**’ ambalo lina maana ya eneo na limetumiwa kimakosa badala ya ‘**mahari**’ lililo na maana ya mali au fedha inayotolewa na mwanamume kupewa wazazi wa mwanamke anayetaka kumwoa ambalo lingefaa zaidi katika muktadha. Vilevile katika (27), maneno **alimpikia simu** badala ya **alimpigia simu**, yanaashiria matumizi mabaya ya fonimu /k/ na /g/. Licha ya kuwa sauti hizi mbili ni vipasuo vivilvyo na sifa bainifu zinazofanana zinatofautiana katika sifa ya mghuno, /k/ ni sauti isoghuna ilhali /g/ ni sauti ghuna. Pia katika (28) **baba** badala ya **papa** kuna kubadilishana kwa nafasi kati ya /p/ na /b/, sauti hizi zinapatikana katika kategoria la vipasuo. Tofauti iliyopo ni kuwa /p/ si ghuna bali /b/ ni ghuna. **Hadhiri** katika (29) limechukua nafasi ya **athiri** na kupelekeea kauli husika kuwa na kasoro. Fonimu/ð/ na /θ/ zinabadilishana nafasi kwa kuwa zote zina sifa mbili kuu za kifonetiki zinazofanana: ni vikwamizwa na zinapotamkwa ncha ya ulimu ugusa meno, tofauti ni kuwa /ð/ ni ghuna ilhali /θ/ si ghuna. Katika (30-31) neno **jini** limetumiwa badala ya **chini** na **ufunguza** badala ya **punguza**, huonyesha kuwa mwanafunzi alishindwa kubainisha tofauti kati ya sauti hizi zote. Maana za maneno yaliyotumiwa katika nafasi za maneno yaliyostahili yalipelekeea kuwepo kwa makosa ya kisemantiki. Hatimaye, mfano wa (32), sauti /v/ imetumiwa katika nafasi ya /f/, hizi ni sauti za kundi la vikwamizo na zinazotamkiwa midomoni na menoni. Fonimu /v/ ni ghuna ilhali /f/ si ghuna. Katika neno ‘**vutahi**’ badala ya ‘**futahi**’ ambalo lina maana ya ‘**bahati njema**’ ambalo lingefaa zaidi katika kauli hiyo. Hivyo basi, katika mifano iliyo hapo juu,

fonimu zingine zote zinafanana isipokuwa /l/ na r/, /k/ na /g/, /ð/ na /θ/, /tʃ/ na /ʃ/, /p/ na /f/, /v/ na /f/. Tofauti ya hizo sauti ndiyo imeleta tofauti ya maana. Makosa hayo yanaweza kusahihishwa kama ifuatavyo:

- 26 Baba alipokea mahari ya dada...
27. Mama alimpigia baba simu wakati...
28. Nilipoenda sokoni nilinunua papa ya...
29. Sheng huathiri Kiswahili
30. Baba alianguka chini alipokuwa...
31. Hupunguza uchungu kwa...
32. Kusoma gazeti ni...
33. Yeye ana futahi...

3.2.5 Matumizi ya Lugha ya kishairi


Lugha ya ushairi kwa kawaida ni tofauti na lugha inayotumiwa katika uandishi wa kawaida. Kwa mujibu wa Kivuva (1992), lugha hii huweza kufupishwa au kurefusha au kutofuata mpangilio wa maneno katika sentensi kwa minajili ya kupata idadi fulani ya mizani katika shairi husika. Hii hutegemea bahari ya shairi ambalo mtunzi anaazimia kulitunga, hivyo basi, mwanafunzi anapoitumia lugha ya kishairi maana iliyokusudiwa humtatiza msomaji. Tapo hili lilikuwa na makosa **59** ambayo ni asilimia **7.9** ya jumla ya makosa yaliyotambuliwa. Kauli zifuatazo zinaonyesha matumizi ya lugha ya kishairi:

- 34)* *Baba hendi katika kuvua leo...*
- 35)* *Niposoma magazeti silewe...*
- 36)* *Mama alikimbilia wakati baba alimchapa kwa usalama kwa*
- 37)* *Magazeti hutusaidia kujuwa...*
- 38)* *Palikuwa na storia kwetu wakati...*
- 39)* *Magazeti piya hutuwesha...*
- 41)* *Sikumwona lakini nilimtafutababa ...*

Katika mfano wa (34), mwanafunzi alitumia mbinu ya inkisari. Huu ni uhuru wa mtunzi wa mshairi wa kufupisha baadhi ya maneno ili kupata idadi fulani ya mizani katika shairi lake. Baadhi ya watafitiwa waliathiriwa na lugha hii na kuitumia katika uandishi wao wa

insha pasi kujuu athari yake. Badala ya mwanafunzi katika (34) kuandika ‘**haendi**’ analifupisha na kuandika ‘**hendi**’ na kuwa na mizani miwili badala ya mitatu. Hali hii pia inachukuliwa kama udondoshaji wa irabu. Kwa mujibu wa Schane (1973), mfanyiko huu unahusishwa sana na miundo mwafaka ya silabi. Katika baadhi ya lugha za kibantu mathalani lugha ya Kiswahili sanifu, hali hii ya udondoshaji wa irabu hutokea wakati ambapo irabu imetanguliwa na irabu nyingine au inapotanguliwa na konsonanti katika mofu ya kiambishi ngeli na kufuatwa na konsonanti nyingine. Mfanyiko huu aghalabu hutokea katika nomino za ngeli ya kwanza, ya pili na ya tatu katika viambishi vyatupatanishi wa vitenzi vyatuputanishi wa videnzi vyatuputanishi wa vivumishi katika ngeli mbalimbali. Irabu inadondoshwa ili kupata muundo KKI, kwa mfano: mutoto <mtoto> = KKIKI.

Mfano wa (35), kuna mvutano wa irabu, ambao ni mfanyiko unaohusu sauti mbili za irabu kuungana na kuleta sauti ya katikati. Aghalabu irabu moja huwa ya juu ilhali nyingine ni ya chini. Sauti ya juu huvutwa chini kidogo na ile ya chini kuinuka kidogo. Matokeo yake ni kwamba sauti itakayotokea si ya chini wala ya juu bali ni ya katikati. Sauti zile zinazovutwa huishia kutupiliwa mbali. Tazama jedwali la IPA la vokali za kimsingi:



Asili: Mgullu (1999) *kielelezo cha vokali za kimsingi*

Maneno mengi huonyesha mfanyiko huu katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano:

$$\{ma+ino\} = meno$$

$$\{ja + itu\} = \{jɛtu\}$$

Bakari (1982), anadai kuwa hii ni kwa sababu ya kurahishisha matamshi. Katika mfano wa (35) kwa neno ‘selewi’ inavutwa au inashushwa na kuwa /ɛ/ {si + elewi} = {slewi} ambayo ni ya katikati.

Hivyo basi, katika mfanyiko huu irabu /i/ ya (+juu) huvutwa chini na kuwa (-juu) /ɛ/ na irabu ya chini na (+ nyuma) huvutwa na kuwa (-nyuma) /ɛ/. Sauti hizo zinazovutana hudondoshwa na badala yake sauti /ɛ/ hutokea.

Sheria yake ni:

/a/ \longleftrightarrow /i/ \longrightarrow /ɛ/

Na katika (36), neno ‘alikimbililia’ lina kasoro kutokana na kurudiwa kwa kiambishi (‘li’). Mwanafunzi alitumia mbinu ya mazda ambapo neno husika hurefushwa kwa kuongezewa viambishi ili kupata idadi fulani ya mizani. Vilevile katika (37 na 40), mbinu ya tabdila imetumiwa kwa maneno **piya** na **kujuwa** mtawalia. Hapa mpangilio wa vitamkwa au sauti katika neno hubadilishwa kwa minajili ya urari wa vina. Schane (1972), anadai kuwa uchopekaji wa sauti husimamia kaida ya kuingiza sauti katika umbo asilia. Mageuko haya yanatumika namna mbalimbali katika mfululizo wa matamshi na uundaji wa maneno, hasa kimitindo, uambishaji wa maneno na utohozi mikopo. Mitindo ya matamshi ya maneno inatumika kwa hiari ya msemaji wa lugha bila kubatiliza misingi ya sarufi.

[ɔa] \longrightarrow [ɔwa]

[pia] \longrightarrow [piya]

[lea] \longrightarrow [leja]

Mageuzi haya yanachopeka kikadirio (KA) [w], [y] au [j] katika mazingira ya vokali ya chini, ya nyuma au ya mbele mtawalia. Tunaweza kuwakilisha sheria ya kijumla kwa kurejelea pahali pa kutamkia vokali.

\emptyset \longrightarrow K / V

[KA] [+PA]

Kimani, Mwiaki na Buliba (2006), wanaeleza kuwa mojawapo ya sababu za kuunda ‘nusu irabu’ ni kule kuleta muundo mwafaka wa silabi. Nusu irabu huundwa wakati ambapo sauti ya irabu /u/ huimarika na kuwa nusu irabu /w/ au wakati ambapo irabu /i/

huimarika na kuwa /j/. Sauti hizo za irabu huhitaji nguvu kidogo katika kutamka zikilinganishwa na irabu na hiyo ndiyo sababu ya kusema kuwa irabu hizo zimeimarika.

Katika mfano wa (39), mwanafunzi alitumia mbinu ya utohozi. Utohozi katika uundaji wa maneno ni utaratibu wa kuyabadili maumbo ya maneno yaliyokopwa kutoka lugha chanzi ili yalingane na kuoana na fonolojia ya lugha lengwa (Buliba, Njogu na Mwikali 2006; Kiango, 2004). Utohozi kutoka lugha za kigeni unasisitizwa na wanasayansi hasa kwa ajili ya kutunga istilahi za kimataifa ambazo kwa mujibu wa miiko ya sayansi lazima zihifadhiwe katika uasili wake kubadili tahajia yake wala fonimu zake. Utaratibu huu unahusisha mabadiliko mbalimbali ya kifonolojia. Kwa mfano, kunaweza kutokea uchopekaji wa irabu katika msamiati unaohusika ili kudhibiti muundo asili wa lugha. Muundo wa silabi unaopendelewa katika Kiswahili, ni wa silabi wazi. Kwa mfano, neno ‘bed’ linatoholewa na kuwa ‘kitanda’ ili kufungamana na muundo unaopendelewa. Kwa mfano neno ‘storia’ katika (39) lilitumiwa badala ya neno ‘hadithi’ ambalo lingeleta ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Mwanafunzi hakuzingatia utaratibu unaozingatiwa katika kutohoa maneno kutoka lugha zingine hadi lugha ya Kiswahili.

Kwa mfano:

Kiingereza	muundo wa silabi	Kiswahili	muundo wa silabi
Pass [pa:s]	KVK	Pasi	KVKV
Soup [su:p]	KVK	Supu	KVKV

Kila mazingira ya uchopekaji inahusu sauti ya konsonanti. Ø → v / k

Hatimaye, katika (41), mwanafunzi alivuruga ujumbe kwa kuboronga sarufi. Huu ni uhuru wa kukiuka kanuni za kisarufi za lugha kwa nia ya kutosheleza vina na mizani, kuchangia mkato wa lugha ya kishairi. Kwa mfano, miundo ya sentensi inapogezuwa na kusisitiza dhana kwa kuileta mwanzo ikiwa kwa kawaida ingekuja baadaye katika mshororo au kipande. Uhuru huu hujitokeza kwa:

1. Kukiuka mpangilio sanifu wa maneno katika sentensi. Kwa kuzingatia nadharia ya sarufi zalishi, sentensi za Kiswahili hufuata muundo wa kiima na kiarifu.

Ruwaza inayokubalika ni ya nomino au kiwakillishi chake kuja kabla ya kivumishi; na kitenzi hutangulia kielezi katika sentensi.

2. Kukwepa tahajia- kuendeleza maneno isivyostahili. Mazida, tabdila na inksari ni mifano ya ukwepaji wa aina hii. Kwa mfano, neno ‘kuja’ linaweza kuandikwa kitabdila likawa ‘kucha’ ili kupata kina ‘cha’. Maneno haya yana maana tofauti. Yatakapotumiwa katika mazingira mengine, maana iliyokusudiwa haitamfikia anayetarajiwa.

Mwanafunzi alikiuka sheria za kiisimu alipoandika ‘**sikumwona lakini nilimtafuta baba**’. Lugha hii hukubalika katika utunzi wa mashairi pekee na mtunzi hawezi kulaumiwa ama kukosolewa kuwa amevunja sheria za kisarufi. Mwanafunzi anapoitumia lugha ya aina hii katika uandishi wa insha hukwamiza mawasiliano na ujumbe hautamfikia mtarajiwa kwa sababu lugha ya kishairi haileweki na kila mtu kwa urahisi. Marekebisho yafuatayo yan gefaa kwa kauli zilizopo hapo juu:

35. Baba haendi kuvua leo.
66. Niliposoma magazeti sikuelewa (kufahamu)
37. Mama alikibilia usalama wakati baba alimchapa...
38. Magazeti hutusaidia kujua...
39. Palikuwa na hadithi kwetu wakati...
- 40 Magazeti pia hutuwezesha...
41. Nilimtafuta baba lakini sikumwona...

3.2.6 Kuacha Neno katika Sentensi

Lugha ya Kiswahili ina aina mbalimbali za maneno. Maneno haya yakiwa ni nomino, kitenzi, kivumishi, kiwakilishi, lielezi, kiunganishi, kihuishi na kihisishi. Maneno haya hutumiwa katika uundaji wa tungo za lugha ya Kiswahili. Uundaji wa tungo hizi huzingatia uhusiano wa neno kwa neno.

Kwa mujibu wa Cruse (1986), kimapokeo sentensi ilielezwa kama kipashio cha kujieleza kinachosheheni fikra kamili. Huwa ni kipashio huru kimuundo na kikubwa zaidi kati ya

vipashio vya kiisimu ambavyo hutumiwa kisarufi. Hivyo basi, maneno yaliyoko katika sentensi hufanya kazi za aina aina. Kwa mfano, yapo maneno yanayoonyesha mtenda tendo au mtendewa tendo na mtendwa, nayo huitwa nomino, nayale yanayotaja tendo huitwa kitenzi na kadhalika. Tatizo hutokea pale ambapo neno au maneno zaidi huachwa katika sentensi. Matokeo ni sentensi zisizosheheni fikra kamili. Katika utafiti wetu makosa **66** sawa na asilimia **8.8** yalitambuliwa katika insha tulizochanganua. Mifano ifuatayo inadhihirisha udhaifu huo:

- 42)* *Kutoka kwa tunapata mambo mapya na....*
- 43)* *Chungu cha kilipasuka wakati...*
- 44)* *Huwapa wanafunzi ya kazi*
- 45)* *Athari lugha sheng'...*
- 46)* *Ili kukuza kiwango Kiswahili...*
- 47)* *Magazeti huendeleza talanta tofauti mionganoni wanafunzi*
- 48)* *Magazeti hupasa ujumbe dharura juu...*
- 49)* *Hutupa msamiati Kiswahili au kimombo na...*

Kuachwa kwa neno ‘**magazeti**’ katika **(42)** hupelekeea kutolewaka kwa kauli hiyo. Maana iliyokusudiwa hutatizika kwa sababu haieleweki iwapo mambo mapya yalitoka wapi? Kwa mtandao, redio, runinga au magazetini. Hivyo basi, hali hii hutinga mawasiliano kwa kuwa ujumbe uliokusudiwa haukumfikia aliyedhamiriwa. Mfano katika **(43)**, nomino (neno linalotaja kitu, mtu au jambo), ‘**mboga**’ lililohitajika liliachwa na kutatiza mawasiliano. Katika **(44)** Maneno mawili, nomino ‘**matumaini**’ na kitenzi ‘**kupata**’ yameachwa. Kiteni likiwa ni neno ambalo hutumiwa katika sentensi kuashiria kitendo kilichofanyika, kitakachofanyika au kinachofanyika. Maneno haya ni nguzo muhimu katika upataji wa ujumbe. Mwanafunzi anapoandika bila hayo maneno huacha msomaji katika hali ya taharuki. Hujiuliza maswali, wanafunzi wanapewa nini? Na nani? Uhusiano gani uliopo kati ya kihuishi ‘**ya**’ na nomino ‘**kazi?**’ maana haijitokezi wazi. Vilevile katika **(45-49)**, mwanafunzi aliacha vihusishi (neno linaloonyesha uhusiano baina ya neno moja na neno au maneno mengine katika sentensi moja na nyininge). Vihuishi vilivyoachwa ni: ‘**za**’, ‘**ya**’, ‘**cha**’, ‘**mwa**’, ‘**wa**’ na ‘**wa**’. Kuachwa kwavyo kumezifanya kauli hizo kuwepo na kasoro. Mwanafunzi anapondika kwa haraka na kutopitia kazi baada ya kuiandika

husababisha kuwepo na kauli kama hizi. Mtafiti aliyarekebisha makosa husika kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi. Kwa kutafuta neno au vihusishi ambavyo vingeleta maana katika kauli husika. Hivyo basi, marekibisho yafuatayo ni tafsiri ya mtafiti.

42. Kutoka kwa magazeti tunapata mambo mapya na...
43. Chungu cha mboga kilipasuka wakati...
44. Huwapa wanafunzi matumaini ya kupata kazi...
45. Athari ya lugha ya sheng'...
46. Ili kukuza kiwango cha Kiswahili...
47. Magazeti huendeleza talanta tofauti mionganoni mwa wanafunzi
48. Magazeti hupasha ujumbe wa dharura juu...
49. Hutupa msamiati wa Kiswahili au Kiingereza na...

3.2.7 Kutenganisha Neno Visivyo

Kosa la kutenganishwa kwa neno moja hupatikana sana katika maandishi. Wanafunzi wengi hutatizwa na maneno yaliyo marefu sana kiasi cha kufikiria kulitenganisha ili yawe mawili au zaidi. Asemavyo MBAABU (1995), umbo la neno la aina hiyo huwa na mzizi wa vitenzi. Kabla ya mzizi huo viungo kadha wa kadha kama vile viambishi, na viungo vyatengeneza. Baada ya mzizi viambishi vyatengeneza kauli au jinsi tofauti kama vile *-ewa-* (kutendewa), *-esha* (kutendesha) na *-ana-* (kutendana) hupachikwa kwa mzizi wa kitenzi. Kwa kuwa viungo hivyo vyote havipatikani vikiwa huru, vyote pamoja na mzizi wa kitenzi huunda neno moja. Hivyo basi, neno moja linapotenganishwa hapatakuwepo na mawasiliano. Tapo hili lina makosa **67** ambayo ni asilimia **8.8**. Yafuatayo ni baadhi ya makosa tuliyotambua katika utafiti wetu:

- 50)* *Miti hani hi...*
- 51)* *Mwanafunzi huji nufaisha sarufi...*
- 52)* *Mbari yao ita kusanyika juma..*
- 53)* *Wana funzi wanaposoma magazeti...*
- 54)* *Magazeti ni chombo cha mawa siliano...*
- 55)* *Wanafunzi wengi hawazi elew..*
- 56)* *Kifaranga alishi kuwa na mwewe*
- 57)* *Nyanya aliki beba...*

58)*...*nilipofika nyumbani siku pata chakula...*

59)* *Kupata alama zitakazo wawe zesha...*

Ni wazi kwamba katika lugha ya Kiswahili hakuna maneno kama hayo yaliyopigiwa mstari hapo juu, bali ni sehemu za maneno na hazibebi maana kamili. Kwa mujibu wa Mdee (1986), neno ni mgawanyiko wa lugha wenye maana na maana hiyo hupotea ikiwa mgawanyiko usiofaa utatatumiwa. Baadhi ya maneno yakigawanywa huleta maana tofauti na ile iliyokusudiwa na mwandishi. Katika mfano wa (50), neno **miti hani** ni nomino na lilitengwa na kuwa maneno mawili yaliyo na maana mbili tofauti. ‘**Miti**’ likiwa na maana ya mmea wenye shina gumu na ‘**hani**’ ni kwenda kumpa pole mfiwa. Hivyo basi, kwa mujibu wa muktadha yanapotumiwa, ujumbe haueleweki vizuri. Maneno katika (51 na 52), viambishi awali ‘**huji**’ na ‘**ita**’ ambavyo ni muhimu kwa kitenzi vimetengwa na kujisimamia kama maneno kamili. Viambishi hivi hujengana na kuunda sarufi ya lugha. Mgullu (1999), anaeleza kuwa vitenzi vinaweza kuambishwa viambishi mbalimbali ili kuongezea maana mbalimbali za kisarufi. Hata hivyo, viambishi pekee havitaleta maana bila kuambishwa kwa mzizi wa neno.

Mifano iliyopo katika (53-57), inaonyesha namna ambavyo wanafunzi walivyotenganisha mzizi ambao kwa kawaida hautenganishwi, kwa kuwa ni sehemu kuu katika neno ambayo haibadilikibadiliki. Kwa mfano, maneno ‘**mawasiliano**’ na ‘**mwanafunzi**’ yalitengwa na kuunda maneno ambayo hayana maana yoyote katika sentensi. Hayo ni maneno ambayo kisarufi hayahitaji viambishi vyovoyote tena yanapotenganishwa huonyesha udhaifu wa mwanafunzi wa kutokuwa makini anapoandika insha yake. Katika sentensi ya (58), neno **sikupata** liliandikwa kama maneno mawili ambayo ni **siku** na **pata**. Haya ni maneno mawili katika mazingira ya sentensi hii na yalipoandikwa na mwanafunzi, maana iliyokusudiwa imepotea, kwani yamejitokeza kama mofimu huru. ‘Siku’ likiwa na maana ya kipindi cha muda wa saa ishirini na nne kuanzia asubuhi hadi asubuhi ilhali pata ni kuwa na jambo, hali au kitu. Ili kuleta maana iliyokusudiwa, maneno haya yanastahili kuandikwa kama neno moja ‘sikupata’. Kiambisi ‘si’ kinasimamia kikanushi ilhali kiambishi ‘ku’ ni cha wakati uliopita. Hivyo basi, inadhihirika wazi kuwa viambishi hivi haviwezi kujisimamia katika sentensi yoyote, kwa sababu viambishi hivi huwa ni mofimu tegemezi zinazohitaji mizizi ya vitenzi. Kwa mfano:

Kitenzi kilicho na matumizi ya ‘o’ rejeshi katika (59), kimetenganishwa na kuunda maneno matatu ambayo hayabebi maana yoyote. Neno ‘**zitakazo wawe zesha**’ ni tofauti kabisa na ‘**zitakazowawezesha**’. Mbaabu (1995:74), anadai kuwa neno likiwa refu huwatatiza baadhi ya wanafunzi kiasi cha kufikiria kuligawanya liwe maneno mawili au zaidi. Kwa kufanya hivyo husababisha kosa na hutinga mawasiliano. Wanafunzi hukisia kuwa ‘o’ rejeshi hutumiwa kuonyesha maneno yaliyo tofauti na hayapaswi kuunganishwa na kuunda neno moja. Marekebisho mwafaka ni kama ifuatavyo:

50. Mitihani yao...
51. Mwanafunzi hujinufaisha katika sarufi...
52. Mbari yao itakusanyika juma...
53. Wanafunzi wanaposoma magazeti..
54. Magazeti ni chombo cha mawasiliano...
55. Wanafunzi wengi hawazielewi...
56. Kifaranga alishikwa na mwewe...
57. Nyanya alikibeba...
- 58...dhidi ya tabia
59. Kupata alama zitazowawezesha...

Mwanafunzi anapoyagawa maneno hayo hapo juu (50-59), yanaweza kupoteza maana katika muktadha.

3.2.8 Matumizi ya Msamiati Usiofaa

Hali hii ya matumizi ya msamiati usiofaa, hutokea wakati mwanafunzi hupachika neno lisilofaa katika muktadha. Misamiati aliyo nayo inamkanganya na anaitumia vibaya anapajaribu kujielezea kwa lugha ya pili anayojifunza. Hali hii inapotokea kunatokea athari ya kimaana kwa sababu neno linabadilisha maana iliyokusudiwa. Pia, iligunduliwa kuwa maneno ambayo ni visawe na vitate yaliweza kubadilishwa na mwanafunzi hata bila mwanafunzi kugundua kuwa amefanya kosa. Hii ni kwa sababu maneno yanayokaribiana huweza kuwasilishwa pamoja katika ubongo wa binadamu na mwanafunzi huweza kuyatumia maneno hayo pasipo kutambua kuwa amesababisha makosa.

Vilevile mwanafunzi aliweza kubadilisha neno ili kuepukana na shida inayomkabili na hali hii humfanya kutumia mbinu zake maalumu kuunda neno litakalofaa katika hali hii yake. Makosa haya yanayofanywa na mwanafunzi yanadhihirisha hali yake ya leksia katika ubongo wake. Kwa mujibu wa K.I.E (2000), wanafunzi wengi wa shule za msingi na sekondari wanakumbwa na matatizo ya kimatamshi, uteuzi wa msamiati, sarufi na kuingiliana kwa lugha, hali ambayo huathiri mawasiliano. Baadhi ya wazungumzaji wanaelewaka kwa shida ilhali wengine hawaeleweki kabisa. Tapo hili ndilo lililokuwa na idadi kubwa ya makosa yaliyotambuliwa na kuchanganuliwa katika matini za watafitiwa. Makosa **110** ambayo ni asilimia **14.7** yalitambuliwa. Baadhi ya makosa hayo ni:

60)* *Baba alinunua nyumba kwa bei gari ya...*

61)* *Baba alienda baharini kushika papa wa...*

62)* *kuku anachungulia kifaranga...*

63)* *Baba hufanya kazi kwa nguvu ili...*

64)* *Magazeti hujenga msamiati wa...*

65)* *Nilipomaliza shule...*

66)* *Mwalimu Mkuu ana mpango wa kando...*

Katika mfano wa (60) neno ‘**gari**’ ni tofauti na neno ‘**ghali**’ ambalo lingetumiwa katika kauli hii. Gari lina maana ya chombo cha kusafiria na ghali ni bei kubwa. Kwa kutumia neno gari nafasi ya ghali maana hupotea. Huu mfano unaashiria hali ya kuimarika kwa konsonanti. Schane (1973) anaifahamu kanuni hii kama kanuni ya kiasilia ya usimilisho tangulizi katika lugha nyingi za kibantu, mfanyiko huu huhusu, likwidi /l/ na /r/. Dhana ya kuimarika inarejelea hali ya sauti ambayo kwa kawaida hutamkwa kwa nguvu kidogo kubadilika na kuwa ya kutamkwa kwa nguvu nyingi. Nguvu za sauti huditidimika kutoka kwa vipasuo vikielekea kwa vizuiwa-kwamizwa, vikwamizwa, nazali, likwidi, nusu irabu na mwishowe irabu. Kudhoofika huku kunazingatiwa pia na hali ya mghuno. Kwa mfano, sauti za vipasuo zisoghuna zinahitaji nguvu nyingi kuliko zile ambazo ni sauti ghuna. Tazama jedwali lifuatalo:

Jedwali la 5: Kielelezo cha kuimarika kwa konsonanti.

	SI GHUNA	GHUNA
Vipasuo	1	2
Vizuiwa-kwamizwa	3	4
Vikwamizwa	5	6
Nazali		7
Likwidi		8
Nusu irabu		9
Irabu		10

Asili: Mtafiti (2016).

Sauti zilizo katika nafasi ya kwanza ni vipasuo visoghuna na zinazohitaji nguvu nyingi. Zilizo katika nafasi ya pili ni vipasuo ghuna. Nafasi ya tatu ni vizuiwa-kwamizwa visoghuna kisha vizuiwa-kwamizwa ambazo ni ghuna. Nafasi ya tano ni vikwamizwa

visoghuna zikifuatwa na zile ambazo ni ghuna. Nazali zimechukua nafasi ya saba kisha likwidi hufuata. Kwa hivyo sauti zilizodhaifu zaidi ni zile za irabu. Hivyo basi, iwapo mfanyiko utatokea unaobadilisha sauti fulani kiasi cha kupata sifa za sauti inayohitajika nguvu zaidi ili kutamka, sauti hiyo husemekana kwamba imeimarika.

Pia, makosa yalitokea katika kauli hizo hapo juu kwa sababu mwanafunzi alitumia msamiati unaokaribiana sana kimaana lakini kisemantiki haufai katika muktadha husika. Mfano katika (61), huwa ni kosa kwa sababu mwanafunzi alitumia '**kushika**' akirejelea dhana ya kushika mtu mkononi au kamata badala ya '**kuvua**' ambalo lingefaa zaidi katika muktadha, likiwa na maana ya kunasa samaki kutoka majini. Kauli katika (61), '**anachungulia**' ni kosa kwa sababu mwanafunzi alitumia msamiati usiofaa badala ya kutumia neno '**linda**' ambalo lingefaa zaidi na ujumbe kueleweka bila shida yoyote. Mwanafunzi anaposhindwa kujieleza katika lugha lengwa, atarejelea lugha anayoifahamu vizuri ambayo ni lugha yake ya kwanza. Katika Nadharia ya Sarufi Zalishi, Chomsky (1957), anadai kuwa atatumia ujuzi alionao katika lugha asilia kujieleza katika lugha lengwa. Uwezo huo humwezesha kutumia maumbo na miundo ya lugha asilia katika mawasiliano andishi ya lugha lengwa. Hivyo basi huhamisha dhana kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili, sarufi ya lugha ya kwanza huwa msingi wa sarufi ya lugha ya pili. Mwanafunzi atatumia sarufi tayari anaifahamu akiendelea kujifunza sarufi ya lugha lengwa.

Msamiati '**nguvu**' badala ya '**bidii**' katika (62), ni tofauti japo yana maana sawa tunaporejesha fikra zetu kwa kufanya jambo. Nguvu ni uwezo wa kufanya jambo na bidii ni jitihada au ari ya kufanya jambo. Neno bidii ndilo lililofaa zaidi, lakini mwanafunzi alichanganyikiwa na kutumia msamiati usiofaa. Mfano uliopo katika (63), neno '**jenga**' lilitumiwa visivyo badala ya neon '**kuza**'. Jenga lina maana ya kutengeneza nyumba na kuza ni kitu kupata kuzidi. Maneno haya yalimkanganya mwanafunzi na kwa kutumia jenga badala ya kuza maana inavurungika. Vilevile katika (64), '**shule**' ni mahali wanafunzi hupata mafunzo na '**masomo**' ni mafunzo ya kutupa ubingwa wa fani maalumu. Mwanafunzi anapotumia maneno haya katika sentensi hufikiria kuwa yanaweza kubadilishana nafasi na maana iliyokusudiwa kusalia. Hii huonyesha hali ya kutotumia

sheria kikamilifu. Mwanafunzi hutumia sheria zilizo rahisi kuwasilisha hoja zake. Tujuavyo, jinsi mtu anavyowasiliana ndivyo anavyoandika, kwa hivyo atahamisha makosa yale ayafanyanyo wakati wa mawasiliano na kupeleka katika maandishi. Mwanafunzi anaposhindwa ni msamiati upi mwafaka katika matini anaishia kutumia msamiati potovu.

Vilevile mfano uliopo katika **(66)**, mwanafunzi amekosea kwa kuchagua msamiati ‘**mpango wa kando**’ na kuutumia badala ya ‘**mkware**’ au ‘**jicho la nje**’ ambalo ni mwafaka zaidi. Licha ya kuwa ni kupunguza makali (tasfida) hufanya kauli husika kutoeleweka kwa haraka. Misamiati hii hutokea kwa sababu ya misimu (semi za muda ambazo hubuniwa na kutumiwa katika mazingira maaluma na katika kipindi maalumu cha wakati). Misimu hii hupata maana yake kutoka kwa watumiaji pamoja na muktadha wa mahali na wakati. Ingawa misimu huzuka na kutoweke baada ya muda, baadhi ya misimu hudumu na kukubalika kama semi / msamiati sanifu wa lugha.

Misamiati iliyopigiwa mstari hapo juu **(60-66)**, huweza kutumiwa katika muktadha fulani na isisababishe kosa lolote. Kisarufi neno huwa sawa lakini nafasi yake katika sentensi husababisha kasoro kimaana. Wanafunzi wanaposhindwa kutambua maana ya msamiati husika, wanatumia msamiati usiofaa katika sentensi. Wanafunzi wengi huwa na hoja nzuri lakini hupoteza alama kwa kutojua namna ambavyo wanatumia msamiati mwafaka katika maandishi. Makosa hayo yangesahihishwa kama ifuatavyo:

60. Baba alinunua nyumba kwa bei ghali
61. Baba alienda baharini kuvua papa...
62. Kuku anamlinda kifaranga...
63. Baba hakufanya kazi kwa bidii
64. Magazeti hukuza msamiati...
65. Nilipomaliza masomo...
66. Mwalimu Mkuu ana jicho la nje (mkware)...

3.2.9 Kuacha Sauti katika Neno

Katika lugha yoyote ile neno huwa ni mkusanyiko wa silabi zinazoweza kutamkwa kama kitu kimoja au kuandikwa na kuleta maana fulani. Hivyo basi, neno lisiponakiliwa vizuri

maana iliyokusudiwa haitamfikia msomaji na hapatakuwepo na mawasiliano yoyote. Makosa haya hutokea kwa kuacha silabi moja au mbili katika neno. Katika utafiti huu, kundi hili lilikuwa na makosa (58) ambayo ni sawa na asilimia 7.8. Mifano ifuatayo inadhihirisha makosa hayo:

- 67)* *Ma i di yalibadilishwa kwa kupata papa...*
- 68)* *Fatuma aliosha vyobo vile kwa ...*
- 69)* *Baba almnulia kitabu cha Fasihi na...*
- 70)* *Magazeti hum elimisha...*
- 71)* *Huweza famisha mwanafunzi...*
- 72)* *Magazeti huwawesha kuandika i sha ya...*
- 73)* *Huwapa wa funzi mwelekeo wa...*
- 74)* *Nchi ngine huwa na...*
- 75)* *Baba livua papa kubwa wa...*

Sauti ambazo zimeachwa katika (67-75), hujumuisha irabu na konsonantsi. Katika (67), neno ‘**maidi**’ ambalo ni nomino halikuendelezwa vizuri, sauti /h/ na /n/ zimeachwa na kulifanya neno hilo kutokuwa na maana iliyonuiwa. Mwanafunzi aliathiriwa na lugha yake ya kwanza kwa sababu baadhi ya jamii-lugha huwa hazina sauti hizi katika lugha zao (rejelea jedwali la ukurasa 59). Mfano wa (68), mwanafunzi aliacha sauti moja ya konsonanti /m/ ambayo ni muhimu sana katika neno ‘**vyombo**’ na kulifanya neno hilo kutosheheni maana yoyote. Katika ngeli ya **ki-vi** viambishi viwili ‘**ki-**’ na ‘**vi-**’ au ‘**ch-**’ na ‘**vy-**’ hutumiwa kuashiria umoja na wingi mtawalia. Mwanafunzi anapoacha kuvitumia viambishi hivyo vya ngeli katika nomino husika au katika sentensi, huashiria upungufu wa umilisi wa viambishi ngeli katika Kiswahili. Hali hii ilichangia kuwepo kwa ujumbe ulio na utata. Katika mifano ya (69- 73), wanafunzi wameacha sauti moja au mbili katika baadhi ya maneno. Kwa mfano, neno **alimnulia** <alimnunulia>, **humelimisha** <humwelimisha>, **famisha** <fahamisha>, **huwawesha** <huwawezesha>, **isha** <insha> na **wafunzi** <wanafunzi>, yalitumiwa badala ya maneno yaliyopo mabanoni ambayo yangewasilisha ujumbe uliohitajika katika kauli hizo. Vilevile katika (74), kivumishi ‘**ingine**’ ambacho ni kivumishi cha pekee kimenakiliwa bila kuambishwa kiambishi muhimu cha kuashiria ngeli ya nomino husika. Kiambishi ‘nyi’ ambacho kinaashiria nomino nchi kimedondoshwa na mwanafunzi husika. Vilevile mfano katika (75) kiambishi

‘**a**’ ambacho kinaashiria nafsi na ‘**m**’ ambacho ni kiambishi kinachoashiria kitendwa katika kitenzi **vua** kimeachwa. Pia, kivumishi **kubwa** kimeandikwa bila kiambishi ‘**m**’ na kukosa upatanisho wa kisarufi na kupelekea kuwepo kwa sentensi zilizo na upungufu. Makosa haya yanaweza kurekebishwa kama ifuatavyo:

67. Mahindi yalibadilishwa kwa kupata papa...
68. Fatuma aliosha vyombo vile kwa...
69. Baba alimnunulia kitabu cha Fasihi na...
70. Magazeti humwelimisha...
71. Huweza kumfahamisha mwanafunzi...
72. Magazeti huwawezesha kuandika insha ya...
73. Huwapa wanafunzi mwelekeo wa...
74. Nchi nyingine huwa...
75. Baba alimvua papa mkubwa...

3.2.10 Kubadilisha Mpangilio wa Fonimu katika Neno

Katika matini za wanafunzi tulizochanganua, tulibaini kuwa baadhi yao walibadilisha mpangilio wa fonimu katika baadhi ya maneno. Hali hii ilichangia kuwepo kwa maneno yanayotatiza uwasilishaji wa ujumbe uliodhamiriwa. Hili ndilo kundi ambalo likuwa na makosa machache mno. Makosa **33** ambayo ni asilimia **2.3** yaligunduliwa. Makosa hayo yanaweza kuchukuliwa kama ya taipu, lakini mtafitiwa aliyaradidi. Umaratokezi wa kila kosa ulichukuliwa kama kosa la kisemantiki kwa sababu maana iliyokusudiwa haikumfikia msomaji. Yafuatayo ni baadhi ya makosa tuliyotambua katika utafiti wetu:

- 76)**Chungu sizisohesabika...*
- 77)**Yule in mnogojwa na...*
- 78)**Mama aliweka kikombe juu ya maze...*
- 79)**Wanafunzi kufahamu mambo bararaba jnsi...*
- 80)**Wanafunzi wanafaidika kwa kujitayarisha mtahina na...*
- 81)**Wanafunzi wengeni hupenda magazeti ili...*
- 82)**Huwafahamisha mambokusuhu...*
- 83)**Magazeti huweza kuboresha msamiati, safuri...*
- 84)**Gazeti ni kijitabu ambacho kina kusarana kinachachopishwa ili...*

85)*. *Magazeti yanatusaidia kukuza luhga...*

Kuanzia mfano wa (76-85), maneno yaliyopigiwa mstari huashiria kuwa watafitiwa walibadilisha mpangilio wa fonimu na kuzifanya kauli hizo kutoamiliika kimaana. Baadhi ya fonimu ambazo zimebadilishwa ni zile zinazokaribiana sana kimatamshi. Ubadilishanaji wa mpangilio huu katika neno ‘**in**’ katika (76), hutokana na mazoea ya lugha ya Kiingereza. Badala ya neno husika kuchukua mpangilio wa Kiswahili ‘**ni**’, wanafunzi aliliandika kwa lugha ya Kiingereza.

Mfano wa (77), mtafitiwa ametumia irabu /a/ mahali ambapo irabu /e/ ingetumiwa. Kwa kufanya hivyo, neno la msimbo ‘**maze**’ liliundwa ambalo lina maana ya msichana badala ya neno ‘**meza**’ ambalo lina maana ya kitu kilichotengenezwa kwa mba, madini au kioo chenye uvungu na ubapa juu unaotumiwa kwa kulia, kuandikia au kwa kuchezza. Lakini mtafitiwa alipotumia ‘**maze**’ alichangia kuwepo kwa kasoro na kutinga mawasiliano. Katika mifano iliyopo (78-85), maneno **bararaba, mtahina, wengeni, kusuhu, safuri, kusara, kilichachopishwa** na **luhga**, mpangilio wa fonimu umebadilishwa na matokeo yake ni kuvurugika kwa maumbo ya maneno husika na kupelekea ujumbe kutoeleweka na aliyedhamiriwa. Mara nyingi wanafunzi wanapopewa mjarabu wa kuandika insha ya Kiswahili, hupewa maagizo ya kuzingatiwa. Miongoni mwa maagizo hayo ni muda wa kuandika insha. Pia wanafahamishwa urefu wa kila insha. Kwa mfano, katika utafiti huu, watafitiwa walipewa muda wa saa moja na urefu wa maneno (200-250). Wanafunzi huchukulia muda kuwa mchache hali ya kuwa hauwatoshii kuwakilisha hoja zao. Kwa hivyo wanaandika kwa kasi sana ili waweze kumaliza hoja zao kwa muda wa saa moja na urefu wa maneno 200-250 uliohitajika. Wanakosa wakati wa kufikiria zaidi ya kupanga wanayokusudia kuandika. Hatimaye, huandika wasiyokusudia wakifanya makosa, hususani ya kubadilisha mpangilio wa fonimu unaostahili katika lugha ya Kiswahili.

Aidha, wanakosa wakati wa kupitia nakala zao kabla ya kuzitoa kwa mtahini. Sentensi zilizopo hapo juu (76-85) zilikuwa na makosa ya ubadilishaji wa fonimu. Mtafiti angeweza kuyaepuka makosa haya kama angekuwa makini wakati akiandika insha yake au kudurusu kazi yake baada ya kuikamilisha na hatimaye kuiwasilisha kwa usahihishaji.

Maneno hayo yangeandikwa kama ifuatavyo:

76. Chungu hawakuhesabika...
77. Yule ni mgonjwa...
78. Mama alikiweka kikombe juu ya meza...
79. Wanafunzi wanafahamu mambo barabara jinsi...
80. Wanafunzi wanafaidika kwa kujinufaisha mitihani...
81. Wanafunzi wengine hupenda magazeti ili...
82. Huwafahamisha mambo kuhusu...
83. Magazeti huweza kuboresha msamiati, sarufi...
84. Gazeti ni kijitabu ambacho kina kurasa na kilichochapishwa...
85. Magazeti yanatusaidia kukuza lugha...

3.2.11 Kuunganisha Maneno Visivyo

Luga ya Kiswahili ina mofimu mbalimbali ambazo huunganishwa kwa kuunda maneno ya Kiswahili. Maneno haya huwa ya aina mbalimbali, kwa mfano, nomino, Kivumishi, kitenzi, kielezi, kiwakilishi, kiunganishi, kihuishi na kihisishi. Kila neno lazima lijisimamie katika sentensi kulingana na uhitaji. Kwa sababu hii kuunganishwa kwa maneno husababisha utata katika sentensi ya Kiswahili.

Kwa hivyo, maneno yanapotumiwa katika sentensi hutarajiwa yawasilishe ujumbe muhimu, lakini yanapounganishwa na kuandikwa kama neno moja huwatatiza wasomaji wa insha, barua au maandishi yoyote yale. Maana inayokusudiwa inaweza kupotea na msomaji anaweza kupata maana isiyokusudiwa. Mipaka kati ya neno na neno inahitajika iwe wazi ili pasiwe na utata wakati wa kusoma maandishi.

Asemavyo MBAABU (1985), maneno mawili yanapounganishwa huunda istilahi mpya za Kiswahili ambazo hutumiwa katika maandishi pasi kujuu kama zinawasilisha maana au la. Katika nomino kuna baadhi yao ambazo huunganishwa na kuunda nomino moja inayokubalika na inayowasilisha dhana moja na wala si mbili. Kwa mfano,

(Nomino+Nomino) mbwa + mwitu= mbwamwitu lililo na maana ya mnyama wa jamii ya mbwa aishiye porini. Hivyo basi, kuyaunganisha maneno visivyo na kuyatumia kama neno moja kulijitokeza katika uchanganuzi wa matini za baadhi ya watafitiwa. Makosa yaliyotambuliwa ni **46** ambayo ni sawa na asilimia **6.2.** Makosa hayo yanadhihirika katika mifano hii:

86)* *Yego anasifanjema...*

87)* *Wakisoma magazeti hujikosoa kisarufihijainakadhalika....*

88)* *Kwetu si mbali na dukakuu*

89)* *Chungu hiki kinamaji...*

90)* *Magazeti yana sehemu ambazo nizamuhimu...*

91)* *Ukosefu wa vitabu vya kiadavya ...*

92)* *Magazeti yanafaa kupelekwa shulen i kila mara ilikuwawezesha...*

Katika mifano **(86-92)**, mwanafunzi aliyunganisha maneno mawili hata matatu na kuunda istilahi moja ambayo haina maana. Maneno matatu katika **(86)** yaliunganishwa visivyo na kuunda neno ambalo hata kulitamka ni shida, ‘**anasifanjema**’(ana +sifa +njema). Kwa kufanya hivyo maana hupotea kwa sababu katika Kiswahili na hata kamusi hamna neno la muundo huo. Maneno hayo matatu ni tofauti na yalistahili kuwekewa nafasi ya kuyatenga ili ujumbe uweze kumfikia aliyenuiwa. Katika mfano wa **(87)**, nomino mbili zimeunganishwa na kuunda neno ‘**kisarufihijai**’ ambalo linapelekea kuwepo na dosari (kisarufi + hijai). Kiunganishi ‘**na**’ kimeunganishwa na neno ‘**kadhalika**’ na kuunda neno **nakadhalika** ambalo limepelekea kauli hiyo kupoteza maana. Katika mfano wa **(88)** nomino **duka** na kivumishi cha sifa **kuu** ni maneno ambayo hayastahili kuunganishwa. Kwa kuyaunganisha na kuunda neno moja ‘**dukakuu**’ (duka + kuu) hupelekea kuwepo kwa kosa la kisemantiki na hivyo kusababisha kasoro katika sentensi husika.

Katika mfano wa **(89)**, kuna kosa la kuunganisha kitenzi na nomino na kuunda neno moja ‘**kinamaji**’. Kitensi **kina** kinamaanisha kuwa na kitu fulani huku **maji** likimaanisha kiowevu kinachopatikana kutokana na mvua katika bahari, maziwa, mito na kadhalika ambacho hutumika kwa kupikia, kunywa au kuoga. Maneno hayo yalipounganishwa yalipelekea kuwepo kwa msamiati usioafiki maana lengwa. Vilevile maneno matatu yaliunganishwa katika mfano wa **(90)**. Mwanafunzi aliunganisha kitensi kishirikishi

kipungufu, kihuishi na kivumishi (ni + za + muhimu) sawia na (91) pale ambapo kivumishi kimeunganishwa na kihuishi (kiada + vya). Mfano wa (92) neno ‘ili’ ni kiunganishi kitumiwacho kuyaunganisha mawazo tofauti katika sentensi na hivyo ni kosa kukiunganisha na kitenzi ‘**kuwawezesha**’ ambacho hufanya kazi tofauti katika sentensi husika. Hivyo basi, maneno yaliyounganishwa hapo juu yanawatatiza wasomaji wengi na kupelekea kupatikana kwa ujumbe usiokusudiwa na mwandishi. Yafuatayo ni marekebisho ya kauli hizo:

86. Yego ana sifa njema...
87. Wakisoma magazeti hujikosoa sarufi, hijai na kadhalika.
88. Kwetu si mbali na duka kuu..
89. Chungu hiki kina maji..
90. Magazeti yana sehemu ambazo ni za muhimu...
91. Ukosefu wa vitabu vya kiada vya...
92. Magazeti yanafaa kupelekwa shulen i kila mara ili kuwawezesha...

3.3 Vyanzo vya Makosa ya Kisemantiki

Ni vigumu kuamua kwamba hali au kosa fulani hutokana na sababu maalumu kwa kuwa kosa moja linaweza kusababishwa na mambo mengine mengi. Vyanzo vilivyojadiliwa vilielezwa kutoka kwa matokeo yaliyopatikana kutokana na hojaji pamoja na usahihishaji wa insha za wanafunzi. Vyanzo hivyo ni pamoja na:

1. Athari ya sheng'
2. Athari ya lugha ya kwanza
3. Ukiukaji wa sheria za lugha lengwa
4. Athari ya lugha ya ushairi
5. Kuandika kwa haraka

3.3.1 Athari ya Sheng'

Sababu ya kushamiri na kuenea kwa msimbo wa sheng ni kutokana na vijana kutaka kuzungumza mambo yao ya siri. Pia uvivu wa mwanafunzi wa kutotaka kuandika maneno kikamilifu huchangia kuwepo kwa makosa ya kisemantiki na hatimaye kuwasilisha

ujumbe ambao haueleweki na msomaji. Kwa mujibu wa Githiora (2002) sheng ni maarufu kimawasiliano mionganini mwa familia za mitaani jijini Nairobi, wafanyakazi wa kuajiri, kwa mfano, wachuuzi, vijana wa kuegesha magari, wafanyakazi wa juakali mionganini mwa wengine. Hata hivyo, kwa sasa msimbo wa sheng unaanza kupata umaarufu mkubwa kimatumizi na umeanza kupenya na kuwa lugha ya matumizi kwa watu wa madaraja karibu yote mijni. Lugha ya msimbo ya sheng kwa mujibu wa Muake (2011), pia imeanza kutumika hata katika vyombo mbalimbali vya habari. Kama vile redio, runinga na baadhi ya magazeti nchini Kenya na vilevile imeanza kusambaa kutoka mitaa ya watu wa mapato ya chini katika miji kama Nairobi na kuanza kutumika katika maeneo mengine mengi ya kijamii, kama vile vyombo vya habari katika Sanaa hususani muziki na uigizaji.

Wanaomiliki vyombo vya habari wamegundua matumizi ya sheng ndiyo njia mwafaka zaidi ya kulifiki soko kubwa la vijana kwa ajili ya kueneza matangazo ya bidhaa na huduma za kibashara. Kwa hivyo sheng imekuwa daraja la kuwafikia na kuwavutia vijana ambao ndio asilimia kubwa ya Wakenya.

Wazazi wengi katika miji mikubwa nchini Kenya nao huona sheng kama msimbo unaotumiwa na vijana kuweka mpaka wa kimawasiliano kati yao na wazazi wao. Vilevile wazazi huchukulia sheng kama msimbo wa ukaidi mionganini mwa vijana na msimbo usio na faida zozote kielimu. Hatimaye, mwanafunzi hujifunza kanuni fulani kutoka sheng na kuzitumia kwa mapana katika uandishi wake. Matokeo yake ni ujumbe uliovurugika ambao unatinga mawasiliano kwa kuwa anayesoma anaweza kupata ujumbe uliokusudiwa au usiokusudiwa. Kwa mfano,

93* Magukaa hupenda kula papa kila...

Sahihi: Wazee hupenda kula papa kila...

94)* Magazeti huwapa wanafunzi shughuli wakati wameboeka na...

Sahihi: Wanafunzi husoma magazeti wakati hawana kazi na...

Mifano hiyo inaonyesha kwamba mwanafunzi ameathiriwa na msimbo wa sheng. Kwa mfano, katika (93), mwanafunzi alipotumia neno ‘**magukaa**’ alitaka kufikisha ujumbe kwamba wazee (wenye umri mkubwa) wanapenda kula papa (samaki mkubwa wa baharini) ujumbe haueleweki moja kwa moja. Na mfano wa (94), mwanafunzi ametumia

neno ‘**wameboeka**’ ambalo lina maana ya ‘**hawana kazi**’. Hivyo basi, uchunguzi huu ulitumika kuonyesha baadhi ya makosa ya kisemantiki yaliyofanywa na watafitiwa kutokana na athari ya msimbo wa sheng.

Msimbo huu huonekana kama lugha inayotinga ujifunzaji wa lugha rasmi nchini Kenya, ambazo ni Kiingereza na Kiswahili na ambazo pia hutumika kuendesha masomo shulen. Kulingana na Iraki (2004), umaarufu wa matumizi ya sheng miongoni mwa vijana hasa katika sehemu za mijini nchini Kenya ni tatizo kubwa katika ujifunzaji wa sarufi sahihi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza shulen. (Mifano zaidi ya matumizi ya sheng na marekebisho yako katika ukurasa wa 50).

3.3.2 Athari ya Lugha ya Kwanza

Katika mchakato wa ujifunzaji wa lugha ya pili, mwanafunzi huzalisha msamati usio sanifu kutokana na athari ya lugha yake ya kwanza. Cruse (1986) katika uchunguzi wake aligundua kwamba makosa mengi huwa na ufananisho wa lugha ya kwanza na sentensi nydingi huvuruga maana iliyodhamiriwa na mwandishi. Anaendelea kusema kwamba watu wanapojojifunza lugha ya pili huwa tayari wanayo lugha ya kwanza. Baadhi ya kanuni wanazozielewa katika lugha ya kwanza hutumiwa katika usemajji na uandishi wa lugha ya pili. Tayari akilini mwake amemudu mifumo ya lugha ya kwanza anayoitumia kila siku katika mawasiliano. Kutokana na hali hii kuna mazoea ya kuzitumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili na hivyo makosa hutokea. Katika utafiti wetu tuligundua kuwa watafitiwa walioshiriki katika utafiti huu waliathiriwa sana na lugha zao za kwanza na kupelekea kuwepo kwa makosa ya kisemantiki katika matini zao. Kwa mfano:

3.3.2.1 Mrundiko wa Maneno katika Sentensi

Athari ya lugha za kwanza za watafitiwa ilipelekea kuwepo kwa mrundiko wa maneno katika sentensi na kuleta kasoro katika matini zao. Licha ya kwamba lugha ya kwanza ndiyo husababisha makosa hayo, kwa upande mwengine makosa hayo hutokea kwa sababu mwanafunzi hajui uamilifu wa viambajengo (nomino, kiwakilishi, kivumishi, kitenzi, kielezi, kiunganishi, kihuishi na kihisishi). Udhaifu huu wa mwanafunzi kushindwa kubainisha nafasi na matumizi ya viambajengo vya sentensi huhuishwa na namna ya

ujifunzaji wa lugha ya pili.. Hii ni kutokana na kutokuwa na umilisi wa viambajengo au utaratibu wa kupanga maneno katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano:

95)**Magazeti pia humpa uzoefu mwanafunzi kwani kusoma yeye anaweza kuwa na uzoefu wa kusoma vitabu vilivotaniwa ili kupita mtihani na...*

Sahihi: Pia, magazeti humpa mwanafunzi uzoefu wa kusoma kwa mapana kwa minajili ya kupita mtihani na...

96)* *Yale yanayoendelea huko nje wanafunzi wanayapata kutoka kwa magazeti wao wakiwa ndani ya shule wakiendelea na...*

Sahihi: Magazeti huwajuza yanayotendeka katika nchi yao...

Au

Magazeti huwafahamisha yanayojiri wakiwa shulen...

Katika mfano (**95 na 96**) wanafunzi walirundika maneno na mengine kuyaendeleza visivyo kama vile neno ‘**taniwa**’ badala ya ‘**tahiniwa**’ na kumfanya msomaji kutatizika. Pia, mwanafunzi hakuzingatia mpangilio wa maneno unaostahili katika lugha ya Kiswahili. Asemavyo Talmy (2000), kando na uneni wowote ule, mpangilio wa matukio na imani kuhusu mambo fulani, lazima yawepo ili maana iweze kujitokeza katika muktadha. Hivyo basi, maneno katika sentensi hustahili kupangwa kwa njia inayofaa ili ujumbe umfikie aliyedhamiriwa.

3.3.2.2 Kuacha Sauti katika Neno

Kosa hili hutokana na matamshi ya watafitiwa ambayo yalihamishwa kutoka lugha zao za kwanza katika uandishi wa matini zao. Pia mwanafunzi anapoandika matini yake kwa haraka kuna uwezekano wa kuacha baadhi ya sauti katika neno au maneno. Baadhi ya sauti zilizodondoshwa huwa hazipatikani katika lugha za kwanza za watafitiwa. Wakati mwingine wanafunzi huingiza miundo ya lugha zao za kwanza katika lugha husika. Hii ni kwa kuwa ni nadra sana sauti zilizoachwa kupatikana katika lugha ya kwanza ya mwanafunzi, (rejelea jedwali la 4, ukurasa wa 51). Kwa mfano:

97)* *Wanafunzi wanaeza kusoma magazeti ili...*

Sahihi: Wanafunzi wanaweza kusoma magazeti ili...

98)* *Huonyesha maendeleo ya s^hule na...*

Sahihi: Huonyesha maendeleo ya shule...

Kwa mujibu wa mifano hiyo (97-98) ni wazi kuwa watafitiwa waliacha sauti moja au mbili katika baadhi ya maneno na kuzifanya kauli hizo kuwa na utata katika uwasilishaji wa ujumbe. Watafitiwa waliacha sauti (**w**) katika neno **walieza** badala ya kuandika **waliweza** na sauti (**h**) iliachwa katika neno **shule**.

3.3.2.3 Kutumia Fonimu Isiyofaa katika Neno

Haya makosa huchangiwa na athari ya lugha za kwanza za watafitiwa. Watafitiwa walitumia fonimu isiyofaa katika baadhi ya maneno kwa kuwa hizo ndizo sauti ambazo wamezoea katika lugha zao za kwanza na kuyafanya maneno husika kuwa na kasoro. Hali hii ilipelekea kuwepo kwa ujumbe usioelewaka kabisa. Kwa mujibu wa Mgullu (1999), hali hii hutokana na matamshi ya baadhi ya wazungumzaji na labda pia kutosikia vizuri kwa baadhi ya wasikilizaji. Katika **jedwali la 4** (ukurasa wa 52) tulionyesha sauti ambazo zinaweza kutambulishwa na kutofautisha jamii-lugha mbalimbali. Mifano ifuatayo ni ithibati tosha ya makosa yaliyojitokeza katika matini za watafitiwa:

99)* Tunapochalibu kuzoma magazeti tunajifunza...

Sahihi: Tunapajaribu kusoma magazeti tunajifunza...

100)* Shulen i kuna uapa wa magazeti ya...

Sahihi: Shulen i kuna uhaba wa magazeti...

Katika mfano wa (99) mwanafunzi alichanganyikiwa kati ya konsonanti **ch** na **j** ambazo zote ni vipasuo-kwamizwa na hutamkwa huku upande ulioinuliwa juu wa ulimi ukiwa katikati mwa kinywa. Hii ni kwa sababu baadhi ya watafitiwa hawana fonimu **j** katika lugha zao za kwanza. Vilevile katika (100) mwanafunzi ametumia fonimu **p** isiyofaa kwa neon **uapa** badala ya **uhaba**. Licha ya kwamba **p** na **b** ni vipasuo na hutamkwa kwa kuibana hewa kwenye midomo, tofauti ni kwamba watafitiwa hawana **b** ambayo ni ghuna katika lugha zao za kwanza badala yake wana **p** ambayo si ghuna.

3.3.2.4 Uteuzi wa Msamiati Usiofaa

Mwanafunzi aliathiriwa na lugha ya kwanza na kutumia msamiati usiofaa katika muktadha na kupelekea kuwepo kwa maana isiyokusudiwa. Mwanafunzi hutumia msamiati usiofaa anapajaribu kujieleza katika matini yake. Hii ni kwa kuwa maneno haya ya lugha ya pili hayajaratibiwa vizuri katika leksikografia ya mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili. Mwanafunzi husababisha makosa haya anapajaribu kuiwakilisha lugha yake ya pili ambayo anajifunza. Ellis (1994) akimnukuu, Corder (1978), anasema kwamba watu wanaojifunza lugha ya pili huwa tayari wanayo lugha ya kwanza. Baadhi ya kanuni wanazozielewa katika lugha ya kwanza huzitumia katika usomaji na uandishi wa lugha ya pili.

Pia lugha ya Kiswahili ilichangia makosa ya matumizi ya msamiati usiofaa katika maandishi. Hii ni kwa sababu mwanafunzi huwa na msamiati sahihi lakini hushindwa kutofautisha ni upi mwafaka katika sentensi husika. Pia, hali duni ya ujifunzaji wa lugha ya pili na ukosefu wa umilisi wa sheria za lugha ya pili katika hatua ya ujifunzaji huchangia kuwepo kwa makosa husika. Asemavyo Gouala (1991), wanafunzi huathiriwa na lugha zao za asili katika uwezo wa kupata lugha ya pili. Kwa mfano:

101)* *Watasoma magazeti ili wasikie yanayoandikwa..*

Sahihi: *Watasoma magazeti ili waelewe yanayoandikwa...*

102)* *Uzuri wa magazeti shulen ni...*

Sahihi: *Umuhimu wa magazeti shulen ni...*

Katika mfano (101), mwanafunzi alitumia neno ‘**wasikie**’ likiwa na maana ya kupokea mawimbi ya sauti kwa kutumia sikio badala ya neno ‘**kuelewa**’ ambalo lina maana ya kufahamu jambo ambalo ni mwafaka katika kauli hiyo. Mwanafunzi ametumia neno ‘**uzuri**’ katika (102), likiwa na maana ya kupendeza na kupelekea ujumbe kutoeleweka badala ya kutumia neno ‘**umuhimu**’ ambalo ni hali inayofanya kitu au jambo fulani lihitajike katika jamii.

3.3.2.5 Ufanuzi Uliokithiri

Mwanafunzi hufanya makosa kwa kutumia wanachojua kuhusu lugha kwa hali ambapo sheria hizo hazitumiki. Mwanafunzi huwa ana umilisi wa kanuni za lugha fulani na anapajaribu kujieleza, hutumia kanuni za lugha hizo kwa kueleza hoja zake kwa lugha lengwa. Brown (1994), anaeleza kuwa ufanuzi uliokithiri ni ishara ya mwanafunzi kuazima ruwaza kutoka kwa lugha ya kwanza na kutanua ruwaza katika lugha ya pili. Pia, ukosefu wa umilisi wa msamiati mwafaka kwa mwanafunzi utakaomwezesha kuandika sentensi zilizo sahihi kimantiki. Hatimaye mwanafunzi hulazimika kutafakari hoja zake katika lugha ya lengwa ya Kiswahili na husababisha makosa ya kisemantiki kwa kuwa ujumbe haumfikii aliyedhamiriwa. Matokeo yake ni matumizi ya maneno mengi ambayo huvuruga maana iliyonuiwa na mwandishi. Kwa mfano:

103)* *Magazeti haya huwa na ilani au onyo ambazo humpa mwanafunzi ufaafu wa hatari za kutenda matendo na hali ya starehe, raha nyingi za dunia na....*

Sahihi: Magazeti huonya dhidi ya anasa za dunia na...

104)* *Magazeti humwezesha mwanafunzi kutambua misamiati ya maneno maalumu ambayo pengine vitabu anavyosoma hawezi kuyapata, maneno hayo kurahisisha mazungumzo yake...*

Sahihi: Magazeti hukuza msamiati wa mwanafunzi...

Kwa mfano katika (103), mwanafunzi ametumia maneno ishirini na matano (25) kufafanua hoja ambayo kama angeiandika vizuri ingetumia maneno manane (8) tu. Vilevile mwanafunzi katika (104), ametumia maneno kumi na tisa (19) kuwasilisha ujumbe wake badala ya kutumia maneno machache ambayo yangewasilisha ujumbe kwa njia rahisi na ya kueleweka kabisa.

3.3.3. Ukiukaji wa Sheria za Lugha Lengwa

Kwa mujibu wa Dulay na Burt (1974), makosa mengi hutokana na lugha hiyo na wala hayasababishwi na lugha ya pili. Kwa jumla inahusisha uumbaji wa miundo isiyofuata desturi katika nafasi ya muundo wa lugha ya pili (Kiswahili). Ukiukaji wa sheria za lugha uliojitokeza katika matini za watafitiwa ni: kuunganishwa kwa maneno na kutenganishwa kwa neno ambalo kwa kawaida halitenganishwi.

3.3.3.1 Kuunganishwa kwa Maneno

Wanafunzi huunda maneno yasiyofuata sheria kutokana na msingi wa maarifa ambayo wamejifunza au wamefunzwa mapema juu ya maneno katika lugha lengwa. Muungano wa maneno kama njia moja ya kuunda maneno mapya unakubalika katika lugha ya Kiswahili lakini watafitiwa wengine walikiuka sheria za kuyaunganisha maneno na kuzua maneno yasiyokubalika katika lugha ya Kiswahili. Makosa hayo huweza kusababishwa na uzembe wa baadhi ya wanafunzi wa kutosoma kwa mapana ili kuwa na umilisi wa maneno yanayostahili kuunganishwa na katika kiwango kipi. Pia kutomakinika kwa mwanafunzi hasa anapoandika kazi yake husababisha kuwepo kwa makosa husika. Kwa kiwango fulani kuandika kwa haraka kwa baadhi ya wanafunzi huwafanya kutoacha nafasi inayostahili kati ya neno moja na lingine. Matokeo yake ni kauli zilizo na utata kwa kuwa ujumbe haueleweki kwa sababu miungano hiyo haipo katika lugha ya Kiswahili. Maneno yafuatayo yaliunganishwa visivyo:

105)* *Magazeti huwapa wanafunzi hamu ya kujuazaidi kwa...*

Sahihi: Magazeti huwapa wanafunzi hamu ya kujua zaidi kwa...

106)* *Wanafunzi hupenda kusikizana kusoma magazeti ya...*

Sahihi: Wanafunzi hupenda kusikiza na kusoma magazeti ya...

107)* *Wanafunzi wasekondari husoma magazeti ili...*

Sahihi: Wanafunzi wa sekondari husoma magazeti ili...

Katika mifano (105-107), wanafunzi waliyaunganisha maneno ambayo hayaunganishwi na hivyo kutatiza mawasiliano. Mfano wa (105), mwanafunzi aliunganisha kitensi ‘**kujuu**’ na chagizo ‘**zaidi**’ na kuunda neno ambalo halisomeki wala kuwasilisha maana maalum. Vilevile katika (106), kitensi ‘**kusikiza**’ kimeunganishwa na kiunganishi ‘**na**’ na kuunda istilahi yenyе kasoro. Aidha, katika mfano wa (107), mwanafunzi alifanya kosa la kuunganisha kihuishi ‘**wa**’ (cha A unganifu) na nomino ‘**sekondari**’ na kuunda neno ambalo ni changamani.

3.3.3.2 Kugawanywa kwa Neno Visivyo

Tatizo hili la kugawanywa kwa neno moja na kuwa mawili katika maandishi ni kinyume cha kuunganishwa kwa maneno mawili na kuunda neno moja. Wanafunzi walikiuka sheria za lugha ya Kiswahili ambazo zinastahili kufuatwa wakati wa kuandika matini yoyote yale.

Kosa hili lilijitokeza katika baadhi ya matini za watafitiwa tulizochanganua na kutatiza ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Sababu ya kufanya hivyo ni uvivu wa wanafunzi wa kutosoma kwa mapana ili kufahamu sheria zinazofuatwa katika utenganishaji wa maneno na ni maneno yepi yanayostahili kutenganishwa. Kama asemavyo Katz (1986), maana ya neno au maneno yoyote yanayotumiwa katika utungaji au uandishi wa matini yoyote ile sharti yasheheni maana. Hivyo basi, mwanafunzi anapolitenganisha neno moja na kuwa mawili humtatiza msomaji zaidi kwa kuwa hakuna maneno ya aina hiyo katika lugha ya Kiswahili. Makosa haya yalipelekea kuwepo kwa istilahi zisizokubalikaka katika Kiswahili sanifu. Kwa mfano:

108)**Magazeti hutu elimisha kwa kutumia lugha...*

Sahihi: Magazeti hutuelimisha kwa kutumia lugha...

109)**Ninaposoma magazeti hunifanya ni na changanyi kiwe na...*

Sahihi: Ninachanganyikiwa nisimapo magazeti...

110)**Wanufaika kuto-kana na magazeti kwa...*

Sahihi: Wanufaika kutohana na magazeti kwa...

Kauli zilizotenganishwa (108-110), zilipelekea kuwepo kwa makosa ya kisemantiki kwa sababu neno ‘**hutu**’ na ‘**elimisha**’ hayawasilishi maana kamilifu katika kauli husika.

3.3.4 Athari za Lugha ya Kishairi

Wanafunzi wanapotumia lugha ya kishairi katika utungaji wa sentensi na uandishi wa matini huvuruga maana iliyonuiwa na mwandishi. Hivyo basi, mwanafunzi anastahili kutumia maneno ambayo yanaeleweka moja kwa moja. Katika utunzi wa mashairi, watunzi wana uhuru wa kutozingatia kanuni za lugha ya Kiswahili na hawawezi kulaumiwa kwamba wamekosea. Iwapo mwanafunzi ameathiriwa na lugha ya kishairi, matokeo ni sentensi zisizoleweka kwa urahisi. Matini tulizochunguza, zilionyesha hali ambayo baadhi ya wanafunzi walitumia lugha ya kishairi na kuwasilisha ujumbe kwa njia inayotatiza. Matumizi ya lugha ya kishairi yaliyojitokeza katika matini za watafitiwa ni kama: kuacha fonimu au kuongeza fonimu katika neno na kutofua mpangilio wa maneno katika sentensi.

3.3.4.1 Kuacha au Kuongeza Fonimu

Mwanafunzi aliyathiriwa na lugha ya kishairi na kupoteza maana na ujumbe uliokusudiwa. Katika lugha ya Kiswahili, fonimu ikiachwa katika neno au kuongezwa hupelekea kuwepo kwa istilahi isiyokubalika na isiyowasilisha maana kamilifu. Asemavyo MBAABU (1985), baadhi ya walimu hufunza mashairi bila kuwaelekeza kwamba ipo tofauti kati ya tungo hizi na Kiswahili sanifu. Wanawaacha wanafunzi katika hali isiyoelewaka na hatimaye kupelekea kuwepo na matini isiyoelewaka. Katika baadhi ya kazi za watafitiwa tulizochanganua, hali hii ilijitokeza na kusababisha kosa la kisemantiki. Mifano ifuatayo inadhihirisha mifanyiko hiyo:

111) Magazeti hutusaidia kujuwa yale...*

Sahibi: Magazeti hutusaidia kujua yale...

112) Hutujuza mambo yanayohusu afia...*

Sahibi: Hutujuza mambo yanayohusu afya

113) Wanafunzi taka kusoma magazeti ili...*

Sahibi: Wanafunzi wanataka kusoma magazeti ili...

114) Usomapo gazeti huelewa mahitaji ya familiyia...*

Sahibi: Usomapo gazeti huelewa mahitaji ya familia...

Mifano katika (111-114), inaonyesha kuwa watafitiwa waliathiriwa na lugha ya kishairi.

Mfano wa (111 na 112), mwanafunzi alitumia mbinu ya kishairi inayojulikana kama ‘tabdila’ ambayo ina maana ya kubadilisha mpangilio wa herufi au vitamkwa katika neno ili kupata ufanano (urari) wa vina vinavyotakikana. Katika (113), mbinu ya inkisari imetumiwa inayomaanisha hali ya kufupisha maneno fulani katika mashairi kwa madhumuni ya kupata idadi ya mizani inayohitajika au kupata ulingano fulani wa silabi hasa katika vina vya shairi. Katika (114), mwanafunzi alitumia mbinu ya mazda, ambayo ni kurefusha baadhi ya maneno kwa minajili ya kupata idadi ya mizani inayohitajika katika shairi lolote lile.

3.3.4.2 Kutofuata Mpangilio wa Maneno katika sentensi

Mwanafunzi kwa kutojua athari yake, anatumia mtindo wa kuandika shairi na kutatiza mawasiliano. Katika sentensi maneno yanastahili kupangwa kwa njia ambayo inaweza

kuleta maana kamili. Neno linapoachwa au mpangilio wa maneno usipozingatiwa, ujumbe unavurugika. James (1998:150), anaeleza kuwa makosa ya aina hii hutokana na athari ya uwili-lugha ama wingi-lugha wa mwanafunzi. Anaendelea kusema kuwa mpangilio huu mbaya wa maneno katika sentensi unahusishwa pia na njia ambazo mwanafunzi alipitia alipokuwa akikua. Katika ushairi mtunzi wa shairi ana uhuru wa kutofuata kanuni za Kiswahili sanifu na shairi lake halitakataliwa kwamba lina kasoro. Mifano ifuatayo inaashiria mpangilio wa maneno usiofaa katika sentensi:

115) Magazeti waandishi wanatumia lugha ya sanifu ya Kiswahilli...*

Sahihi: Waandishi wa magazeti wanatumia lugha sanifu ya Kiswahili.

116) Wanafunzi hupata unaostahili ujumbe wa...*

Sahihi: Wanafunzi hupata ujumbe unaostahili wa...

117) Katika ujumbe magazetini wanafunzi hufahamu vitu vingi vya...*

Sahihi: Wanafunzi hufahamu mambo mengi kutoka kwa magazeti.

Katika mifano (**115-117**), mpangilio wa maneno katika sentensi ulikiukwa kwa sababu ya athari ya lugha ya kishairi na kupelekea ujumbe kutoeleweka. (Mifano zaidi rejelea uchanganuzi wa makosa ya kisemantiki ukurasa wa 74).

3.3.5 Kuandika kwa Kasi

Mara nyingi makosa hutokea wakati wa kuandika kwa kasi kwa kuwa mawazo humjia mwanafunzi akilini kwa upesi. Kwa kuwa ni vigumu kuandika hivyo, kuna uwezekano wa kufanya makosa yanayopelekea kuwepo kwa ujumbe usioeleweka kwa uraisi. Kuandika kwa kasi huchangia makosa ya kisemantiki.

Katika lugha yoyote ile neno huwa ni mkusanyiko wa silabi zinazoweza kutamkika kama kitu kimoja au kuandikwa na kuleta maana fulani. Hivyo basi, neno lisiponakiliwa vizuri maana iliyokusudiwa haitamfikia aliyetarajiwa na hapatakuwepo na mawasiliano. Makosa haya hutokea kwa kuacha silabi moja au mbili katika neno. Kwa mfano:

118) Mag_{et}i yana umuhimu lakini wanafunzi hawa_{om}i.*

Sahihi: Magazeti yana umuhimu lakini wanafunzi hawasomi.

119) Ni v_yuri kusoma magazeti ili kubo_{es}ha lugha yetu.*

Sahihi: Ni vizuri kusoma magazeti ili kuboresha lugha yetu.

120 Magazeti yanaan ikwa kwa kuwa uza wanafunzi au watu yanayoendelea nchini.*

Sahihi: Magazeti yanaandikwa kwa kuwajuza wanafunzi au watu yanayoendelea nchini.

Kwa mujibu wa mifano hiyo (**118-120**) kuna ithibati tosha kuwa wanafunzi waliacha sauti moja au mbili katika baadhi ya maneno na kuzifanya kauli husika kuwa na utata katika uwasilishaji wa ujumbe. Katika (**118**) wanafunzi waliacha sauti (z) kwa neno magazeti na (s) kwa neno hawasomi. Vilevile katika (**119 na 120**) wanafunzi waliacha sauti (z), (r), (d) na (j) kwa maneno vizuri, kuboresha, yaanaandikwa na kuwajuza mtawala. Kauli hizo zilikuwa na dosari. Ujumbe haukueleweka na msomaji.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wenyewe walichangia makosa yaliyojitokeza katika utafiti huu. Licha ya kuwa, baadhi ya shule hazina vitabu vya hadithi katika lugha ya Kiswahil ila vya lugha ya Kiingereza, wanafunzi wengine ni wavivu. Hawana wakati wa kusoma vitabu zaidi ya vile vilivyoidhinishwa na Wizara ya Elimu na matokeo yake ni kuwa na msamiati finyu. Wengine hukariri maneno kikasuku pasi kujua maana yake na baadaye kuyatumia katika uandishi wao na kupelekea kuwepo kwa makosa ya kisemantiki yanayotokana na utumiaji wa msamiati usiofaa katika muktadha na kuvuruga maana iliyokusudiwa.

Aidha, wanafunzi wengine huwa na msamiati bora lakini wanashindwa kuutumia vilivyo katika sentensi. Baadhi ya wanafunzi wanaposoma vitabu hujiburudisha tu wakati ambapo hawana kazi ya kufanya. Huwa hawazingatii matumizi ya maneno na miundo ya sentensi iliyotumiwa na mwandishi.

Baadhi ya walimu wa Kiswahili hawana tajriba ya ufunzaji wa lugha ya Kiswahili. Wengi huegemea katika ufunzaji wa karatasi ya tatu (fasih) na kuacha sehemu ya matumizi ya lugha (Sarufi) ambayo ni nguzo muhimu katika ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Hali hii huwafanya wanafunzi kutumia lugha ya kishairi katika uandishi wa insha.

Isitoshe, baadhi ya wasimamizi wa shule za upili huchangia pakubwa makosa ya kisemantiki. Wanafunzi mara nyingi hawaruhusiwi kutumia lugha ya Kiswahili shulenii isipokuwa wakati wa somo la Kiswahili katika mazingira ya darasani. Adhabu kali

hutolewa kwa wanafunzi wanaopatikana wakizungumza lugha ya Kiswahili shulenii. Hali hii inawatia wanafunzi wahaka. Pia kuna uhaba wa vitabu vya Kiswahili hususani vya hadithi katika baadhi ya shule ikilinganishwa na vya lugha ya Kiingereza. Magazeti mengi yanayonunuliwa ni ya lugha ya Kiingereza tu. Hali hii inawafanya wanafunzi kudharau lugha ya Kiswahili na kuthamini lugha ya Kiingereza, na matokeo yake ni makosa mengi ya kisemantiki kujitokeza wanapoandika matini zao.

3.6 Hitimisho

Makosa mbalimbali ya kisemantiki yalitambuliwa, yakaainishwa na kuchanganuliwa kwa kina katika utafiti huu. Makosa hayo ni matumizi ya sheng'; mrundiko wa maneno katika sentensi; ufanuzi uliokithiri; kuongeza sauti visivyo katika neno; matumizi ya lugha ya kishairi; kuacha neno katika sentensi; kutengenisha neno visivyo; matumizi ya msamiati usiofaa katika muktadha; kuacha sauti katika neno; kubadilisha mpangilio wa fonimu katika neno na kuunganisha maneno visivyo. Umaratokezi wa kila kosa ulionyeshwa katika jedwali 2 (ukurasa wa 44). Illobainika kuwa tapo la utumiaji wa msamiati usiofaa ndilo likuwa na idadi kubwa ya makosa 110, ambayo ni asilimia 14.7. Tapo la ubadilishanaji nafasi wa fonimu katika neno ndilo likuwa na idadi ndogo ya makosa 17 ambayo ni sawa na 2.3. Hii ni ishara kuwa watafitiwa walikuwa na changamoto kubwa katika tapo hilo la kwanza.

Pia, katika sura hii tumeshughulikia vyanzo vya makosa ya kisemantiki yaliyojitokeza katika matini tulizochanganua. Tuligundua kuwa ni vigumu kuamua kwamba hali au kosa fulani hutokana na sababu maalumu kwa kuwa kosa moja linaweza kusababishwa na mambo mengine mengi. Vyanzo hivyo ni pamoja na: athari ya lugha ya sheng; athari ya lugha ya kwanza; ukiukaji wa kanuni za lugha lengwa na athari ya lugha ya kishairi.

SURA YA NNE

MBINU ZA KUPUNGUZA UTOKEAJI WA MAKOSA YA KISEMANTIKI

4.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa Cann (1983), vikwazo vinavyotinga mawasiliano ya Kiswahili ni vingi na vinazidi kupata nguvu. Ni muhimu basi kuweka mikakati kabambe ya kuimarisha Kiswahili. Makosa yanapotokea katika matini za wanafunzi huwa tatizo kubwa kwa walimu wa Kiswahili kwa jumla. Mapendekezo yafuatayo yanatokana na matokeo ya uchanganuzi wa matini za wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu.

4.2 Matumizi ya Lughya ya Kiswahili

Lughya hupitisha ujumbe kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa njia ya maandishi na mazungumzo. Wanafunzi hujua lughya kuitia maingiliano yao wenyewe kwa kubadilishana mawazo na kuchagua maneno yanayofaa kutumiwa katika muktadha. Asemavyo Ontieri (2010:141), mwanafunzi ana jukumu kubwa la kutekeleza katika juhudzi za kupunguza utokeaji wa makosa katika matini anayoandika. Usikivu na ushirikiano na mwalimu wake wa Kiswahili ni kati ya mambo makuu ambayo huweza kuchangia uboreshaji wa uandishi. Mwanafunzi anashauriwa kudurusu kazi yake baada ya kuiandika, ili kurekebisha makosa yanayodhihirika katika uandishi wake. Mwanafunzi anapaswa kuchunguza makosa ambayo hutokea mara kwa mara aandikapo kwa kutilia maanani vipengele ambavyo hukwamiza uelewekaji wa ujumbe wake.

Mara nyingi makosa mengi hutokea wakati wa kuandika kwa haraka kwa kuwa mawazo humjia mwanafunzi akilini kwa upesi. Kwa kuwa ni vigumu kuandika hivyo, kunao uwezekano wa kufanya makosa yanayopelekea kuwepo kwa ujumbe usioeleweka kwa urahisi. Makosa ya aina hii yanaweza kurekebishwa kwa urahisi. Mwanafunzi aliyeandika insha yenye aina hii ya makosa angweza kuyasahihisha mengi ya makosa hayo ikiwa angeisoma kazi yake amalizapo kuiandika.

Kwa mujibu wa Nurse (1986), njia bora ya kukuza au kuboresha msamiati ni kusoma vitabu vingi vya Kiswahili. Vilevile ingekuwa bora zaidi iwapo kila mwanafunzi atakuwa

na kamusi ili kutafuta maana za maneno magumu anayoyapata katika usomaji wake. Mwanafunzi akizoea hivyo, atakuwa na maneno mengi ya kutumia anapoyahitaji. Ajiepushe na kosa la kuhamisha mawazo yake moja kwa moja kutokana na lugha nyingine anazozijua kama vile lugha ya kwanza na lugha ya Kiingereza. Mwanafunzi aandike sentensi fupi zinazolelewaka kwa kuwa kuandika sentensi ndefu kunaongeza uwezekano wa kufanya makosa ya kuchanganya viambishi na pengine kupotosha maana.

4.3 Njia za Ufundishaji

Katika uchanganuzi wa kazi za watafitiwa walioshiriki katika utafiti huu, makosa mengi yaliyojitekeza yalionyesha kuwa watafitiwa hawakuwa na umilisi wa mambo ya kimsingi katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu unapendekeza kwamba wanafunzi wanahitaji kufundishwa jinsi ya kutamka maneno yanayowakanganya na kuyaandika katika daftari kwa sababu baadhi ya wanafunzi hujifunza maneno kwa haraka ilhali wengine huwa na shida ya kuyatamka na kuyaandika baadhi ya maneno. Walimu wamakinike katika miundo ya kimsingi hasa msamiati na maendelezi ili wanafunzi nao wamakinike katika uandishi wao. Walimu wawe waangalifu wanapofundisha aina za maneno na matumizi yao katika sentensi ili kuimarisha utumiaji wao katika muktadha kwa njia mwafaka. Jedwali lifuatalo linaonyesha aina za maneno katika lugha ya Kiswahili ambayo yanatarajiwa kutiliwa mkazo katika ufundishaji:

Jedwali: 5 Aina za maneno

AINA	MIFANO
Nomino	Kisumu, mwalimu, wema, warsha ya Kiswahili, maziwa na kuimba
Vivumishi	Mwenye, wengi, kifalme, nadhifu, wangu, yuyu huyu, wangapi naambaye
Viwakilishi	Mimi, yule, papo hapo, kwetu, werevu, zipi, mengi, wenyewe, wa, na amacho
Vitenzi	Anawaimbia, anasoma, walikuwa, ni, anaimba, akicheza.
Vielezi	Salama, kifahari, anaonjaonja, ovyo, chururu, kwa, kesho,milele, mara kumi n.k
Vihuishi	Tangu, vya, katikati ya, kuliko, kwa kuwa, na, n.k
Viunganishi	Pamoja na, ijapokuwa, kisha, kwa sababu, ama, ila, wala, basi, kwa kuwa n.k
Vihisishi	Masalale!, Aka!, Ebo!, Kumbe!, Jamani!, Maskini!, Nabii!, Alla!, Kefule!, Eee!, n.k

Asili: Mtafiti (2016)

Kwa hivyo, walimu wahakikishe kila mwanafunzi ana umilisi wa aina za maneno hayo ili kusiwe po na mirundiko ya maneno katika sentensi. Hili litafanikiwa iwapo walimu watawapa wanafunzi kazi nyingi zaidi ya ile ambayo wanafanya darasani ili kuzamia maktabani kutafuta majibu wakati wao wa ziada. Kwa kufanya hivyo watakuwa na ari ya kusoma vitabu vingi vya Kiswahili na baadaye watafahamu mpangilio mwafaka wa maneno katika sentensi

Pia, walimu wa Kiswahili wanahimizwa kuanzisha zoezi la kuandika kwa wanafunzi na kuwahamasisha kuandika mara nyingi ili kukuza lugha ya Kiswahili kimaandishi. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba wanafunzi hawafanyi mazoezi mengi ya kuandika insha. Kwa hivyo, wanafunzi wahimizwe kuandika darasani, nyumbani na katika majarida. Wapewe insha ambazo mada zao zinaleweka wazi au zenye wanapenda au wana uzoefu

nazo ili waandike kuzihusu. Sheria za uandishi wa insha zifafanuliwe kwa minajili ya uandishi mwafaka na kupunguza makosa yanayovuruga ujumbe ulionuiwa na mwandishi. Mwalimu asisitize umuhimu wa kusahihisha makosa yanayovuruga maana lengwa. Wazazi wawanunulie watoto wao vitabu vya kusoma na kuandika na walimu wanapaswa kuwahimiza kuvisoma vitabu vingi vya Kiswahili. Hii itawafanya wanafunzi kuwa wabunifu katika uandishi wao wa Kiswahili na kupunguza utokeaji wa makosa ya kisemantiki katika siku za baadaye.

Walimu wa Kiswahili wasijitenge katika ufundishaji wa Kiswahili bali washirikiane na wenzao kusisitiza usahihi mionganini mwa wanafunzi. Walimu wanafaa kuwasaidia wanafunzi katika kukuza msamiati wao katika lugha ya Kiswahili kwa kuhamamasisha wanafunzi kujadiliana ili kukuza mazungumzo yao ambayo yana dhima kubwa katika maandishi. Wawape wanafunzi fursa ya kutumia lugha ya Kiswahili gwarideni na darasani kwenye majadiliano ambapo walimu wa masomo mengine huhudhuria ili kuwasaidia kuelewa sheria za lugha ya Kiswahili. Hii itawafanya kumakinika na kujikosoa au kukosolewa na wanafunzi wengine, na hivyo kupunguza makosa ya kisemantiki katika uandishi wao. Katika mijadala, walimu wawahimize wanafunzi kufikiria kwanza kwa lugha ya Kiswahili na wawasadie kufanya hivyo, ndiposa wanafunzi wasipate fursa ya kutafsiri mawazo yao ya lugha ya kwanza kwa Kiswahili ili tuepukane na makosa yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza. Hili litafanikiwa iwapo walimu watashirikiana na wanafunzi kuboresha lugha ya Kiswahili kwa kuyarekebisha makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika mawasiliano yao ya kila siku.

Aidha, walimu wasionyeshe makosa tu katika matini za wanafunzi bali wawaeleze wanafunzi sababu zilizopelekea kauli husika kuwa kosa na wawaelekeze namna ya kuepukana na kosa lenyewe katika uandishi wao. Hili litatendeka kwa kuwahimiza wanafunzi kutumia kamusi kwa maneno ambayo hawana uhakika nayo ili kuzuia utokeaji wa makosa ya kisemantiki kwa kutumia msamiati usiofaa katika muktadha.

Vilevile walimu wabuni mbinu mbalimbali za ufundishaji ili wanafunzi waweze kufahamu vipengele mbalimbali vya kuzingatiwa katika uandishi wa insha. Kwa mfano, walimu watumie mbinu ya kuwaweka wanafunzi katika makundi mbalimbali na kuwapatia mada

ya kushughulikia kama kundi. Hatimaye watakapokuwa tayari katika uwasilishaji kwa wanafunzi wengine darasani, watalazimika kuwasilisha kwa lugha ya Kiswahili badala ya lugha zao za kwanza. Kosa litakapojojitekeza katika mawasiliano yao, wanaweza kukosoana wao kwa wao. Pia, katika harakati hiyo ya uwasilishaji mwalimu atayaandika makosa yatakayojitekeza na baadaye kuyajadili pamoja na wanafunzi ili wasiyarudie katika uandishi wao wa insha.

Walimu wawahimize wanafunzi kutumia lugha ya Kiswahili katika mazingira ya darasani na nje ya darasa, kama vile katika mijadala na michezo ya kuigiza ambapo kuna hali halisi ya kubuni baadhi ya matendo. Wakati wanafunzi wanapoigiza wanajifunza namna ya kuzungumza kwa ufasaha kwa kueleza mawazo yao kwa njia iliyowazi na hali hii huimarisha uandishi wao wa insha. Hivyo basi, walimu wanaweza kutumia njia ya kuigiza katika kurekebisha matumizi ya lugha ya wanafunzi wakati wa kufundisha masuala yanayohitaji kuigizwa kama vile Fasihi Simulizi

4.4 Mafunzo ya Kujikumbusha kwa Walimu wa Kiswahili

Uandishi wa insha hauwezi kuimarika hivi hivi tu, unahitaji walimu hodari na wataalamu wenye maarifa ya hali ya juu wa kuyashughulikia. Ni muhimu basi mafunzo ya walimu na wasomi wa lugha ya Kiswahili yawe ya kiwango cha juu. Haya yanaweza kutekelezwa kwa kuhakikisha wanafunzi wanaosomea Kiswahili katika vyuo vya elimu ya juu wamefundishwa vizuri. Hii itasaidia kuwaelekeza wanafunzi kuandika insha bora.

Aidha, ili kuimarika katika ufundishaji wa insha na ujuzi wa uandishi, kuna haja ya walimu wa Kiswahili kushiriki katika shughuli za kitaaluma kama semina, katika jopo la walimu wanaofundisha Kiswahili na kozi za kujikumbusha. Kushiriki kwa walimu kwenye shughuli za kitaaluma huwahamasisha juu ya shida wanazopitia wanapofundisha na vile wanaweza kutafuta njia mwafaka za kukabiliana nazo darasani. Kushiriki huku kunawasaidia kutangamana na wataalamu mbalimbali katika eneo hili la kufunza lugha na kusaidia walimu kubuni mikakati muhimu ya kufunza Kiswahili kama somo na kama lugha ya pili kwa baadhi ya wanafunzi.

4.5 Uandishi wa Mashairi

Katika uchanganuzi wa matini za watafitiwa, mtafiti aligundua kuwa baadhi yao walitumia lugha ya kishairi ambayo ilipelekea kuwepo kwa makosa ya kisemantiki. Watunzi wa mashairi wahimizwe kuandika mashairi katika Kiswahili sanifu pasipo kutumia uhuru walio nao wa kutunga mashairi yasiyolewaka. Asemavyo Nabhany (1987), ni ukweli usioweza kukanushika kwamba mashairi yanaweza kuandikwa kwa Kiswahili pasipo kutumia maneno ya Kiamu, Kimvita au lahaja yoyote ile. Huenda uchunguzi zaidi wa vitabu vya mashairi ukahitajika siku zijazo ili kuhakikisha kwamba katika shule za msingi na za sekondari wanafunzi wanasoma mashairi yale tu yaliyoandikwa katika Kiswahili sanifu. Nabhany (1987), anaendelea kusema kuwa ingawa lugha hubadilika kila mara, mabadiliko hayo hujitokeza sana katika lugha ya maongezi kuliko lugha ya maandishi. Baada ya lugha kusanifishwa, lugha ya maandishi huhimili mabadiliko na hudumu kwa miaka na pengine karne nyingi. Kwa hivyo hatuna haki ya kuigeuza lahaja ya maandishi ya Kiswahili kwa uvivu wetu wa kuiandika lugha kutegemea vile lafudhi zetu zinavyobadilika licha ya vile zinavyotofautiana. Inafaa ieleweke kwamba, kuwa na ujuzi wa lugha ya kwanza haimaanishi kwamba mtu hahitaji kujifunza lugha sanifu. Watu wengi kote ulimwenguni huenda shule kujifunza lugha zao. Ni muhimu wale wenye kutumia Kiswahili tangu kuzaliwa kwao wajifunze Kiswahili sanifu ili lahaja zao zisiwe pingamizi katika mawasiliano yao kimaandishi.

4.6 Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala Nchini Kenya

Kwa mujibu wa Michira (2000), Taasisi hii ndiyo inayoidhinisha vitabu vinavyotumiwa katika shule za msingi na za sekondari. Taasisi husika kuchunguza vitabu vya Kiswahili vinavyouzwa madukani na kutumiwa katika suala zima la ufundishaji ili kutathmini kiwango cha msamiati unaotumiwa na waandishi. Kamusi ifanyiwe marekebisho kwa kuwa baadhi ya maneno huwa na maana isiyokisi ukweli wa neno. Ili kudhibiti sheng, ni muhimu sera mpya ya Kiswahili iliyomadhubuti na inayochukuana na hali ya sasa, ibuniwe. Sera hii yapasa ibainishe nyanja mpya na maeneo ya matumizi ya Kiswahili pamoja na hatua za kuchukuliwa dhidi ya wale wanaokaidi sera husika.

Sarufi ndiyo uti wa mgongo wa lugha. Vijana washauriwe kuhusu umuhimu wa kuzungumza Kiswahili sanifu. Kuna haja ya kuweka utaratibu wa matumizi ya kuzingatiwa na wanaotumia lugha ya Kiswahili katika vyombo vya habari, sanaa, muziki, mikutano na mawasiliano rasmi. Hivyo basi, viongozi wawe katika mstari wa mbele kutumia Kiswahili sanifu na kuhimiza matumizi yake. Pia, pawepo na mashindano ya uandishi na uzungumzaji wa Kiswahili mionganoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Mwisho kabisa, serikali iunde Taasisi inayochunguza lugha inayotumiwa katika majarida na magazeti ili wanafunzi wanaposoma waweze kukuza msamiati wao.

4.7 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amefafanua mbinu mbalimbali ambazo zinaweza kuzingatiwa ili kusaidia katika upunguzaji wa makosa ya kisemantiki katika matini za wanafunzi wa shule za upili. Mbinu hizo ni pamoja na: matumizi ya lugha ya Kiswahili, njia za ufundishaji, mafunzo ya kujikumbusha kwa walimu wa Kiswahili, uandishi wa mashairi na uwajibikaji wa Taasisi ya ukuzaji wa mitaala nchini.

SARA YA TANO

MUHTASARI, MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa utafiti huu, kulingana na malengo, maswali ya utafiti, mapendekezo na kubainisha sehemu ambazo zinaweza kushughulikiwa katika tafiti za baadaye.

5.2 Muhtasari

Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchanganua makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika matini za watafitiwa mia moja ishirini wa shule za upili, katika kaunti ya Kakamega.

Sura ya kwanza imechambua misingi ya utafiti huu. Mbali na kuchanganua kwa kina dhima ya mawasiliano katika jamii, imeanganzia makosa ambayo yanapelekea ujumbe kutoeleweka kwa walionuiwa. Suala la utafiti huu lilibainishwa na malengo ya utafiti huu kuorodheshwa. Nayo ni:

1. Kuchanganua makosa ya kisemantiki katika matini za wanafunzi wa shule za upili.
2. Kujadili vyanzo mbalimbali vya makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili.
3. Kupendekeza mbinu za kupunguza utokeaji wa makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili.

Aidha, tumeonyesha maswali yanayoongoza utafiti huu ambayo ni pamoja na;

1. Je, kuna makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika matini za wanafunzi wa shule za upili?
2. Je, vyanzo vya makosa ya kisemantiki yanayojitokeza katika matini za wanafunzi husababishwa na ukiukaji wa sheria za kiisimu?
3. Je, makosa ya kisemantiki katika matini za wanafunzi yatapunguzwaje?

Aidha, katika sura hii ya kwanza vilevile, tumbainisha upeo na mipaka ya utafiti, eneo la utafiti na sababu zilizopelekea kuchaguliwa kwa mada hii zimeorodheshwa wazi. Pia, umuhimu wa utafiti huu kwa walimu wa Kiswahili, wanafunzi na wanajamii kwa jumla umedhihirishwa. Nadharia ambazo ziliongoza utafiti huu (Nadharia ya Uchanganuzi Makosa pamoja na Nadharia ya Sarufi Zalishi) zilifafanuliwa na dhima yao katika kufanikisha utafiti huu kuangaziwa kwa kina. Katika sura ya kwanza tuliangazia eneo la utafiti, wahusika lengwa, mbinu ya uteuzi wa sampuli na vifaa vyta utafiti viliviyotumiwa (hojaji na mjarabu) ili kufanikisha utafiti huu. Pia, mbinu zilizosaidia katika ukusanyaji wa data zilizotuwezesha kutolea maamuzi ya utafiti huu na uchanganuzi wa data zimeangaziwa kwa kina.

Katika sura ya pili, tumefafanua maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu maana na taaluma ya semantiki ambayo yalitusaidia katika uchanganuzi wa data iliyofanikisha utafiti huu. Aidha, katika sura hii tumeangazia mapitio ya wasomi mbalimbali ambayo yalikuwa na ukuruba na utafiti huu. Wasomi mbalimbali wameonyesha namna ambavyo lugha za kwanza za watafitiwa zinavyotinga ujifunzaji wa lugha ya pili. Wengine wamechangangua makosa kwa kuangazia lugha mbalimbali kama vile Kiarabu, Kigisu, Cinamwanga, Ekegusii, Kijapani, Kinyala, na kadhalika. Pia, tulianganzia wataalamu waliochangangua vyanzo vyta makosa mbalimbali kwa lugha lengwa na waliojihuisha na athari za lugha mbalimbali katika lugha ya Kiingereza. Kupitia kwa mapitio ya wataalamu hao, tuligundua kwamba makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi hayajashughulikiwa, suala ambalo utafiti huu ulizamia.

Sura ya tatu, inahusu uchanganuzi wa data ya utafiti huu. Tumeyaainisha makosa kumi na moja ya kisemantiki yaliyojitekeza katika insha za watafitiwa. Tuligundua makosa yanayotokana na matumizi ya msimbo wa sheng kwa baadhi ya watafitiwa ambao ni wazaliwa wa kaunti ya Kakamega lakini walihamia mijini na wale ambao mahali pa kuzaliwa ni mjini na wanaishi mjini. Kutohakana na kutangamana na wanafunzi, wengine wameathiriwa hadi kiwango cha kuhamisha msimbo huu kutoka mazungumzo hadi maandishi. Mrundiko wa maneno katika sentensi ulijitonekeza katika baadhi ya insha za watafitiwa, kwa kutohakana na umilisi wa viambajengo vyta sentensi na utaratibu wa mpangilio wa maneno katika lugha ya Kiswahili. Pia, tuligundua kwamba watafitiwa

walitanua msamiati wa neno katika lugha ya pili na kupanua msamiati wa neno alilo nalo ili kukabiliana na hali iliyomtatiza na kuathiri ujumbe uliokusudiwa. Aidha, baadhi ya watafitiwa walitumia sauti moja mahali palihitajika sauti nyingine tofauti. Sauti zilizobadilishwa zilikuwa na sifa sawa. Kulikuwa na makosa yaliyotokana na matumizi ya lugha ya kishairi kwa baadhi ya watafitiwa. Lugha ya kishairi iliyotumiwa ni inkisari, mazda, tabdila, utohozi na kubananga sarufi ya Kiswahili.

Makosa mengine yaliyojitokeza ni kuacha neno katika sentensi. Maneno yaliyoachwa ni nomino, vitenzi na vihusishi na hivyo kuathiri mawasiliano. Isitoshe, tuligundua makosa ya kutenganishwa na kuunganishwa kwa baadhi ya maneno. Watafitiwa walitatizika na maneno yaliyokuwa na viambishi vyta ‘o’ rejeshi na yale ambayo ni mrefu sana. Watafitiwa wengine waliyaunganisha maneno mawili hadi matatu, kwa mfano nomino na kivumishi, kiunganishi na nomino au kitenzi na kielezi na kuunda istilahi zenyekasoro. Matumizi ya msamiati usiofaa uliathiri mawasiliano. Baadhi ya watafitiwa walitatizwa na maneno yaliyokaribiana kimaana na yale yanayokaribiana kimatamshi lakini yana maana tofauti. Tuligundua kwamba watafitiwa waliacha sauti katika baadhi ya maneno na sauti (**h**) iliachwa katika maneno mengi hasa katika mwanzo wa maneno husika. Aidha, watafitiwa walibadilisha mpangilio wa sauti katika neno na kupelekea kuwepo kwa makosa ya kisemantiki.

Pia, sura hii inaangazia vyanzo vyta makosa yaliyojitokeza katika matini za watafitiwa tuliyochanganua. Vyanzo hivyo ni pamoja na: athari ya msimbo wa sheng. Athari hii ilidhihirika kupitia uundaji wa maneno yasiyoleweka kwa baadhi ya watafitiwa ilhali wengine waliyafupisha maneno. Pia, walichanganya viambishi vyta Kiswahili na mzizi wa lugha ya Kiingereza. Makosa mengine yalitokana na athari ya lugha za kwanza za watafitiwa. Athari hii ilipelekea kuwepo kwa makosa mengi ya kisemantiki. Kwa mfano kulikuwa na mrundiko wa maneno katika sentensi, kuachwa kwa sauti katika neno, kutumia sauti isiyofaa katika neno, uteuzi wa msamiati usiofaa na ufanuzi uliokithiri. Aidha, watafitiwa waliazima ruwaza kutoka lugha ya kwanza na kutanua ruwaza katika lugha ya pili. Pia, makosa yanayotokana na ukiukaji wa sheria za lugha ya Kiswahili yalitambuliwa. Makosa ya kuunganishwa kwa maneno mawili hadi matatu ili kuunda istilahi moja, kutenganishwa kwa neno moja kuwa mawili hadi matatu yalijitokeza katika

baadhi ya matini za watafitiwa. Makosa mengine yalitokana na athari ya lugha ya kishairi kama vile kuongezwa au kuachwa kwa sauti katika baadhi ya maneno na kutofuata mpangilio wa maneno katika sentensi na ujumbe kuvurugika.

Sura ya nne imejikita katika mbinu mwafaka za kupunguza utokeaji wa makosa ya kisemantiki yaliyochanganuliwa katika matini za watafitiwa. Mbinu hizo ni pamoja na: Kwanza, matumizi ya lugha ya Kiswahili. Mwanafunzi anahimizwa kutumia Kiswahili sanifu katika mazingira ya darasani na nje ya darasa. Asome vitabu vingi vya Kiswahili ili kuboresha msamati wake katika uandishi wake. Pili, njia ya ufundishaji. Walimu wabuni mbinu mpya za ufundishaji kwa kuwapa wanafunzi kazi nyingi za kufanya wakiwa nyumbani. Kuwagawa wanafunzi katika makundi mbalimbali na kuwapa mada inayoeleweka kuishughulikia na hatimaye kuiwasilisha darasani. Walimu wa Kiswahili washirikiane na walimu wengine na wamakinike katika usahihishaji wa matini za watafitiwa. Aidha, walimu wa Kiswahili wapatiwe mafunzo ya kujikumbusha kwa kushiriki katika shughuli za kitaaluma na kubadilishana mawazo. Waandishi wa mashairi wanaweza kupunguza utokeaji wa makosa ya kisemantiki kwa kutunga mashairi kwa Kiswahili sanifu. Taasisi ya ukuzaji wa mitaala nchini Kenya itasaidia kupunguza makosa ya kisemantiki kwa kutathmini kiwango cha msamati unaotumiwa katika vitabu vilivyoidhinishwa na kutumiwa katika suala zima la ufundishaji. Pia kubuniwe sera inayodhibiti matumizi ya lugha ya Kiswahili.

5.3 Matokeo

Matokeo yafuatayo yalitimiza malengo ya utafiti huu. Malengo hayo ni;

5.3.1 Kutambulisha Makosa ya Kisemantiki katika Matini za Wanafunzi wa Shule za Upili.

Lengo hili lilitimizwa kwa kuweka bayana makosa yaliyotambuliwa katika matini za wanafunzi. Makosa hayo ni:

- i. Matumizi ya Sheng

Makosa haya yalidhihirika katika baadhi za matini za wanafunzi. Kosa hili lilichangwa na ukopaji, utohozi, kubuni maneno kinasibu na uambishaji wa kiambishi ‘ku’ kwa mzizi wa vitenzi na ‘–sh’ au ‘–s’ kwa majina halisi ya mahali na watu.

ii Mrundiko wa maneno katika sentensi

Baadhi ya wanafunzi hawakuzingatia utaratibu wa kuunda sentensi zilizosheheni maana. Mpangilio wa upatanisho wa kisarufi ulikiukwa.

iii. Ufafanuzi uliokithiri

Kosa hili lilitokea wakati wanafunzi walipojaribu kujieleza kwa lugha ya Kiswahili kutokana na mawazo ya lugha ya kwanza. Baadhi ya wanafunzi walihamisha maana ya neno kutoka lugha ya kwanza hadi lugha anayojifunza kwa sababu ya upanuzi wa maana.

iv. Kutumia sauti isiyofaa katika neno

Utumiaji wa sauti isiyofaa uliwatatiza baadhi ya wanafunzi. Sauti zilizowatatiza kwa wingi ni [r] na [l]; [b] na [p]; [s] na [z]; [f] na [v]; [g] na [k], [t] na [d]. Hizi ni sauti zilizoaminika kuwa na ukuruba katika sifa za kifonetiki.

v. Matumizi ya lugha ya kishairi

Mtafiti aligundua kuwa uhuru wa kishairi ultumiwa na baadhi ya wanafunzi. Hali hii ilivuruga mpangilio wa maneno au sauti unaokubaliwa na wanaisimu. Mbinu za inksari, mazda, tabdila, utohozi na kuboronga sarufi zilitumiwa na kuzalisha sentensi zisizosheheni maana.

vi. Kuacha neno katika sentensi

Udondoshaji wa neno au maneno yaliyostahili kuwepo katika sentensi ulionekana kwa baadhi za matini za wanafunzi. Maneno yaliyodondoshwa zaidi yalikuwa ni nomino, viunganishi na vihusishi.

vii. Kutenganisha na kuunganisha maneno

Utafiti huu uligundua kuwa nomino, virejeshi, viambishi awali na mizizi vilitengwa na kujisimamia kama maneno kamili katika sentensi. Hali hii ilisababisha dosari. Baadhi ya wanafunzi hukisia kuwa matumizi ya ‘o’ rejeshi huonyesha maneno yaliyo tofauti na hayapaswi kuunganishwa. Kinyume cha kosa hili ilidhihirika kupitia kwa uunganishaji wa baadhi ya maneno visivyo na kuunda istilahi zisizokubalika. Uunganishaji wa maneno uliojitokeza ni wa kiunganishi na kitenzi, nomino na kihuishi, na nomino na kivumishi.

viii. Matumizi ya msamiati usiofaa

Mtafiti aligundua kuwa maneno ambayo ni vitate au yaliyo na ukuruba wa kimaana yalitumiwa na watafitiwa bila kugundua kuwa wamefanya kosa. Maneno hayo ni kama, [kusika badala ya kuvua]; [nguvu badala ya bidii]; [gari badala ya ghali], na [jenga badala ya kuza].

ix. Kuacha sauti katika neno

Kosa hili lilijitokeza katika maneno yaliyo na sauti mwambatano. Sauti zilizodondoshwa na baadhi ya watafitiwa ni kama vile, [m], [n], [h], na [w].

x. Kubadilisha mpangilio wa fonimu katika neno.

Katika matini za wanafunzi tulizochangazua tuligundua kuwa baadhi yao walibadilisha mpangilio wa fonimu katika baadhi ya maneno. Baadhi ya fonimu zilizobadilishwa ni kama vile, [s], [z],[r], [e], [i], [r], na [g].

5.3.2 Kufafanua Vyanzo vya Makosa Yaliyotambuliwa

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kufafanua vyanzo vya makosa yaliyotambuliwa. Vyanzo hivyo ni pamoja na:

- i) Athari ya msimbo wa sheng

Tuligundua kuwa baadhi ya watafitiwa waliathiriwa na msimbo huu wa sheng. Walitumia baadhi ya misamiati ya sheng katika utungaji wa sentensi na uandishi wa matini zao.

ii) Kuna makosa yaliyotokana na athari ya lugha za kwanza za watafitiwa.

Makosa hayo ni pamoja na: mrundiko wa maneno katika sentensi; kutumia fonimu isiyofaa katika neno; uteuzi wa msamiati usiofaa na ufanuzi uliokithiri.

iii) Ukiukaji wa sheria za lugha lengwa

Katika kipengele hiki mtafiti aligundua makosa ya kutenganishwa kwa baadhi ya maneno visivyo na kwa upande mwingine kuyaunganisha maneno ambayo kwa kawaida hayaunganishwi,

iv) Athari ya lugha ya kishairi

Baadhi ya watafitiwa waliathiriwa na idhini iliyopo katika uandishi wa mashairi. Makosa hayo ni, kuacha fonimu katika baadhi ya maneno na kutofufata mpangilio wa maneno katika sentensi.

v) Kuandika kwa haraka

Hali hii ilichangia udondoshaji wa sauti, kuunganishwa na kutenganishwa kwa baadhi ya maneno katika matini za watafitiwa.

5.3.3 Mbinu za Kupunguza Utokeaji wa Makosa ya Kisemantiki Yaliyotambuliwa

Hili ndilo lengo la tatu la utafiti huu. Mapendekezo yafuatayo yanatokana na matokeo ya uchunguzi wa matini za wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu.

I. Matumizi ya lugha ya Kiswahili

Wanafunzi hujua lugha kupitia maingiliano yao wenyewe kwa kubadilishana mawazo. Pia kwa kuchangua maneno yanayofaa katika muktadha. Wanafunzi waelezwe umuhimu wa kuzungumza lugha ya Kiswahili, wasome vitabu vingi vya lugha ya Kiswahili na wadurusu kazi zao baada ya kuziandika ili kuzirekebisha.

II. Njia za ufundishaji

Walimu wa Kiswahili wawe waangalifu wanapofundisha aina za maneno. Wahimizie wanafunzi kuandika insha kwa wingi ili kukuza lugha ya Kiswahili kimaandishi. Wabuni mbinu mbalimbali za ufundishaji na watilie mkazo vipengele muhimu vya kuzingatiwa katika uandishi wa insha.

III. Mafunzo ya kujikumbusha

Mafunzo ya walimu wa Kiswahili na wasomi wa lugha ya Kiswahili yawe ya kiwango cha juu. Walimu wa Kiswahili kushiriki katika shughuli za kitaaluma kama semina, katika jopo la walimu wanaofundisha Kiswahili na kozi za kujikumbusha.

IV. Uandishi wa mashairi

Watunzi wa mashairi wahimizwe kuuandika katika Kiswahili sanifu pasipo kutumia uhuru walio nao wa kutunga mashairi yasiyoeleweka kwa urahisi.

V. Taasisi ya ukuzaji mitaala nchini Kenya

Taasisi husika kuchunguza vitabu vinavyotumiwa katika suala zima la ufundishaji. Kutathmini kiwango cha msamiati unaotumiwa na waandishi kama unaafiki kiwango kinachohitajika.

5.4 Hitimisho

Kutokana na utafiti huu, makosa **747** yaliyobainishwa katika matini za watafitiwa yalichanganuliwa kwa kina. Matumizi ya msamiati usiofaa ndilo tapo lilikuwa na idadi kubwa ya makosa (makosa**110** ambayo ni asilimia **14.7**). Tapo la ubadilishanaji wa fonimu lilikuwa na kiwango cha chini cha makosa **17** ambayo ni asilimia **2.3**. Vyanzo vya makosa

husika ni: matumizi ya msimbo wa sheng, ukiukaji wa sheria za lugha ya Kiswahili, matumizi ya lugha ya kishairi na athari ya lugha za kwanza za watafitiwa. Njia za ufundishaji zikiboreshwa makosa ya kisemantiki yatapungua.

Aidha, matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa kuweka wazi sehemu ambazo zinawatatiza wanafunzi katika uandishi wao. Sehemu hizo zitakaposhughulikiwa kwa kina Kiswahili kitaenezwa na kukidhi haja za mawasiliano katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kimazingira na katika sayansi na teknolojia katika ulimwengu huu wa utandawazi.

5. 5 Mapendekezo

Washikadau anuwai wanahitajika ili kuboresha mawasiliano andishi ya Kiswahili. Utafiti huu ulichanganua makosa mbalimbali yanayotinga mawasiliano andishi. Makosa husika yatawasaidia walimu wa Kiswahili katika kupunguza makosa yanayojitekeza katika matini za wanafunzi. Vipengele vya uandishi wa matini anuwai visisitizwe na walimu wa Kiswahili wakati wa ufundishaji. Makosa yashughulikiwe kwa njia ya kipekee kwa kuwa yanatatiza uelewekaji wa ujumbe. Walimu wawapatie wanafunzi kazi nyingi za kuandika shuleni na nyumbani ili kuimarisha mawasiliano andishi.

Ur (1996), anadokeza kuwa wakati wa kurekebisha kazi iliyoandikwa, ni vyema kwa mwalimu kuweka alama zinazostahili katika sentensi, neno, au kiunganishi ili kuonyesha aina ya kosa lililotokea. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wanaweza kujisahihisha wenyewe kwa kuzingatia chanzo cha kila kosa. Kuwepo kwa makosa ni kipengele muhimu kwa yejote anayejifunza lugha ya pili. Hivyo basi, makosa yarekebishwe papo hapo ili kuzuia urudiaji. Mwalimu akosoe makosa yanayotatiza uelewekaji wa ujumbe. Kuyakosoa ni njia moja ya kuwafanya wanafunzi kuelewa namna lugha lengwa hufanya kazi. Marekebisho husaidia kuboresha mawasiliano. Walimu watumie mbinu tofauti katika kufunza na kuandika insha kama vile kuwapa kazi ya makundi, kuwahuisha katika uigizaji na kuandaa mihadhara mbalimbali shuleni. Watumie mbinu zinazowapa wanafunzi motisha kujifunza lugha ya Kiswahili. Ni wajibu wa walimu kuwaelekeza wanafunzi kwenye mchakato wa kuandika matini. Walimu waorodheshe vipengele vinavyowakwaza wanafunzi ubaoni na kusisitiza maana na matumizi ya kila kipengele.

Katika uchanganuzi makosa, walimu lazima watambue chanzo cha kila kosa katika matini za wanafunzi ili kubainisha njia mwafaka za kuyarekebisha makosa husika. Kwa kufanya hivyo, mwanafunzi atajua sheria zinazotawala lugha husika na kuzitumia ili kuepuka makosa yatakayokwamiza uelewekaji wa ujumbe (Keshavarz, 1997). Walimu wafuatilie na kuwakumbusha wanafunzi makosa ya awali ili kuwasaidia kuepuka kuyarudia hayo makosa. Kwa mujibu wa Brown (2000), makosa yashughulikiwe kwa njia ya kipekee kwa kuwa yanatatiza uelewekaji wa ujumbe. Makosa ya wingi, utumiaji wa vibainishi visivyo sahihi na njeo si muhimu kama makosa yanayohusu mpangilio wa maneno katika sentensi. Muhimu katika uchanganuzi makosa ni kurekebisha makosa yanayoathiri mwanafunzi katika uwasilishaji wa ujumbe kiulimwengu kwa kujenga ujuzi wake katika mawasiliano.

Wanafunzi pia wana wajibu katika kuboresha mawasiliano andishi ya Kiswahili. Wanafunzi wasome vitabu vingi vya lugha ya Kiswahili ili kuwa na umilisi wa matumizi ya Kiswahili sanifu. Kwa kufanya hivyo, watafahamu miundo mbalimbali ya sentensi, matumizi ya aina mbalimbali za maneno na nafasi inayostahili kuachwa kati ya neno moja na lingine. Waandike matini mbalimbali kadri wanavyoweza ili kuimarika katika uandishi wao. Wapitie kazi zao wamalizapo kuziandika ili kurekebisha makosa yaliyojitokeza walipokuwa wakiandika kwa haraka. Watumie Kamusi ya Kiswahili sanifu ili kufahamu maana ya msamiati ambao unawatatiza. Pia, watumie lugha sanifu ya Kiswahili katika mandhari na miktadha halisi ili waweze kukuza ufasaha na umilisi wao katika mazungumzo na maandishi. Kwa hivyo, kujifunza kuwasiliana ni kujifunza lugha husika pia. Kupitia mawasiliano au mazungumzo na watu wengine ulimwenguni, mwanafunzi hukuza kaida za muundo na matumizi ya lugha husika. Mazungumzo katika Kiswahili hayana budi kukuzwa shulenii kwa vyovyyote vile kwani huko ndiko muktadha muhimu wa ujifunzaji lugha.

Kwa Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala nchini Kenya, watalie mkazo vipengele vinavyowatatiza wanafunzi katika uwasilishaji wa ujumbe katika mawasiliano andishi ya Kiswahili. Wachunguze vitabu vinavyotumiwa katika suala zima la ufunzaji wa Kiswahili katika shule za msingi na za upili. Watathmini kiwango cha msamiati ambao umetumiwa katika uandishi wa vitabu vya lugha ya Kiswahili ili kuboresha mawasiliano andishi ya Kiswahili.

Vipengele vinavyotatiza mawasiliano andishi ya Kiswahili vilichanganuliwa katika utafiti huu. Waandishi wa vitabu vya Kiswahili wanapaswa kusisitiza vipengele husika katika uandishi wao. Wazingatie mazoezi anuwai katika uandishi wa vitabu vinavyotumiwa katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili hususani vitabu vinavyotumiwa katika viwango mbalimbali vya elimu (katika shule za msingi na za upili).

5.6 Utafiti Zaidi

Utafiti huu ulishughulikia makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili mionganoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Kuna masuala mbalimbali ambayo yanaweza kushughulikiwa kwa kuwa hatukuyashughulikia katika utafiti wetu.

- 1) Utafiti huu ulitumia mawasiliano andishi kama msingi wa kuchanganua makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wa shule za upili. Makosa ya kisemantiki katika mazungumzo hayakushughulikiwa kwa vyovyyote vile katika uchanganuzi huu. Pana haja ya utafiti kufanywa ukilenga athari ya lugha ya mazungumzo kwa lugha andishi.
- 2) Utafiti wetu ulikuwa juu ya makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi kwa wanafunzi wa shule za upili. Utafiti mwagine unaweza kufanywa kuhusu makosa ya pragmatiki ambayo hujitokeza katika mawasiliano andishi. Makosa katika matumizi ya lugha yatawekwa wazi kwa kuzingatia mikitadha mbalimbali. Hali hii itapelekea kueleweka kwa nafasi ya muktadha katika kujitokeza kwa makosa mbalimbali katika matumizi ya lugha ya Kiswahili.
- 3) Makosa katika matumizi ya lugha husababishwa na mambo mbalimbali. Utafiti huu umechananua vyanzo mbalimbali vya makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi. Suala la makosa yanayofanywa na watangazaji wa habari katika runinga au redio laweza kufanyiwa utafiti.
- 4) Utafiti huu ulishughulikia makosa ya kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wa shule za upili katika mawasiliano andishi ya Kiswahili. Utafiti mwagine unaweza kufanywa kuhusu makosa yanayofanywa na walimu wa shule za msingi au za upili katika mazungumzo ama mawasiliano andishi ya Kiswahili.

MAREJELEO

- Abdulaziz, M.H na Osinde, K. (1997). *Sheng and English: Development of Mixed Codes among the Urban Youth in Kenya*. In: International Journal of the Sociology of Language. (Sociolinguistic Issues in Sub-Saharan Africans. Pp 45-63
- AbiSamra, N. (2003). *Analysis of errors in Arabic Speakers' English Writing*. Beirut: American University of Beirut. Retrieved November 18, 2013 from <http://abisamra03.Tripod.com/nada/languageacg-erroranalysis.html>.
- Adam, M. (2000). *Cultural History: Arabic, Hausa na Kiswahili na Unity and Development Natural Seminar of the Teaching of Kiswahili in Uganda*: IUIU. Mbale -10-11- 14200
- Asiba, A. (1985, August 30). *Can Sheng' Stand the Test of Time*. Sunday Nation Nairobi.
- Ashton, A. O. (1944). *Swahili grammar* (including intonation). Singapore: Ban Wah Pte Ltd
- Bakari, M. (1988). *Analysis of Modern Swahili Text and Language Skills*. Nairobi: University of Nairobi.
- Bakari, M. (1982). *The Morphophonology of Northern Swahili Dialects*. Tasnifu ya MA (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Broomfield, G. W. (1975). *Sarufi ya Kiswahili*. Oxford: Oxford University Press.
- Brown, H. D. (1987). *Principles of Language Learning and Teaching*. Retrieved May 10, 2014 From <http://www.google.com>.
- Brown, H. D. (2000). *Contribution of Error Analysis to Foreign Language Teaching*. Retrieved June 21, 2014 from <http://www.google.com>.

- Buliba, A., Nyonje, K. na Mwihaki, A. (2006). *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi: Engilish Press Ltd.
- Buliba, A. Njogu, K. na Mwihaki, A. (2006). *Sarufi ya Kiswahili Uchanganuzi na Matumizi*. Nairobi: Jomo Kenyetta Foundation.
- Chepkwony, L. C. (2011). *Uchunguzi wa Matatizo ya Kisarufi mionganoni mwa Wanafunzi Wa Kikipsigis: Mfano Wilaya ya Bomet*. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.
- Cann, R. (1983). *Formal Semantic*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Chomsky, N. (1987). *Language and Mind*. New York: Harcourt Brace.
- Chomsky, N. (1957). *Syntactic Structures*. S-Gvavenhage (The hague) Netherland: Mouton & Company.
- Corder, S.P. (1967). *The Significance of Learners Errors*. Reprinted in J.C., Richards (Mh) (1974, 1984). *Error Analysis: Perspective on Second Language Acquisition*. London: Longman. Retrieved January 12, 2014 from <http://absamra03.tripod.com/Languageacq-erroranalysis.htm>.
- Cruse, D. A. (1986). *Lexical Semantic*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Dowty, D. R. (1986). *Thematic roles of Semantics*. Dordrect: Reidel.
- Crowley, T. (1982). *An Introduction to Historical Linguistic*. Oxford: Oxford University Press.
- Cruse, D. A. (1986). *Lexical Semantic*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Dulay, H. na Burt, M. (1974). *You Can't Learn Without Goofing*. In J. C Richard (Mh.), *Error Analysis*. London: Longman.
- Eco, U. (1976). *A Theory Semiotic*. Bloomington: Indian University Press.

- Ellis, R. (1994). *The Study of Second Language Acquisition*. Oxford: Oxford University Press.
- Fauconnier, G. (1997). *Mapping in Thought and Language*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Fries, C. (1945) *Teaching and Learning English as a foreign language*. Ann Arbor: University of Michigan Press. Retrieved December 28, 2013 from eng.hzu.edu.cn/upload.doc.
- Furaha, S. (2001). *Makosa ya Kisintaksia katika Ujifunzaji wa Kiswahili: Mfano Kutokana na Wanafunzi wa Ikolomani wilaya ya Kakamega*. Tasnifu ya Ph.D (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Gass, S. na Selinker, L. (1994). *Second language Acquisition: An introductory course in N*. AbiSamra (2003) *An Analysis of Errors in Arabic Speakers' English Writings*. Retrieved October 19, 2013 from [htt://absamra03.tripod.com/Languageacq-erroranalysis.htm](http://absamra03.tripod.com/Languageacq-erroranalysis.htm).
- Griffiths, P. (2006). *An Introduction of English Semantic and Pragmatic*. Edinburgh University Press.
- Githiora, C. (2002). Sheng: Peer Laguage, Swahili Dialect or Emerging Creole? In: *Journal Of African cultural Studies*, 15,2,159-18
- Gouala, P. M. (1991). *Problems of Learning English in the Congo due to Mother Tongue Interference*. Shahada ya P.G.D.E (Isiyochapishwa) University of Nairobi.
- Habermas, J. (1979). *What is Universal Pragmatics?* Trans. Thomas McCarthy, *Communication And Evolution of Society*. BOSTON: Beacon, 1-68.
- Habwe, J. H. na Karanja, P. (2003). *Misingi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Halliday, M. A. K. (1966). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Edward Arnold.

Harmer, S. (1998). *A contribution of Error Analysis to Foreign Language Teaching*.

Retrieved June 21, 2014 from <http://www.google.com>.

Haroon, M. (1998). *Kuathirika kwa Kiswahili na Kigisu Nchini Uganda Kifonolojia, Kimofolojia, Sintaksia na Utamaduni*. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa) Kampala University Press

Heim, I. (1989). *Semantics in Generative Grammar*. Oxford: Blackwell

Iraki, F.K. (2004). ‘*Cognitive Efficiency: The Sheng Phenomenon in Kenya*’. International Pragmatics Association 14:1.15=68

Jackendoff, R. (1990). *Semantic Structure*. Cambridge MA: MTT Press.

James, C. (1998). *Errors in Language Learning and Use Exploring Error Analysis*. Harlow: Longman.

Jie, S. (2010). *Study of Errors in Chinese English MajorsEnglish Majors’ Writing*.

Retrieved June 29, 2014 from <http://ccsenet.org/ass>

Kariuki, M. (2000). *Aspects of syntactic Information Packing*. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa), Egerton University, Kenya.

Katz, J. (1986). *Common Sense in Semantic. New Directions in Semantic*. Ed. By E. Lapore 159-235, New York. Academic Press.

Kembo, S. (1996). *Language Attitude, Use and Proficiency. A Sociolinguistic Study of English in Kenya*. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa) . Moi University.

Kempson, R. M. (1976). *Semantic Theory*. Cambridge: Cambridge University Press.

Keshavarz, M. H. (1997). *Contribution of Error Analysis to Foreign Language Teaching*.

Retrieved June 21, 2014 from <http://www.google.com>.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B. na Msanjila, Y. P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili*

Sanifu Sekondari na Vyuo (SAMAKISA). Dar es Salaam: TUKI.

Kivuna, S. M. (1992). *Nuru ya Ushairi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

K.I.E. (2000). *Guidelines of Early Childhood Development in Kenya*. Nairobi: National Centre For Early Childhood Education.

Laufer, J. (1997). *Some Properties of the Language Learner's Lexicon as Evidenced by Lexcal Confusion*. IRAL, 29 (4), 317-330.

Lass, R. (1984). *Phonology. An Introduction to Phonology*. Cambridge: Cambridge University Press.

Lennon, P. (1991). *Errors: Some Problems of Definition, Identification, and Distinction in applied Linguistics*. Retrieved June 11, 2014 from <http://dx.doi.org/10.1093/applin/12.2.180>.

Lengo, P. E. (1995). *Contribution of Error Analysis to Foreign Language Teaching*. Retrieved June 21, 2014 from <http://www.google.com>.

Lakoff, G. (1988). *Cognitive Semantic. Meaning and Mental Representation*. Bloomington: Indian University Press.

Llach, M. P. (2005). *The Relationship of Lexical Errors and their Types to Quality of ESL Compositions: An Empirical Study*. Portal Linguarum, 3. 45-57.

Lott, C. M. (1983). *The Second language Acquisition*. Retrieved 28, 2014 from <http://www.cds.eun.eg/en.htm>.

- Lynon, J. (1963). *Introduction to Theoretical Linguistic*. Cambridge: Cambdrige University Press.
- Mangwa, D. O. (2004). *Athari za Ekegusii katika Kiswahili na Zilivyochangia Matokea Mabaya ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili kwa Wanafunzi Wakisii Wilaya ya Kisii Kusini Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kiku cha Egerton, Kenya.*
- Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M. na Msanjila, Y. P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbaabu, I. (1978). *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Nairobi: KLB.
- Mbaabu, I. (1985). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: KLB
- Mbaabu, I. (1995). *Usahihishaji wa Makosa katika Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Press.
- Mbula, J. E. (2011). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kikamba: Mfano wa Wilaya ya Kitui*. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mbwesa, K. J. (2006). *Introduction to Management Research*. A study Handbook. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mdee, J. S. (1986). *Kiswahili Muundo na Matumizi yake*. Dar es Salaam: International Publishers, Ltd.
- Mekacha, R. D. (2011). *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Longhorn Publishers.

Michira, N. O., Iribemwangi, P. I. na Mbatia, M. (2014). *Ukuzaji wa Kiswahili*. Nairobi: Printwell Industries Ltd.

Moshi, M. (1971). *Loan Words in Luganda: A Search for Guide in Adaption of African Language to Morden Cordination*: In Whiteley W.H. led Language Use and Social Chicago. International African Institute London: Oxford University Press.

Muaka, L. (2009). *The Dynamics of Language Use Among Rural and Urban Kenyan Youths*. Tasnifu ya Ph.D (Isiyochapishwa), University of Illionois.

Muchome, H. S. S. (1998). *The Impact of English on Ethnic Community Language in Tanzania Acase tudy of Cinamwanga*. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa).

University of Paris.

Mugenda, O. M. na Mugenda, A. G. (1999). *Research Methods: Quantitative & Qualitative Approches*. Nairobi: Acts Press

Mukuria, D. M. (2002). *Tathmini ya Vigezo Vinavyotumiwa Kufundishia Ngeli za Kiswahili Katika utafiti wa Kiswahili Simala* K. Nyala (Mh) Moi University.

Mukuthuria, M. (2004). *Kuathiriana kwa Kiswahili Kimeru: Mfano kutokana na wanafunzi wa Kitigania*. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton.

Murioki, P. W. (2012). *Uchanganuzi wa Makosa katika Ufahamu na Ufupisho kwa Wanafunzi wa shule za upili. Mfano wa Kaunti ya Isiolo*. Tasnifu ya M. A. (isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

Muthu, K. F. (2005). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kisintaksia katika Tafsiri za Magazeti (Taifa Leo)*. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

- Mutungu, B. N. (2001). *Makosa ya Kileksia katika Insha na Chanzo chake: Uchanganuzi Wa Shule tano za Upili wilanyani Kiambu*. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.
- Mwangi, J. N. (2011). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kimofo-sintaksia katika Kiingereza: Mfano Kutokana na Wanafunzi jijini Nairobi*. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Nabea, W. (2009). *The Journal of Pan African Studies*, Vol 3, September 1, 2009. Kenya: Negotiation with Hegemony. University of Vienna Austria.
- Nabhany, S. A. (1987). *Malenga wa Karne Moja*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.
- Newmey, F. J. (1993). *Grammatical Theory. Its Limits and Its Possibilities*. Chicago University : Chicago Press.
- Njoroge, K. (1987). *The Acquistion of Six Morphosyntactic Structure of Engilish by Kenya School Children* Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa), University of Edniburgh.
- Nurse, D. (1980). *Bantu Migration into E.A. A Liguisti Evidence of Paper No 138* (Isiyochapishwa) Institute of African Studies (AS) University of Nairobi.
- Noor, H. (1996). *English Syntactic Errors Committed by Arabic Speaking Learners of English*. King Abdulaziz University, Educational Science. Scientific Publishing Centre, 1441-1465
- Norrish, J. (1983). *Language Learners and their Errors*. Macmillan: Macmillan Press.
- Obeidat, H. (1986). *Syntactic and Semantiki Errors*. In James (1998). *Errors in Language Learning and Use Exploring Error Analysis*. Harlow: Longman.
- Obuchi, S. M. na Mukhwana, A. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele*.

- Nairobi: A~Frame Publishers.
- Ogechi, N. O., Shitemi, N. L. na Simala, K. I. (2008). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.
- Ogechi, N. O. (2002). *Trilingual Codeswitching in Kenya: Evidence from Ekegusii, Kiswahili English and Sheng*' Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa). Hamburg: University of Hamburg.
- Ontieri, J. O. (2010). *Uchanganuzi wa makosa katika insha za wanafunzi wa shule za Upili: Mfano wa wilaya ya Nakuru, Kenya*. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Ontieri, J. O. (2011). Tafsiri Sisisi na Athari zake katika Mawasiliano. Katika P. S. Malangwa na L. H. Bakize (Wah.), *Jarida la Kioo cha Lugha*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Onyango, J. O. (1997). *Uziada wa Kisarufi katika Kiswahili cha Wanafunzi wa Kinyala Mtazamo wa Uchanganuzi Linganuzi*. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Patricia, G. E. (1990). *A Study of the Word Structure and Processes Involved in Word Formation in Sheng*' A Case Study of Eastland Area Nairobi. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.
- Pearsall, T. E. na Cunningham, D. H. (1988). *The Fundamentals of Good Writing*. New York: Macmillan Publishers.
- Penny, K. W. (2001). *An Analysis of Students Errors Pattern in Written English. Suggested Teaching Procedures to Help*. Retrieved January 20, 2014 from http://www.cels.bham.ac.uk/resources/essays/penny_2.pdf.

- Richards, J. C. (1974). *Error Analysis and Second Language Strategies*. In J. H. Schumann and N. Stenson (Wah.), *New Frontiers in Second Language Learning*. R Rowley. Mass: Newbury House
- Rono, M. (2012, July 20). We Should Arise and Save Kiswahili. *The People*: Nairobi.
- Patton, M. Q. (2001). *Qualitative Research Methods*. Thousands Oaks CA: Sage Publication.
- Pontner, P. (2005). *What is Meaning? Fundamentals of Formal Semantic*. Malden, MA: Blackwell.
- Ryanga, Sheila, C. W. A. (2000). Umuhimu wa Lugha za Kienyeji katika Uendezaji wa Kiswahili. *Makala Iliyowasilishwa katika Kongamano la Kimataifa Lililoandaliwa na CHAKITA*, Oktoba 3-06-2000 Mombasa: Kenya.
- Saeed, J. I. (2009). *Semantics*. Hong Kong: Graphic Limited.
- Schane, S. (1973). *Linguistic Change and Generative Phonology*. Oxford: Oxford University Press.
- Spada, N. na Lightbourn, P. M. (1999). *How Languages are learnt*. Oxford: Oxford University Press.
- Sridhar, S. N. (1981). katika Fisiak (Mh.) *Constrastive Linguistic and Language teacher*. Oxford: Pergamon. Retrieved May 30, 2014 from <http://www.unb.br/let/graham/conon/htm>
- Ur, L. S. (1996). *Contribution of Error Analysis to Foreign Teaching*. Retrieved June 21, 2014 from <http://www.google.com>.
- Talmy, L. (2000). *Towards A Cognitive Semantc*, 2 Vol 5. Cambridge (MA) MIT. Press.
- TUKI (2004). *Kamus ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

- Turner, M. (2006). *The Literary Mind*. Oxford: O.U.P.
- Tyler, A. na Evans, V. (2003). *The Semantic of English Prepositions: Spatial Scenes Embodied Meaning and Cognition*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Wanyoike, E. N. (1978). Vikwazo katika Mafunzo ya Kiswahili Kenya katika Lugha Vol5 No3. Nairobi: *Kenya Language Association*.
- Weiss, H. Carol. (1972). *Evaluation Research*. Edgewood Cliiffs, New Jersey: Prentice-Hall.
- William, M. (1992). *Linguistic Semantic*: Lawrence Eryburn Association Publishers: Nee Jersey.
- Wilkins, R. (1972). *The SecondLanguage Acquisition*. Retrieved 28, 2014 from <http://www.cdc.eun.eg/en.htm>.
- Wyrick, J. (1979). *Steps to Writing Well: Aconcise Guide to Composition*. New York|: Holt, Rinehart & Winston.
- Zimmermann, R. (1986). Semantic and Lexical Errors Analysis. *English Amerikasche Sudien*, 2 (86), 294-305.

KIAMBATISHO 1: HOJAJI

Dhamira kuu ya hojaji hii ni kukusanya data kwa minajili ya kufanikisha utafiti tu.

Tafadhalitoa jibu sahihi katika sehemu hii ifuatayo:

1. Jina lako-----

2. Mahali pa kuzaliwa-----

3. Mahali unakoishi-----

4. Lugha yako ya mama (kwanza)-----

5. Taja lugha zingine uzijuazo-----

6. Je, unaweza kujieleza kwa lugha ya kwanza kwa ufasaha.....
7. Lugha ya Kiswahili inazungumzwa shulen? Ndio au la-----

Fafanua jibu lako-----

- 8.Je unapenda somo la Kiswahili?
- Fafanua jibu lako.....

KIAMBATISHO 2: MJARABU

Muda: SAA MOJA

Tafadhali jibu maswali yote

a) Tunga sentensi moja yenye muundo ufuatao:

Kiima, kiarifu, kitondo, kipozi,ala

b) Tunga sentensi zitakazobainisha maana ya jozi za maneno zifuatazo:

Mbari

Mbali

c) Tunga sentensi zinazodhahirisha ngeli za nomino hizi:

Kifaranga

Sukari

d) Tumia maneno yafuatayo katika sentensi:

Papa

Baba

Sabuni

Zabuni

e) Tunga sentensi nne zikionyesha maana za neno **chungu**.

f) Tunga sentensi mbili tofauti ukitumia vitenzi hivi vya silabi moja:

i) Pa-----
-

ii) La-----

g) Tumia kivumishi cha **sifa** katika sentensi.

2. Kwa maneno 200-250 fafanua umuhimu wa magazeti kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

KIAMBATISHO 3:MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA MJARABU

SEHEMU YA KWANZA

Utungaji wa sentensi

a) Kiima- kitu ama mtu ambaye husababisha kitendo kifanyike.

-hujaza nafasi ya mtenda (mtendwa) katika sentensi.

Kiarifu- sehemu ya sentensi ambayo hufahamisha kitendo kinachoteklezwa na kiima.

Kitondo- nomino ya kitu au mtu wa tatu anayefanyiwa jambo.

Kipozi- nomino ya mtu ama kitu ambacho hupokea pigo ama uzito wa tendo katika sentensi.

Ala – chombo ambacho mtu hukitumia kutenda kazi.

b) Mbari- watu wa kitivo kimoja: jamii, kabilia, ukoo.

Mbali- masafa marefu baina ya mahali na mahali

c) Kifaranga- kiumbe chenye uhai- Ngeli ya A-WA

Sukari- nomino ambazo hazihesabiki- ngeli ya I-I

d) Papa- msisitizo wa mahali hapa.

-samaki mkubwa wa baharini aliye na magamba kwenye ngozi.

- moyo kwenda kwa haraka bila kufuata mapigo ya kawaida.

- kiongozi Mkuu wa kanisa katoliki duniani

Baba- mzazi mwanamume

- Mvulana aliyefika umri wa ubarubaru

- jina la heshima na upendo.

e) Sabuni- mchanganyiko wa vitu vinavyotakana na mafuta na aina mojawapo ya magadi na

ambayo hutumiwa kwa kuvulia ama kuogea au kusafishia vitu.

Zabuni- uza kwa kushindania bei.

-tia thamani.

-utaratibu wa kuuza au kununua vitu, bidhaa au huduma kwa muda maalumu.

f) Chungu- siokuwa tamu, siokuwa na ladha, kali.

-chombo kilichofinyangwa kwa udongo na kitumiwacho kwa kupikia

- mdudu mdogo mweusi wa jamii moja na mchwa, siafu, sisimizi

-kipele, chunusi, kibuja

-idadi kubwa, wingi

g) Pa-Kitenzi- kabidhi mtu kitu -pea, -pewa, -peana, -peka, n.k.

La- Kitenzi- tia chakula mdomoni na kumeza -lia, -lika, -lisha,-liana, -liwa, n.k.

h) Sifa- uzuri au ubaya wa mtu au kitu

Kivumishi- neno linalotoa maelezo zaidi kuhusu nomino

Sentensi (a-g) zionyeshe maana zilizotolewa hapo juu.

KIAMBATISHO 4: MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA INSHA

Insha imedhamiriwa kutahini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi. Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa. Kwa mfano, kutunga sentensi sahihi zenyetutiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yenye mawazo asilia, ubunifu mwingi, na hati nadhifu. Kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha ni lazima kutilia mkazo, mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo.

SARUFI

Sahihisha kwa makini sana ukionyesha makosa yote yanayotokea. Makosa ya sarufi huwa katika:

- ✓ Kuakifisha vibaya: vikomo, viyuo, alama za kuuliza, alama hisi n.k
- ✓ Kutumia herufi ndogo au kubwa mahali si pake.
- ✓ Matumizi mabaya ya ngeli na viambishi, nyakati, vihusishi, muundo mbaya wa sentensi na mnyambuliko wa vitenzi na majina.
- ✓ Kuacha au kuongeza neno katika sentensi.

MAKOSA YA HIJAI

Haya ni makosa ya maendelezo. Makosa ya hijai hutokana na:

- ✓ Kutenganisha neno kama vile aliye kuwa
- ✓ Kuunganisha maneno kamavile
- ✓ Kukata silabi visivyo kama vile lim-a
- ✓ Kuandika herufi isiyofaa katika neno kama mahari badala ya mahali
- ✓ Kuacha herufi katika neno kama alieiba badala ya aliyeiba
- ✓ Kuongeza herufi isiyofaa katika neno kama, piya badala ya pia
- ✓ Kuacha alama inayotarajiwa kuwepo katika herufi
- ✓ Kutoandika kistari cha kuunganisha neno ufikapo pambizoni au mwisho au kuandika mahali si pake
- ✓ Kuandika kistari pahali pasipofaa

- ✓ Kuacha ritifaa au kuiweka pasipofaa
- ✓ Kuandika maneno kwa kifupi, mfano k.m, n.k

MTINDO

Mambo yatakayochunguzwa

- ✓ Mpangilio wa kazi kiaya
- ✓ Utiririko wa mawazo
- ✓ Hati nzuri inayosomeka kwa urahisi
- ✓ Namna anavyotumia methali, misemo, tamathali za semi na mengineyo
- ✓ Kuandika herufi kama Jj, Pp, Uu n.k

MSAMIATI

- ✓ Jumla ya maneno yaliyotumiwa kuafikiana na mada au kichwa kilichopendekezwa.

MAUDHUI

- ✓ Baada ya kusoma insha utafikiria maudhui na msamiati uliomo kwa jumla.

ALAMA ZA KUSAHIHISHIA

= hupigwa chini ya sehemu zmbayo kosa la sarufi limetokeza kwa mara ya kwanza tu.

- hupigwa chini sehemu au neno ambako kosa la hijai limetokeza kwa mara ya kwanza tu.

^ hutumiwa kuonyesha kuachwa kwa neno.

- ✓ Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe X hutumiwa kuonyesha msamiati usiofaa. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe.